# Nipashe

Jumatano Agosti 21, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580002

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





Kunahitajika chombo kitaifa kuratibu shughuli za serikali

Kimataifa

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Waandamana sababu ya ukosefu wa usalama Mashariki ya DRC

BAADA YA MIAKA 55

Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-10

JPM alivyofanikisha kampeni ya Kiswahili kuwa lugha ya SADC

India yapimana nguvu na Pakistan

Ukurasa 20

## Shahidi adai kortini wafuasi Chadema hawakuwa na silaha

UKURASA 2

UKURASA 13

RIPOTI MAALUMU

# Samaki wa mabomu wanavyoeneza kansa

• **Wataalamu** waeleza mbinu za kuwabaini, wavuvi wanaokatwa mikono na mabomu wasingizia kushambuliwa na samaki wakali...*Endelea uk.4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MUME ASHIKILIWA KWA TUHUMA MAUAJI YA MKE**

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha linamshikilia dereva wa kampuni ya utalii ya Mt Kilimanjaro...

UKURASA WA 7

**UHALIFU MKUBWA SASA WAPUNGUA**

SERIKALI imesema katika kipindi cha miezi sita kuanzia Januari, wamefanikiwa kupunguza...

UKURASA WA 7

**JAJI KIONGOZI AFUNGUKA KUCHELEWA KWA MASHAURI**

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, amewataka wananchi na...



Msongamano wa wananchi wakisubiri kupata huduma ya vitambulisho vya taifa katika ofisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Kawe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mkurugenzi kortini madai ya kughushi

UKURASA 3



## Makonda akomalia matapeli wa ndoa

UK. 2

MICHEZO **MANARA AFUNGUKA KUTEMWA SIMBA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Makonda akomalia matapeli wa ndoa

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema sakata la wanaume wanaoahidi kuoa wanawake kisha wanawatelekeza, amelihamishia kwenye mjadala wa pamoja ili kupata suluhu ya kudumu ikiwamo kuwafikisha wahusika mahakamani.

Makonda alisema hayo jijini Dar es Salaam jana, huku akimtaja msanii mmoja maarufu nchini (jina tunalihifadhi), kuwa ni miongoni mwa wanaofanya vitendo hivyo.

Alisema wataanzisha mjadala utakaorushwa mubashara kupitia vyombo mbalimbali vya habari ili wananchi wapate fursa ya kutoa maoni yao kwa sababu ni tatizo ambalo kwa sehemu kubwa linachochea ongezeko la watoto wa mitaani na mmomonyoko wa maadili.

Alisema amepitia baadhi ya vifungu vya maneno ya Mungu katika Qu'ran tukufu na Biblia takatibu ambavyo vyote vinaeleza kuhusu wanaume au wanawake wanaowalaghai wenzao.

"Mjadala unakuja, tujipange, najua wapo marafiki zangu wengi ambao kimsingi wana 'promise' (wanaahidi) kuoa akiwamo (anamtaja msanii huyo), wanaahidi tu kuoa, sasa tujipange inawezekana siku moja wote walioahidiwa kuolewa wakaenda mahakamani," Makonda alisema.

Alisema suala hilo linaathiri watu wengi zaidi na kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kifungu cha 69, 70 na 71 ni kosa kisheria kuachana na mwanamke uliyeahidi kumuoa na hata zawadi uliyompa mtu wakati wa uhusiano unaweza kwenda kuidai mahakamani.

Alisema suala hilo halifungamani na matakwa ya sheria za dini zinazoruhusu wengine kuoa hadi wanawake wanne, bali ajenda muhimu ipo kwenye kuwapotezea muda wadada ambao pengine wangeweza kuwa na familia zao.

Makonda alisema matokeo ya tabia hiyo iliyokithiri zaidi katika jiji hilo, ni kusababisha ongezeko la watoto wa mitaani, yatima, mmomonyoko wa maadili na ombaomba.

Alisema kama wananchi wataona hakuna haja ya kuingilia suala hilo, hakutakuwa na haja ya kumuhoji kuhusu ongezeko la watoto wa mitaani na mmomonyoko wa maadili kwa sababu kuharibika kwa mahusiano ndio msingi wake.

"Hawakatazwi watu kuoa wake na dini nyingine, zinaruhusu watu kuona wake wengi na hata kama unataka kuona wanawake hata 800 wewe oa, lakini tunachokataza ni kuwapa ahadi wadada wa watu na kuwapotezea muda wao wakati wakijiandaa kuolewa na mwisho wa siku anamuacha akiteseka," Makonda alisema.

Alisema wanawake wanaofanyiwa vitendo hivyo huishia kuwachukia wanawake, kutokuwa sawa kazini, kuchukua maamuzi ya kuwaumiza, kuathiri utendaji kazi na kuharibu kabisa maisha yao.

Alisema wapo wanaume waliosababisha wanawake watoe mimba, waliowazalisha wanawake, lakini wamewaachia watoto ambao wanalea wenyewe.

INAENDELEA UK.8



Rais John Magufuli akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Kitengo cha Sayansi Jinai, Biolojia na Vinasaba, Hadija Saidi Mwema, alipotembelea Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk.26. **PICHA: IKULU**

## Mume ashikiliwa kwa tuhuma za mauaji ya mke

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha linamshikilia dereva wa kampuni ya utalii ya Mt Kilimanjaro Safari's, Julius Kabora (45), kwa tuhuma za mauaji ya mke wake Rehema Elihudi (31)mkazi wa Kijiji cha Saitabahu wilayani Arumeru mkoani hapa.

Akithibitisha jana ofisini kwake kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema Rehema alikutwa chumbani kwake akiwa sakafuni Agosti 19,

INAENDELEA UK.8


MASETO COMPANY LIMITED

**NOTISI/TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini kwenye jedwali;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | FREDRICK BASIL MRAMBA | FREDRICK BASIL MRAMBA | NYUMBA NA KIWANJA CHA UKUBWA WA SQM 3111 KILICHOPO MAPINGA – BAGAMOYO (ENEO ZURI KWA KUWEKA KITUO CHA MAFUTA AU BIASHARA NYINGINE. KIPO BARABARANI KINA HATI | 04/09/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | MARIA MPUMAJE MWAMLIMA(TAWI LA TEMEKE) | MARIA MPUMAJE MWAMLIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO KITONGOJI CHA MLAMLENI - WILAYA YA MKURANGA | 05/09/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 003 | PAULO GIRIMBE RAWE (TAWI LA BUGURUNI) | PAULO GIRIMBE RAWE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO KEREZANGE KIVULE- WILAYA YA ILALA | 09/09/2019 SAA 08:00 MCHANA |
| 004 | SAID AKILIMALI KALILWA (TAWI LA UBUNGO) | SAID AKILIMALI KALILWA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA MWASONGA – WILAYA YA KIGAMBONI | 11/09/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 005 | RAHMA AMIN NOFLI | RAHMA AMIN NOFLI | KIWANYA KILICHOENDELEZWA KILICHOKO SOMANGILA – WILAYA YA KIGAMBONI | 11/09/2019 SAA 08:00 MCHANA |
| 006 | JEMIMA PAUL SELEMANI (TAWI LA BUGURUNI) | MARCO MWITA MARCO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA MALELA– WILAYA YA KIGAMBONI | 13/09/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 007 | THE CHAMPIONS TANZANIA (TAWI LA KINONDONI) | MARIA RAPHAEL STEPHANO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO KINYEREZI – WILAYA YA ILALA | 16/09/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |

**Masharti ya Mnada**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo na mahali iliko.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NA:**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 669,
DAR ES SALAAM
Tel+255 02221183403

AU

Maseto Auctioneer,
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 75087,
DAR ES SALA
+255 765 999 000 AU +255 787 288 442 AU
+255 762 260 787

215383202


## Shahidi adai kortini wafuasi Chadema hawakuwa na silaha

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa Sita, Koplo Charles, katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, amedai mahakamani kwamba wakati anarekodi picha za video katika mkutano, hakuona wafuasi wa chama hicho wakiwa wameshika silaha ya aina yoyote.

Kadhalika amedai kuwa hakuona wafuasi wa Chadema wakiwashambulia askari polisi wakati akirekodi picha za video katika mkutano wa kufunga kampeni Februari 16, mwaka jana, uliokuwa unafanyika viunga vya Buibui, Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Shahidi alitoa madai hayo jana wakati akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya wakili Kibatala na **shahidi:**

**Wakili:** Shahidi Koplo ni cheo cha ngapi katika Jeshi la Polisi?

**Shahidi:** Cheo cha tatu.

**Wakili:** Ile video ambayo uliirekodi na mahakama imeiangalia, kuna mahali inaonyesha tarehe ya tukio iliporekodiwa?

**Shahidi:** Mheshimiwa Hakimu, kielelezo kinajieleza kimerekodiwa lini na wapi.

**Wakili:** Kielelezo kimeonyesha tukio lilifanyika lini na sahihi?

**Shahidi:** Kielelezo kinajieleza washtakiwa walikuwa katika tukio gani na kabla sijaanza kuongoza kuonyesha picha zake. Nilisema mahakamani.

**Wakili:** Wakati unarekodi picha za video uliwaona wafuasi wa Chadema wakiwa na silaha ya aina yoyote kama vile, mapanga, visu, mawe au marungu?

**Shahidi:** Sikuwaona wafuasi wa Chadema wakiwa na silaha.

**Wakili:** Je, uliwaona wafuasi wa Chadema wakiwashambulia askari polisi?

**Shahidi:** Hapana sikuwaona.

**Wakili:** Je, ni kweli Rais Jacob Zuma wa Afrika ya Kusini ajiuzulu au alilazimishwa kama alivyosema Mbowe?

**Shahidi:** Hapana mimi sifahamu.

**Wakili:** Kama kweli alijiuzulu kama alivyosema Mbowe, je, kuna kosa gani la jinai?

**Shahidi:** Ni kosa kulingana na wapi alipozungumzia na mazingira ya mkutano.

**Wakili:** Kauli ya Mbowe kuhoji Magufuli (Rais Dk.John Magufuli) ni nani ni kosa la jinai?

**Shahidi:** Mimi sifahamu kwa sababu si mpelelezi wa kesi hii.

**Wakili:** Una uhakika kama Mbowe anafahamu kama Magufuli ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**Shahidi:** Mbowe na Watanzania wengine wote tunafahamu Magufuli ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Wakili:** Mbowe alisema Magufuli ni mwepesi kama karatasi kuna tatizo kwa kutoa kauli hiyo?

**Shahidi:** Mimi kama ofisa wa polisi kauli hiyo niliiona si sahihi katika mazingira yale.

INAENDELEA UK.8

## HABARI KITAIFA

# Mkurugenzi kortini madai ya kughushi

**Na Hellen Mwango**



MKURUGENZI Msaidizi wa Maendeleo ya Vijana wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Ester Liwa (pichani), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na mashtaka 22 ikiwamo kughushi, kutumia nyaraka za uongo kwa lengo la kumdanganya mwajiri, ubadhirifu na ufujaji wa zaidi ya Sh. milioni tano.

Alisomewa mashtaka yake katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Vick Mwaikomba.

Wakili wa Serikali, Pascal Magabe, alidai kuwa kati ya Machi 11 na Juni 30, 2015 mshtakiwa alitenda makosa hayo katika ofisi za wizara hiyo.

Ilidaiwa kuwa, katika shtaka la kwanza hadi 16, kwa nia ovu mshtakiwa alighushi nyaraka yenye kichwa cha habari 'Posho ya Kujikimu' kwa maofisa wa wilaya.

Ilidaiwa kuwa alighushi nyaraka hiyo kwa lengo la kuonyesha watumishi hao walihudhuria mafunzo ya uhamasishaji kwa vijana yaliyofanyika mkoani Singida kati ya Machi 11 - 19, 2015 na kwamba walilipwa Sh. 32,500 kila mmoja wakati akijua si kweli.

Katika shtaka la 17 mpaka 20, mshtakiwa huyo alighushi hati ya malipo ya waandishi wa habari iliyoonyesha Festo Sanga wa Redio Standard Fm, amelipwa jumla ya Sh. 1,030,000 na Emmanuel Michael Sh. 100,000 kama malipo ya kuhudhuria mafunzo hayo.

Liwa pia anadaiwa kughushi hati ya malipo ya jumla ya Sh. 405,000 akionyesha maduka ya vifaa vya ofisi ya Mwaji na Temo, yalilipwa kiasi hicho cha fedha kama gharama ya vifaa vilivyotumika katika mafunzo hayo.

Wakili huyo wa serikali alidai, Juni 25, 2015, akiwa ofisi za Wizara ya Habari, alitumia nyaraka za kughushi Sh. 11,177,000 zilitumika katika kipindi cha mafunzo hayo ya vijana mkoani Singida.

Ilidaiwa kuwa kati ya Machi 11 hadi Juni 30, mwaka 2015, mshtakiwa huyo alifanya ubadhirifu na ufujaji wa Sh. 5,425,000, alizokabidhiwa na wizara hiyo kwa lengo la kufanya mafunzo hayo mkoani Singida.

Mshtakiwa alikana mashtaka hayo. Upande wa mashtaka ulidai kutokamilisha upelelezi na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kesi hiyo.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 3, mwaka huu, mshtakiwa alirudishwa rumande baada ya kushindwa kutimiza sharti la kuwa na wadhamini wawili kutoka taasisi inayotambulika watakaosaini bondi ya Sh. milioni 30.

# Jafo ataka watumishi afya waliohamishwa kurejeshwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ametengua uhamisho wa watumishi saba wa Kituo cha Afya Ipogolo mkoani Iringa waliohamishwa kwa madai ya usimamizi mbovu wa fedha.

Watumishi wao wa idara ya fedha waliohamisha hivi karibuni, wameamuriwa kurejeshwa mara moja katika kituo chao cha kazi.

Jafo alitoa agizo hilo jana kwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Nyamhanga, alipokuwa akifungua mkutano wa siku tano ya waganga wakuu wa mikoa na wilaya, unaofanyika jijini hapa.

Alisema kumekuwa na tabia ya uonevu inayofanywa na waganga wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na wakuu wa vituo hivyo vya afya na kuwahamisha hamisha kwenye vituo vya kazi watumishi jambo ambalo linawafanya wapoteze morali ya kufanya kazi.

"Hatuwezi kulea mambo ya ovyo yanayofanywa na baadhi ya waganga wakuu wa wilaya kwa kuonea watumishi. Hawa watumishi wanajituma usiku na mchana bila kuchoka ili usipatikane mwanya wa kufanya ubadhirifu wa mapato ya serikali," alisema.

Waziri Jafo pia alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainabu Chaula, kufuatilia suala la mganga mkuu wa Wilaya ya Bumbuli mkoani Tanga kubaini sababu za kuhamishwa kwake ili kujua kama amehamishwa kwa kushindwa kufanya kazi au majungu.

"Huyo mganga mkuu alikuwa anafanya kazi yake kwa moyo, lakini hivi sasa ameondolewa kazini. Sasa nataka ufuatilie, je, ameondolewa kwa makosa yake au nini kimetokea? Fuatilia unipe majibu," alisema.

Kuhusu ujenzi wa vituo vya afya, Jafo alisema vituo 352 viko katika hatua mbalimbali na kati ya hivyo, 304 vinakusudiwa kutoa huduma za dharura na upasuaji.

INENDELEA UK. 8


**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

# SALAMU ZA PONGEZI

Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF tunaungana na Watanzania kukupongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **MHE. DKT. JOHN POMBE MAGUFULI** kwa kuchaguliwa kuwa **Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)**. Tunaahidi kuendelea kutekeleza majukumu ya kupambana na umaskini ambayo ni moja ya ajenda kuu za SADC katika kuboresha uchumi na maisha ya wananchi wa eneo hilo



SADC KWA MAENDELEO YA VIWANDA



**PAMOJA TUONDOE UMASKINI**

Mkurugenzi Mtendaji,
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**
Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete,
S.L.P 2719, Dodoma, TANZANIA,
Simu:**+255 26 2963866**, Nukushi:+255 26 2963871,
Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**, Tovuti: **www.tasaf.go.tz**



Samaki wanaovuliwa kwa kutumia mabomu wametajwa kusababisha saratani kwa walaji.

# Namna kubaini samaki aliyevuliwa kwa bomu

**Na Gwamaka Alipipi**

SAMAKI ni kitoweo maarufu nchini. Kwa mujibu wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kwa wastani kila Mtanzania anakula samaki kilo 8.2 kwa mwaka.

Mbali na kuvua kwa ajili ya matumizi ya ndani, Tanzania pia husafirisha samaki kwenda nje ya nchi na kuwauza kwa mabilioni ya shilingi.

Kwa mujibu wa Mpina, katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka 2018/19 (kuanzia Juni 2018 hadi Machi mwaka huu), tani 38,114.72 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 46,098 wenye thamani ya Sh. bilioni 491.15 waliuzwa nje ya nchi.

Umaarufu wake, kupendwa kwake katika milo ya kaya aina zote nchini, husababisha mahitaji ya kitoweo cha samaki kuwa juu siku zote.

Hali hiyo imevutia wajasiriamali wengi ambao wamewekeza katika biashara hiyo kwa kujua kwamba soko ni la uhakika.

Hata hivyo, changamoto iliyoibuka ni kuwapo kwa baadhi ya wavuvi wanaotaka faida ya haraka, wakitumia njia haramu kuvua samaki kwa kutumia mabomu.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe katika baadhi ya maeneo yanayotumika kwa uvuvi kwenye Bahari ya Hindi, umebaini uvuvi huo haramu hufanyika kwa usiri mkubwa na una athari kubwa kwa walaji wa samaki na mazingira.

Katika uchunguzi wake huo, Nipashe pia imebaini vilipuzi hivyo hupatikana kwa njia haramu kutoka maeneo ya uchimbaji madini, utengenezaji barabara na wakati mwingine wavuvi huvitengeneza nyumbani.

Ofisa Uvuvi wa Soko Kuu la Samaki Feri jijini Dar es Salaam, Akhmed Mbarouk, alibainisha kuwa mlipuko mmoja unatosha kuua viumbe hai vyote vilivyoko umbali wa mita za mraba 20. Alisema mlipuko huo unatosha kuua samaki wapatao 400 kwa wakati mmoja.

Alisema soko hilo lina wavuvi 3,000 waliosajiliwa na kwamba kwa mwaka 2018/19, kulikuwa na kesi 14 za wavuvi waliokamatwa kutokana na kujihusisha na uvuvi haramu wa kutumia mabomu.

Mbarouk pia alibainisha kuwa mwaka 2017, walikamata kilo 700 za samaki waliokuwa wamevuliwa kwa mabomu wakitokea Mafia na Pemba.

Alisema mamlaka ya soko hilo hufanya ukaguzi wa mizigo ya samaki wanaoingizwa sokoni kabla ya kuwafikia wanunuzi, akibainisha kuwa samaki wanaoongoza kwa kuvuliwa kwa kutumia mabomu ni jodari, vibua na changu.

Mbarouk alisema katika kumpima samaki, wanamwangalia magamba yake na wanatambua kama samaki huyo amevuliwa kwa njia isiyo halali ikiwa magamba yake yatakuwa na rangi ya kijani au kahawia.

"Pia, tunamwangalia umbo lake, matamvua na sehemu ya kutolea haja, samaki aliyevuliwa kwa mabomu anakuwa anatoa ute mweusi na hata ukimshika mkia, anakuwa anatingishika.

"Tukishampima na kuona dalili hizo, tunawakamata samaki na waliohusika kumvua pia tunawakamata na kuwapeleka polisi. Kabla ya kuwafikisha polisi, tunachukua maelezo yao na kujaza kwenye fomu maalum kwa ajili ya kutaifisha mali," Mbarouk alisema.

Alisema mamlaka ya soko hilo pia huwataka wahusika kujaza fomu za kutenda kosa, ushahidi na ya kuharibu mzigo uliokamatwa.

Mbarouk alisema kuwa katika soko hilo kuna jokofu maalum kwa ajili ya kuhifadhi vidhibiti (samaki) waliowakamatwa wakati kesi ikiendelea mahakamani.

"Tumekuwa tukiwapatia elimu wavuvi kuachana na uvuvi wa kutumia mabomu, hakuna mvuvi anayepewa leseni bila ya kupewa elimu hii muhimu," alisema.

Ofisa Mfawidhi wa Kanda ya Bahari ya Hindi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, West Mbembati, alisema uvuvi wa kutumia mabomu ni haramu na umekatazwa kisheria kwa mujibu wa Shera ya Uvuvi ya Mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009.

Alisema unaweza kumgundua samaki aliyevuliwa kwa kupigwa bomu kwa kumkagua kwa nje na ndani. Alisema kwa mwonekano wa nje, samaki huyo huwa amelegea tofauti na samaki aliyevuliwa kwa njia halali.

"Ukimshika anakuwa amelegea kwa sababu uti wake wa mgongo na mifupa inakuwa haiko imara, imevunjwavunjwa na bomu, tofauti na samaki aliyevuliwa kwa njia salama. Matamvua yake yanakuwa yamejaa damu ambazo zinakuwa zinachuruzika.

"Pia, samaki huyo ukimbonyeza, eneo lililobonyezwa halirudi juu haraka. Hata macho yake yanakuwa yamevilia damu, sehemu ya haja inakuwa iko wazi kwa sababu mishipa iko wazi kwa maana hiyo choo chake kinatoka chenyewe.

"Njia nyingine ya kubaini samaki amevuliwa kwa bomu ni kuangalia kwenye mfuko wake wa hewa unaomwezesha kuzama na kuibuka juu, unakuwa umepasuka, na ndiyo sababu samaki huyo akishapigwa bomu anakuwa anaelea juu ya maji na kushindwa kuzama.

"Samaki huyo ukimpasua, utumbo wake unakuwa umebondeka bondeka mithili ya uji au kuharibika vibaya, nyama zake zinakuwa haziko katika mpangilio mzuri.

"Samaki aliyevuliwa kwa kupigwa na bomu ni rahisi kuharibika haraka hata akiwekwa kwenye friji, lakini ukimla muda mfupi baada ya kuvuliwa, huwezi kugundua tofauti lakini akikaa muda mrefu hupoteza ladha," Mbembati alisema.

Mbembati alisema wavuvi wanaoendesha uvuvi huo wa kutumia mabomu, huufanya nyakati za usiku na wengi wao huwa wanatumwa na matajiri wakubwa.

SARATANI

Nipashe ilizungumza na Ofisa Habari Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Silvester Omary, ambaye alisema huwa wanapima chakula kilichoshasababisha madhara kwa jamii, lakini bado hawajapata kesi ya samaki waliovuliwa kwa kutumia mabomu.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Idara ya Kinga wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Crispin Kahesa, aliliambia gazeti hili kuwa samaki waliovuliwa kwa kutumia mabomu wanasababisha saratani kwa mlaji.

"Tutambue kwamba saratani inatokea pale kunapokuwa na uzalishaji au ukuaji usio wa kawaida wa chembe hai zilizoko kwenye mwili wa kiumbe hai, hali hiyo, hutokea pindi mfumo wa mwili unaoratibu uzalishaji na ukuaji wa hizi chembe hai unapokuwa umeathirika," alisema.

Dk. Kahesa ambaye pia ni Daktari Bingwa wa Kinga na Magonjwa ya Saratani, alisema vitu vinavyosababisha kuathiri mfumo wa mwili na kuchochea saratani viko kwenye makundi mbalimbali yakiwamo ya kibaiolojia.

"Visababisho vingine vya kansa ni wadudu na virusi kama vile HPV, HHV8, bakteria mfano helico bacter pyelori, wadudu mfano wanaosababisha kichocho.

"Visababisho vingine ni kemikali zinazotokana na takasumu za viwanda, mashambani mfano mbolea za chumvichumvi, dawa za kuua wadudu na magugu endapo mtu akitumia chakula chenye mabaki ya dawa hizo, mabomu ya mlipuko kama vile mabomu ya nyuklia na baadhi ya sumu zinazopatikana kwenye tumbaku na vyakula (aflatoxin).

"Vingine ni vya kifizikia mfano miale yenye nguvu kali inayozalishwa na jua na mabomu. Pia kuna mfumo wa maisha usio sahihi wa mwanadamu, matumizi ya pombe, unene kupita kiasi na matumizi makubwa ya vyakula vilivyosindikwa.

"Tutambue kwamba kuna saratani zaidi ya 200 ambazo zinatokea sehemu mbalimbali za mwili wa mwanadamu na kutokea kwa saratani kunategemea sababu nyingi ukiwamo umri wa mtu, kiwango cha visababisho, muda aliotumia hivyo visababisho.

"Sasa, ukiangalia mabomu ya mlipuko yanayotumika kuvua samaki, utagundua dhahiri yametengenezwa kwa kemikali mbalimbali ambazo zimehusishwa na saratani (Organic Amines, Hydrocarbons na Inorganic Chemicals).

"Pia, kunaweza kuwa na madhara ya kifizikia kutokana na mionzi inayoweza kuzalishwa na mabomu haya. Kwa hiyo, tutambue ya kwamba binadamu anaweza kupata madhara kwa kunywa maji au kula chakula kilichokuwa na vimelea vya kemikali zilizoko kwenye mabomu hayo."

Dk. Kahesa alibainisha kuwa miaka ya nyuma, zaidi ya asilimia 67 ya saratani zilikuwa za kibaiolojia (virusi na bacteria), lakini sasa kuna kasi ya ongezeko la saratani zinazotokana na mfumo wa maisha na uchafuzi wa mazingira kunakochochewa na ongezeko la uzalishaji wa takasumu.

Alibainisha kuwa kwa sasa kuna ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani za matiti, tezi dume, mapafu, ngozi, njia za hewa, saratani za damu na njia ya chakula.

ATHARI KWA MAZINGIRA

Ofisa Mazingira Mkuu wa Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Rose Mtui, aliiambia Nipashe kuwa uvuvi wa kutumia mabomu una athari kubwa kwa mazingira.

Alisema uvuvi wa aina hiyo husababisha kuharibika kwa matumbawe ambayo ni uoto wa asili unapatikana chini ya maji.

"Matumbawe ni kama msitu chini ya bahari ambao unanyonya hewa ukaa, matumbawe huwa yanasaidia katika mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa mfano, Tsunami inapotokea, matumbawe yanasaidia kupunguza kasi mawimbi ya bahari yasilete athari nchi kavu.

"Pili, bomu huharibu sehemu za mazalia ya samaki, samaki hutaga mayai sehemu tulivu ama kwenye mapango. Sasa, ukipiga bomu, linaua mayai na samaki wote wakubwa kwa wadogo, linaharibu kila kitu kilichoko ndani ya maji," Mtui alisema.

Ofisa huyo wa NEMC pia alisema uvuvi wa kutumia mabomu unaposhamiri, husababisha samaki kukimbia eneo hilo na kwenda sehemu nyingine, hivyo kusababisha uhaba wa samaki.

KUKATWA MIKONO, MIGUU

Augustine Lukuwi, mvuvi katika Bahari ya Hindi, alisema alianza kujishughulisha na kazi hiyo mwaka 1982 na hakukuwa na uvuvi wa kutumia mabomu.

"Miaka ya 1990 na 2000 ulianza kushamiri, lengo kubwa ni mvuvi kupata samaki wengi kwa haraka. Wavuvi wengi wanakatika mikono na miguu wakiwa katika uvuvi huo.

"Na wakishapata hayo majanga, huwa hawasemi ukweli kwamba waliandaa bomu kwa ajili ya kuua samaki, wanasingizia wameng'atwa na papa au samaki wakubwa," Lukuwi alisema.

Alibainisha kuwa bomu la kuulia samaki linakuwa na mchanganyiko wa mbolea ya chumvichumvi, V6 Water Explosive Gel, mafuta ya taa, utambi na detonator.

"Sasa, hivyo vitu vikiwa pamoja, huo utambi unawashwa na kibiriti na unapeleka moto kwenye detonator, unalipua hiyo V6 ambayo inakuwa imefungwa pamoja na mbolea ya chumvichumvi, ule mlipuko sasa ndiyo unapeleka athari kwa samaki," Lukuwi alisema.

Waembwa Mtoka, mvuvi na mmiliki wa vyombo vya uvuvi katika Bahari ya Hindi, aliiambia Nipashe kuwa uvuvi wa kutumia mabomu bado ni changamoto kubwa nchini licha ya hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali kuudhibiti.

"Huu uvuvi unatia umaskini kwa sababu unamaliza samaki kwa ajili ya miaka ijayo, maana bomu linaua mazalia, samaki wadogo wanakufa, uvuvi huu unapaswa kupigwa vita sana kwa faida ya sasa na ya baadaye. Serikali ya awamu ya tano imejitahidi kudhibiti lakini bado kuna wavuvi wachache wanaendelea na aina hiyo ya uvuvi," alisema.

Salmin Omary, muuza samaki eneo la Kimara Stop Over jijini Dar es Salaam, alisema hana elimu yoyote ya kumbaini samaki aliyevuliwa kwa mabomu.

Alisema huamka alfajiri kwenda Soko Kuu la Samaki Feri kununua samaki kwa wavuvi na kurudi nao dukani kwa ajili ya mauzo.

INAENDELEA UK 26

HABARI KITAIFA

# Makonda aona fursa za walimu, biashara SADC

Na Mary Geofrey

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewataka walimu wa lugha ya Kiswahili kuchangamkia fursa ya kwenda kufundisha mataifa mbalimbali duniani na mkoa wake umejipanga kuwasaidia kuifikia fursa hiyo.

Makonda (pichani) aliyasema jana jijini Dar es Salaam, ikiwa ni siku mbili baada ya Kiswahili kutangazwa kuwa lugha rasmi ya nne ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Awali jumuiya hiyo ilikuwa inatumia lugha tatu za Kiingereza, Kifaransa na Kireno katika shughuli zake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu mkutano wa SADC uliomalizika Jumapili jijini, Makonda alimpongeza Rais John Magufuli kwa kukabidhiwa Uenyekiti wa jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja.



Alisema mkoa utashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kuwasaidia walimu waliokosa nafasi za kazi walioko katika jiji hilo kuifikia fursa hiyo muhimu.

"Tutachangamkia hii fursa ya kuhakikisha walimu waliopo kwenye mkoa huu, ambao hawajapata kazi, kwa kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje lakini pia walimu ambao watataka kuanzia mkoani, wanaweza kuanzia kwa Ofisa Elimu Mkoa ili kuchangamkia fursa hii muhimu," Makonda alisema.

Kiongozi huyo wa mkoa pia aliwataka wafanyabiashara kuchangamkia fursa mbalimbali zitakazotokana na uongozi wa Rais Magufuli kipindi chote cha mwaka mmoja kwa kuwa viongozi wa mataifa mbalimbali watakuwa wanakuja nchini.

Alisema ni muhimu wafanyabiashara wa mkoa huo kujipanga kutumia fursa hiyo muhimu kwa ajili ya kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Makonda pia alisema mkoa umepanga kuwa na kampeni endelevu ya kufanya usafi wakati wote katika jiji hilo badala ya kusubiri wakati wa mikutano ya kimataifa.

# Biteko awacharukia wachimbaji wadogo kuendekeza migogoro

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amewacharukia wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wa eneo la Ikungi mkoani Mara baada ya kubaini kuwa ndio chanzo cha mgogoro kati yao na kampunio ya PolyGold Limited.

Biteko alitoa onyo kwa wachimbaji hao kuacha ujanja ujanja wakati akizungumza na pande zinazohusika na mgogoro huo katika kikao kilichofanyika ofisini kwake Mtumba, jijini hapa.

Aliwataka wachimbaji hao kuacha kusikiliza maneno ya watu walio nje ya makubaliano na mshirika wao na kusema waache tamaa badala yake waheshimu maafikiano waliyofikia kwa hiari bila uwapo wa wizara.

Aliongeza kuwa hata kama wawekezaji ni kutoka nje, wanayo haki ya msingi pale inapoonekana kukiukwa au kuonewa kwa kuwa shughuli zao ni halali na wanafuata sheria.

"Ndugu zangu niwaambie ukweli, huyu mmoja mnayemwona (mwekezaji) ana haki kama ninyi. Akionewa huyo mjue ana watu nyuma yake, ana ubalozi hapa kwa hiyo siko tayari kuchafua jina la serikali na wizara ninayoiongoza kwa kukiuka haki ya upande fulani. Uwe mzawa uwe mwekezaji wa nje, kwangu haki yako utaipata. Kwa hiyo kaeni na mkubaliane na mwekezaji wenu, mimi na wezangu tunatoka tunawaacha nikirudi tupate majibu msimamo wangu nimewapa," alisema Biteko huku akiwa amekasirika.

Kabla ya kuwaonya wachimbaji hao wadogo, Biteko alikutana na pande husika na kusikiliza madai ya kila upande na baada ya kuona wachimbaji wadogo wana makosa, aliwatoa upande wa Polygold na kubaki nao.

Baada ya maelekezo hayo, wachimbaji wadogo wakiongozwa na Edwin Mchihiyo na Sosy Mgonya ambaye leseni yake imenusurika kufutwa na waziri, walikaa pamoja na mwekezaji PolyGold (T) Ltd chini ya uwakilishi wa Sergey Sagsyan na Benny Haule na kuzungumza kuhusu mvutano juu ya mgogoro wao na kufikia muafaka uliosababisha kumaliza mgogoro wao.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mchihiyo alimshukuru waziri kwa kusimamia na kutatua mgogoro wao ambao umefikia tamati na kuahidi wanakwenda kutekeleza makubaliano yaliyokuwa yanaleta msigano baina yao.




SALAMU ZA PONGEZI

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano inatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya maendeleo Kusini mwa Africa ( SADC).

Wizara inaungana na Watanzania wote kukutakia afya njema na maisha marefu wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yako.

Tovuti : www.mwtc.go.tz

Twitter: @WizaraUUM

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Halmashauri Moshi kulinda watoto

**HALMASHAURI** ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro wiki hii imeeleza nia yake kuwa haitakuwa tayari kuona watoto wadogo wakishinda pamoja na wazazi au walezi wao wanaofanya biashara katika soko la mitumba la Memorial lililoko mjini hapo.

Ni hatua nzuri iliyotangazwa hivi karibuni ikilenga kumlinda na kumtunza mtoto dhidi ya mambo hatarishi na sisi tungependa kuipongeza.

Hata hivyo tunaona kuwa ni jambo lililochelewa, ilitakiwa hatua hizo zichukuliwe mapema zaidi kwa kuwa watoto wengi wameumia na kunyanyasika katika mazingira hayo.

Kwa ujumla watoto wanaonekana wakishinda sokoni kuwe ni kwenye maeneo ya kuuza bidhaa za vyakula, mitumba na hata wanyama bila kujali kuwa wanaumia kiafya.

Watoto wadogo wenye umri wa chini ya miaka 18 wanapochwa kukaa kinyemela kwenye maeneo hayo kuna athari nyingi za kiafya na kisaikolojia.

Athari za kiafya ni kama kuvuta hewa yenye vumbi na taka za sumu zinazotoka kwenye injini za magari, bodaboda, viwanda vilivyojirani na majiko ya kuni na mkaa yanayotumiwa kwenye masoko kupika vyakula vya wafanyabiashara.

Lakini, watoto hao wanaweza kukaa katika mazingira machafu yenye harufu mbaya zinazotoka vyooni au mifereji ya maji machafu inayowazunguka pamoja na masoko.

Aidha, uvutaji wa vumbi na hata moshi wa sigara sokoni ni jambo la kawaida na yote hayo yanaathiri mapafu ya watoto ambao ni wadogo na kuwasababishia kupata magonjwa ikiwamo kifua kikuu na mzio (aleji).

Lakini, si hivyo tu watoto hao wanaishi kwenye mazingira yenye kelele, vurumai na fujo zinazotokana na shughuli mbalimbali za uzalishaji zinazozunguka masoko.

Kelele zinaweza kuwa ni honi za magari, pikipiki na kelele za viwandani hasa mitambo na mashine. Maisha ndani ya masoko ni ya vurumai iwe wakati wa mvua au jua. Watoto hao huumizwa na hali ya hewa hasa wakati wa kipupwe na baridi kali hasa mkoani Kilimanjaro.

Kwa ujumla tunaungana na Halmashauri ya Moshi kuwa sokoni si makazi salama na malezi bora ya watoto, hii huhusisha kukosekana huduma za vyoo, chakula safi na salama kinachoandaliwa na mzazi na hata maji ya kunywa.

Ikumbukwe wateja hujisaidia kwenye choo cha kulipia ambacho si salama kwa watoto. Lakini wengine nao wanazungumza maneno makali na matusi ambayo huwakwaza watoto.

Aidha, uhusiano baina ya watu wanaofanya biashara wakati mwingine unaonyesha matendo yanayopotosha watoto wadogo kimalezi. Yote haya ni mambo ambayo yanasababisha Halmashauri ya Moshi kuwaondoa watoto wote kwenye maeneo hayo ya biashara.

Hatua iliyotangazwa na Manispaa ya Moshi ni ya kuigwa na maeneo mengine ya masoko na hata yale yanayofanya biashara pembeni ya barabara.

Huenda umma haujajua kuwa si haki kuwaacha watoto kushinda pembeni ya barabara kuanzia alfajiri hadi usiku.


Tunaipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Moshi na kuwashauri wadau ikiwamo serikali na wengine wanaotetea haki za watoto kuanzisha kampeni ya kutokomeza kwa kuwaondoa watoto masokoni na kwenye maeneo ya biashara ili kulinda afya zao.

Pamoja na hatua hiyo tunaomba serikali ifanya utafiti ili kujua na kuzitangaza athari za kuwaacha watoto kwenye maeneo hayo ili wazazi na walezi waufahamu ukweli.

Kadhalika tunawaomba wafanyabiashara hao wa soko la mitumba Moshi kuukubali ushauri kwa kuwa yote hayo yanalenga kumsaidia mtoto wa Tanzania asiangamie.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Taifa litastawi tukiimarisha zaidi ulinzi kwa watoto wetu

Na Elizabeth Zaya

**SERIKALI** ya Tanzania imeweka sheria, taratibu na miongozo ambayo inashirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali kuhakikisha usalama na ustawi wa watoto nchini.

Lengo la kuweka misingi hiyo ni kuhakikisha mtoto analindwa dhidi ya maovu yote ikiwamo ukatili wa aina zote lakini na kupata haki zake zote.

Hata hivyo, pamoja na kazi kubwa inayofanywa, bado ukatili dhidi ya watoto unaendelea kushamiri na kutupa picha kwamba hitaji la mkakati madhubuti wa kuhakikisha sheria zinazowekwa zinasaidia kupunguza masuala ya ukatili dhidi ya watoto hao kama sio kumaliza kabisa ni la lazima.

Yapo matukio mengi ambayo yamekuwa yakiwakumba watoto wengi yakiwamo ya kubakwa, kulawitiwa na kupigwa.

Na ripoti mbalimbali zinaonyesha kwamba watoto wengi wamekuwa wakifanyiwa vitendo hivyo na watu wanaowazunguka.

Wamekuwa wakifanyiwa vitendo hivyo katika maeneo tofauti ikiwa ni pamoja na majumbani, wawapo njiani kuelekea shuleni, wanapocheza na wenzao au wanapotembea.

Aidha, kutokana na jamii kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu sheria na taratibu za kufuata mara baada ya mtoto kufanyiwa ukatili wa aina yoyote ile, ndiyo sababu mojawapo ambayo inatajwa ya kuviendeleza vitendo hivi vya kuwatesa watoto na kuchangia kuendelea kufanyika.

Suala la utamaduni au desturi na mila ya kuamua kumaliza kimyakimya masuala hayo ya ukatili kwa kisingizio cha kulinda heshima ya mkosaji na hadhi yake katika jamii ni miongoni mwa vyanzo vinavyochangia ongezeko la vitendo hivyo.

Na mbaya zaidi kesi zikipelekwa kwenye mamlaka husika, wenye ushahidi hawafiki mahakamani au mara nyingine mhusika anatoroka na baadaye kesi hufutwa bila kujua hatima ya mtoto aliyepata madhara.

Mpaka sasa kuna idadi kubwa ya watoto waliobakwa na kulawitiwa ambapo takwimu zinaonyesha kwamba mwaka 2015/2016 watoto waliobakwa na kulawitiwa walikuwa 394.

Aidha, mwaka 2016/2017 zilifikia 2,984 huku tafiti zikionyesha kuwa idadi ya watoto waliobakwa itazidi kuongezeka kwa mwaka 2018/2019 na kuwa kubwa zaidi.

Suala hili si la serikali peke yake, ushirikiano unahitajika kutoka kwa jamii yote kwa ujumla ili kushiriki kuutokomeza uhalifu huu ambao unasababisha kuwa na taifa lisilofaa baadaye.

Pia, nguvu za ziada zinahitajika kuhakikisha watoto wanaokumbwa na majanga haya yanasaidiwa kisaikolojia ili kurudi katika hali yao ya kawaida itakayowafanya kuwa viongozi wema na wazazi bora baadaye.

Jamii kwa ujumla inatakiwa iwe macho kupinga vikali ukatili huu unaowakumba watoto wadogo kwa sababu wao ndio taifa la kesho na ndio tegemeo kubwa la taifa katika siku za usoni.

Hivyo hatupaswi kufumbia macho matukio kama haya na kukaa kimya pale tunapogundua mtoto amefanyiwa ukatili, tuchukue hatua ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa katika mamlaka zinazohusika.

Tunatakiwa tufungue macho juu ya haya matukio yanayowakuta watoto wetu na pia tuwe makini na jamii inayotuzunguka kwa ujumla, kwani wengi wao ndio wanaohusika kwa namna moja ama nyingine katika kutekeleza vitendo hivi kwa watoto.

Wazazi kwa sababu ndiyo watu wa kwanza katika maisha ya watoto, wahakikishe wanakuwa karibu na watoto kwa kufuatilia nyendo zao na kuwachunguza.

Walimu na viongozi mbalimbali wa dini wanajitahidi kupiga vita dhidi ya ukatili wa namna hii kwa jamii lakini hali bado ni tete.

Hata hivyo, hawapaswi kukata tamaa, ila kuongeza mwendo na jitihada za kuendeleza vita hivi.

Mamlaka zinazohusika na hatua za kisheria nazo ziendelee kutoa kipaumbele kwa matukio kama haya ili kurahisisha kazi ya kupambana na vita hii na kuokoa viongozi hawa wa siku za usoni.

Jamii ikiwa macho dhidi ya matukio haya na kila mtu akawajibika katika nafasi yake kupambana na vita hii, basi watoto watakuwa salama.

# Uhalifu mkubwa wapungua kwa 2%

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema katika kipindi cha miezi sita kuanzia Januari, wamefanikiwa kupunguza makosa makubwa ya uhalifu kwa asilimia 2.2.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alisema jana kuwa, jumla ya makosa makubwa ya jinai yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi kwa mwaka huu kuanzia Januari hadi Juni yalikuwa 28,252.

Alisema ikilinganishwa na mwaka jana katika kipindi kama hicho, matukio yaliyoripotiwa yalikuwa 28,889.

Akisoma taarifa ya serikali kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, iliyohusu hali ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao kwa kipindi hicho, Masauni alisema kwa sasa matukio ya uhalifu yamepungua.

"Kwa ujumla tumefanikiwa kupunguza makosa 637 kwa mwaka huu. Hii inatokana na juhudi za askari wetu na utekelezaji wa dhana ya ulinzi shirikishi inayotekelezwa," Masauni alisema.

Alitaja makosa hayo makubwa ambayo wameyapunguza ni dhidi ya binadamu, maadili ya jamii, kuwania mali na ya uhalifu wa kifedha. Kuhusu makosa yatokanayo na usalama barabarani, Masauni alisema yamepungua kwa sababu kuna usimamizi wa sheria na kutoa elimu ya usalama barabarani kwa watumiaji wa vyombo vya moto na watembea kwa miguu.

"Takwimu za makosa ya ajali za barabarani katika kipindi cha Januari hadi Juni mwaka huu zinaonyesha kupo kwa jumla ya makosa 1,610 yaliyoripotiwa ikilinganishwa na makosa 2,200 mwaka 2018. Kwa hiyo tumepunguza makosa 590," alisema.

Alisema idadi ya vifo vimepungua kutoka watu 1,051 waliofariki mwaka jana katika ajali za barabarani hadi kufikia 781 walipoteza maisha mwaka huu kuanzia Januari hadi Juni.

### IGP SIRRO ANENA

Naye Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, alisema mafanikio hayo yamechangiwa na matumizi ya teknolojia katika kupambana na uhalifu na amewaonya wahalifu kutafuta shughuli nyingine ya kufanya.

"Tunatumia vifaa maalumu ikiwamo drones (ndege zisizo na rubani) katika kudhibiti uhalifu japo kwa sababu za kiintelijensia hatuwezi kusema ziko ngapi na maeneo gani muhimu tunawaasa wahalifu kuacha mipango yao ya kuvuruga amani ya nchi hii kwa sababu hawatabaki salama," alisema Sirro.



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe na viongozi wengine wa chama hicho wakiwa kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, wakisubiri kusikilizwa kwa kesi inayowakabili. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yaomba wadau kuwa na subira uchaguzi serikali za mitaa

**Na Enock Charles**

SERIKALI imewataka wadau wa uchaguzi kuwa na subira wakati ikiwa katika maandalizi ya kuitangaza rasmi sheria itakayotumika katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwishoni mwa mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara.

Akizungumza na Nipashe alipoulizwa kuhusu maandalizi ya uchaguzi huo ikiwamo kuitangaza sheria itakayotumika katika uchaguzi huo, Waitara alisema maandalizi yatakapokamilika sheria hiyo itatangazwa na serikali, na kuwataka wadau wa uchaguzi kuvuta subira.

"Sheria itatangazwa tu muda utakapowadia, wadau wawe na subira, maandalizi yatakapokamilika itatangazwa, na mwenye mamlaka ambaye ni Rais," Waitara alisema.

Wadau wa uchaguzi vikiwamo vyama vya siasa wametoa malalamiko wakidai kuchelewa kutangazwa kwa sheria hiyo kunaweza kuathiri maandalizi yao kuelekea kwenye uchaguzi huo kwa kuwa kuifahamu sheria hiyo ni moja ya maandalizi muhimu katika uchaguzi huo.

Akizungumza na gazeti hili Katibu Mwenezi wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alidai kuwa kuchelewa kutangazwa kwa sheria hizo kunaathiri mchakato wa vyama maandalizi ya mafunzo kwa mawakala na wagombea wao katika uchaguzi huo.

"Kuchelewa kutangazwa kwa sheria itakayotumika katika uchaguzi wa serikali za mitaa kunaathiri maandalizi yetu kwa sababu huwezi kuandaa wagombea kwa mfano bila kujua kanuni zinasemaje kuhusu sifa za wagombea wanaotakiwa, maana kubadilika kwa kanuni kunaweza kupelekea kubadilika kwa aina ya mgombea," alisema Shaibu.

Uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba, na serikali imeshasema kuwa kiasi cha Sh. bilioni 82 zitatumika.

# Jaji Kiongozi afunguka kuchelewa kwa mashauri

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, amewataka wananchi na wadau wa Mahakama mkoani Kigoma kutoa ushirikiano wa kutosha kwa watumishi wa mahakama.

Jaji Feleshi akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye jengo jipya la Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma iliyopo maeneo ya Kata ya Bangwe Manispaa ya Kigoma/Ujiji, alisema hawacheleweshi mashauri bali wanaochangia kuyachelewesha ni wadau wao wanaowajibika kupeleka mashauri mahakamani, kuchelewa kuja kutoa ushahidi na kuchelewa kupeleka mashahidi.

"Nawaasa wanaKigoma na wadau wa mahakama kujiandaa sasa kutupatia ushirikiano wa kutosha kwa maana sisi kama mahakama hatukuja kwa kubahatisha kuanzisha masijala hii...ndiyo maana nimesema tumekuwa na taratibu na haikuwapo masijala baada ya kuwa kila kitu kimekamilika ikaanzishwa kisheria baadaye wakateuliwa majaji akapatikana msajili na akapatikana mtendaji na watumishi.

"Kwa hiyo kwa watumishi wa mahakama tayari mahakama ipo kwenye maboresho yanayoendelea, na naamini wanaelewa misingi tunayosimamia na viwango vyetu vya kisasa."

PASS
PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT

**Call for proposals: Green Growth Consultant**

**The Private Agricultural Sector Support (PASS) Trust** was established in the year 2000 under the agricultural Sector Program Support.

PASS currently operates as an independent organization, operating as a service provider linking the agricultural and financial sectors. Our main objective is to facilitate access to financial and agribusiness development services for agribusiness entrepreneurs covering the entire agribusiness value chain.

**Our clients** comprise of individual agribusiness entrepreneurs, associations/ groups of smallholder farmers and companies engaged in the agricultural sector. We among other things, assist our clients in developing solid and bankable investment project write ups, and facilitate access to finance through credit guarantee schemes that we operate with commercial banks.

In order to achieve long-term and inclusive growth in agriculture, PASS is aware that attention is needed to ensure responsible development of the sector. One key area of focus is sustainable management of natural resources and minimizing damage to the environment and people in supported projects.

To this end, PASS has incorporated in its 5-year strategy to build a strong green profile and has developed various guidelines and policies to contribute to inclusive and green growth in agriculture, including a policy on Environmental and Social Sustainability.

**Assignment**
PASS is now seeking the services of a technical consultant to work under a short-term assignment for purposes of developing a Strategy for Green Growth as well as a plan for implementation of the commitments made. The strategy is expected to provide directions to how PASS can incorporate the concept of Green Growth in our operations bringing together existing policies, guidelines and collaborations.

**For more information on this assignment, visit www.pass.or.tz**

# Makonda akomalia

INATOKA UK.2

“Wapo wengine wanaingia kwenye makubaliano tuzae kabisa, lakini mwisho wa siku ana muacha na mtoto wake na ikitokea baba amekufa aruhusiwi kabisa hata kuaga kwa sababu hatambuliki kwenye ile familia nyingine,” alifafanua zaidi Makonda.

Agosti 12, mwaka huu, Makonda alisema ana mpango wa kuanzisha kanzi data ya ndoa zote zilizopo katika Mkoa wa Dar es Salaam ili kupunguza utapeli wanaofanyiwa wanawake kwa kudanganywa kuolewa.

“Hii ‘data base’(kanzi data) itasaidia mwanamke akiambiwa kuwa anaolewa ataingia katika mtandao na kuangalia jina la mwanaume huyo kama ameoa au la na hata itawasaidia wanawake ambao wameolewa ili kuzuia waume zao wasioe kwa siri. Wanawake mkishaolewa washawishini wanaume waje kusajili vyeti vya ndoa,” alisema.

# Jafo ataka watumishi afya

INATOKA UK.3

Alibainisha kuwa lengo ni kusogeza huduma za afya kwa wananchi na kwamba vituo 119 vimekwishakamilika na kati ya hivyo, 58 vimeanza kutoa huduma za upasuaji. Pia alisema hospitali za wilaya 67 ziko katika hatua ya mwisho ya ujenzi na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, mwaka huu.

“Kabla ya kuanza ukarabati au ujenzi mwaka 2017, kulikuwa na zahanati 6,640 (asilimia 53) kati ya hizo za serikali ni 4,554 (asilimia 36) katika vijiji 12,545, vituo vya afya ni 701 (asilimia 16) kati ya vituo vya afya 518 vilivyokuwapo ni 115 (asilimia 22.4) tu ndio vilikuwa vinatoa huduma za dharura na upasuaji pindi zinapohitajika,” alisema.

Katika mwaka wa fedha wa 2019/20, alisema serikali imetenga Sh. bilioni 10.4 kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya 52 na Sh. bilioni 33.5 kwa ajili ya hospitali 67 za wilaya.

Naye Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema kabla ya kuboresha huduma za afya nchini, serikali ilikuwa inatumia Sh. milioni 100 kwa mgonjwa mmoja wa kupandikizwa figo nje ya nchi.

“Hivi sasa mgonjwa kupandikizaji figo ndani ya nchi anatumia Sh. milioni 20. Tumeokoa kiasi kikubwa cha fedha, lakini bado tunatumia gharama kubwa kwa kuwatibu wagonjwa wa kisukari, presha na magonjwa yasiyoambukiza,” alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Waganga Wakuu wa Mikoa, Dk. Paul Chawote, aliomba serikali kuhimiza suala la bima ya afya kwa kuwa asilimia 49 ya watu wanaofika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ni wagonjwa wa msamaha, jambo ambalo ni mzigo kwenye vituo hivyo.

# Mume ashikiliwa kwa tuhuma za mauaji

INATOKA UK. 2

majira ya saa 4 usiku chumbani kwake akiwa amefariki.

Kwa mujibu wa kamanda Shana katika chumba hicho walikuta mtandio uliokuwa umetundikwa juu ya paa la chumba hicho, huku mwili huo ukiwa na jeraha mdomoni.

Alisema taarifa za kifo cha marehemu zilitolewa polisi na mume huyo wanayeishi nyumba moja na marehemu, lakini kila mtu analala chumba chake na kwamba baada ya kufika nyumbani hapo majira ya saa 4:00 usiku alichungulia ndani ya chumba cha mkewe na kumkuta akiwa amelala chini na baada ya kumwangalia alibaini kwamba amefariki.

“Tunamshikilia mume wa marehmu kwa ajili ya mahojiano zaidi wakati uchunguzi wa kina ukiendelea ili tuweze kubaini kama kweli marehemu amejiua au ameuawa kwa sababu katika nyumba hiyo alikuwa anaishi na mume wake na hawaishi na mtu mwingine,” alisema.

Kamanda Shana aliwakaribisha wananchi wote wenye taarifa zinahusiana na kifo hicho ofisini ili kubaini ukweli wa tukio hilo na kwamba majina yao yatahifadhiwa.

“Ni mapema mno kueleza kilichosababisha chanzo cha kifo hiki, lakini makachero wetu wanaendelea na uchunguzi, milango ya ofisi yangu ipo wazi niwakaribishe wananchi wote wenye taarifa ya mauaji haya kuzileta kwangu,” alisisitiza.

Kwa mujibu wa majirani walioshuhudia mwili huo ukiwa sakafuni baada ya mume huyo kupiga kelele za kuomba msaada ambao hawakutaka majina yao yaandikwe gazetini, walidai walimkuta marehemu akiwa amelala chini huku pembeni yake kukiwa na Biblia, mtandio na simu yake ya kiganjani.






# Shahidi adai kortini

INATOKA UK.2

**Wakili:** Umeshawahi kumpima uzito Magufuli?

**Shahidi:** Si kazi yangu.

Kesi hiyo inaendelea kusikiliza ushahidi wa Jamhuri leo.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Dk. Zainabu Mango, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon na Wakili wa Serikali Jacqueline Nyantori.

Upande wa utetezi uliongozwa na Peter Kibatala, Jeremia Mtobesya, Hekima Mwasipu na Fredy Kiwelo.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda Mjini, Ester Bulaya; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, **Mwalimu;** Mbunge wa Kibamba, John Mnyika na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Awali Koplo Charles akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, shahidi alidai kuwa Februari 16, 2018 alipangiwa kazi kama mwandishi wa habari kuandika taarifa kwenye mkutano wa kufunga kampeni wa Chadema katika viwanja vya Buibui.

Alidai kuwa alijiandaa na vitendea kazi vyake ikiwamo kamera ya kupiga picha za video na ilipofika saa 10 alasiri, alifika katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuanza kazi.

Alisema alipofika watu walianza kukusanyika na mshereheshaji alitangaza kwamba viongozi wakuu wa chama wameshafika, baada ya muda wabunge na viongozi wakuu walipanda jukwaani alimsikia Mbowe akitoa kauli za kufanya hamasa ya kuichukia serikali.

“Wanachama walipata hamasa na mihemko iliyosababisha wapate jazba ya kuichukia serikali na vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi waliokuwa wamekaa walinyanyuka na kuhamasika, mimi na waandishi wenzangu tulitawanyika pale tuposimama karibu na jukwaa, nilikimbilia kwenye gari polisi kunusuru kamera,” alidai Koplo Charles.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka jana, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawakuwapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa siku ya tukio, Bulaya alishawishi wakazi wa eneo hilo kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Pia ilidaiwa kuwa siku hiyo, katika barabara ya Kawawa eneo la Mkwajuni, Kinondoni, kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya ofisa wa jeshi la polisi, Gerald Ngiichi, na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja vya Buibui, kwenye mkutano wa hadhara, Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki alitamka matamshi kwamba “Kesho patachimbika upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii...wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano... watu wanapotea, watu wanauawa, wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome.”

Maneno hayo yanadaiwa yalikuwa na mwelekeo wa kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania.

Washtakiwa wote walipFosomewa mashtaka yao kwa nyakati tofauti walikana.

HABARI KITAIFA

# Balozi Seif awafunda makatibu wa CCM

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Self Ali Iddi, amewaonya makatibu wa wilaya na mkoa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoonyesha upendeleo kwa mtu yeyote ambaye anataka kuwania uongozi kwani kazi yao ni kuangalia kama refa uwanjani.

Balozi Seif ambaye ni mlezi wa chama hicho mkoani Shinyanga, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara kwenye Kijiji cha Buganzo Kata ya Ntobo Halmashauri ya Msalala, ambapo alieleza kuwa wapo baadhi ya makatibu wamekuwa wakibeba wagombea wanaowataka wao.

Balozi Seif aliwaonya makatibu wa wilaya na mkoa wa CCM kutoonyesha upendeleo kwa mtu yeyote ambaye anataka kuwania uongozi, na kuwa kama wapo, waache mara moja.

Alisema lazima wapime kuona wana sifa ili kupata viongozi wazuri ndani ya chama, na kazi hiyo inafanywa na makatibu waliopewa dhamana, hivyo waache ushabiki kwa kuwa kwa kufanya hivyo, watakuwa wanatimiza wajibu wao.

"Kazi yetu ni kuwapima kama wana sifa zinazofaa, wengine wamekuwa wakijipenyeza kwenye chama na kuonekana kuwa sio mwenzetu," alisema na kuongeza:

"Kazi yenu makatibu ni kuwapima wale wote wanaotaka kuwania uongozi kwa ngazi yoyote."

Aidha, Balozi Seif alisema kilio cha Mbunge wa Msalala, Ezeckiel Maige cha kuhitaji barabara ya lami inayotoka Kahama kwenda Geita amekisikia na kuongeza kuwa imeshatengewe fedha.

Maige alisema barabara ya kutoka Manzese Kahama kwenda mkoani Geita ina urefu wa kilomita 147, na kuwa inahitaji zaidi ya Sh. bilioni moja kwa kipande chake chenye urefu wa kilomita 76 ili itekelezwe kwa kiwango cha lami.

# Waahidi kuwasaidia wanawake wenzao watakaogombea 2020

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANAWAKE wa Shehia ya Msuka Mashariki Wilaya ya Micheweni kisiwani Pemba, wamesema wako tayari kuwapa hamasa na kuwaunga mkono wanawake watakaojitolea kugombea nafasi za uongozi mwaka 2020 na kamwe hawatowabeza.

Walisema watakapowachagua wanaamini watasaidia kutatua matatizo yao yanayowakabili kwenye shehia yao, ikiwamo barabara na ukosefu wa walimu katika shule yao, ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa watoto kufeli katika masomo yao.

Walisema wameshachagua viongozi wanaume kwa miaka mingi sasa, ingawa wakishapata wanahama makazi yao na wanahamia nje ya kisiwa hicho, jambo ambalo linawauma sana, kwani uongozi hutokana na wao.

Wakizungumza katika mikutano ya kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi kisiwani Pemba, uliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) ofisi za Zanzibar, walisema watahakikisha ifikapo mwaka 2020 wanachagua viongozi wanawake, ili wawasaidie kutatua shida zao.

**Tutajipanga na kushirikiana ili mwaka 2020 tuwe na viongozi wanawake katika kada mbalimbali, maana kila mwaka tunachagua wanaume na wanahama.**

"Tutajipanga na kushirikiana ili mwaka 2020 tuwe na viongozi wanawake katika kada mbalimbali, maana kila mwaka tunachagua wanaume na wanahama," alisema Maulid Saleh Omar.

Naye mkazi wa eneo hilo, Maryam Seif Khelef, alisema ipo haja elimu kwa mtoto wa kike ipewe kipaumbele, ili wajengewe uwezo wa ukakamavu mapema, jambo ambalo litasaidia kujiamini kugombea hapo baadaye.

Katibu wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar kisiwani Pemba, Yussuf Abdalla Ramadhan, alisema mwanamke ana uwezo wa kupambana, hivyo ni muhimu kufuata masharti na maadili ya kiislamu.

"Mnayo haki ya kuwa viongozi, lakini msiende kinyume cha masharti na maadili, maadili yaheshimiwe na hapo ndipo mtafanikiwa," alisema shehe huyo.

Mwenyekiti wa timu ya wanaume ya mabadiliko, Suleiman Massoud Said, alisema wanawake wamebeba majukumu makubwa sana na wameachwa nyuma kwa baadhi ya mambo, ikiwamo ya uongozi, hivyo ni vyema kuwapunguzia majukumu hayo, ili wahamasike kuingia majimboni kugombea nafasi hizo.

Naye katibu wa timu hiyo, Mohamed Hassan Ali, aliwataka wanawake wenye nia kugombea nafasi za uongozi, wawe makini na wasikubali kutoa rushwa ya aina yoyote, kwani itamshusha thamani yake.

Ofisa uendeshaji kutoka Tamwa, Pemba, Asha Mussa Omar, alisema kuwa ushiriki wa wanawake katika masuala ya kisiasa upo ingawa ni mdogo, hivyo sauti yake ni ndogo katika kutetea haki zao na watoto.

"Mutakapoingia katika nafasi za uongozi mtaweza kutatua changamoto mbali mbali zinazowakabili, ambazo wanaume hawazitetei," alisema ofisa huyo.

Mkutano huo ni mwendelezo wa mikutano ya kuwahamasisha wanawake kuingia majimboni kuombea nafasi za uongozi ifikapo mwaka 2020 ambayo iliandaliwa na Tamwa chini ya ufadhili wa Umoja wa Mataifa Kitengo cha Wanawake.



Salma Ali Abeid mkazi wa shehia ya Msuka Mashariki, Wilaya ya Michewenu, akichangia jambo katika mkutano wa kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi uliofanyika shehiani hapo na kuandaliwa na Tamwa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara wakopeshwa mil. 600/- kutoka NMB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa mikopo yenye thamani zaidi ya Sh. bilioni 600 kwa wafanyabiashara wa kati na wadogo ambayo imewasaidia kuweza kuongeza mitaji yao na kujikwamua kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro, wakati wa mkutano wa klabu za wafanyabiashara wa mkoa wa Tanga waliopo waliokuwa na mikopo kwenye benki hiyo.

Meneja huyo alisema ili nchi iweze kukua, lazima kuwapo wafanyabiashara ambao wenyewe watachochea ukuaji wa uchumi na ndio maana benki hiyo wakaamua kuwekeza kwa kiasi kikubwa hicho na wanataka kukuza eneo hilo.

Alisema wafanyabiashara hao wadogo wakikua kesho na kesho kutwa ndio ambao watakuwa wateja wakubwa zaidi na uchumi wa nchi utaendelea kukua, kwa sababu kwenye kukopa na kukopeshana na kuwezesha ndio kunakofanya biashara zinaweza kukua kupata mafanikio.

"Kwa kiasi kikubwa mikopo hii imeweza kuwasaidia kwa asilimia kubwa wafanyabiashara kuendeleza biashara zao ambazo zimekuwa chachu ya wao kuweza kupata maendeleo, hivyo kujikuta wakipiga hatua kuwa za kiuchumi," alisema.

Aidha, alisema kwamba benki hiyo imekuwa ni mkombozi mkubwa kwa Watanzania kutokana na kujikita kuendeleza wafanyabiashara wadogo na wa kati, ambao wanaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa maendeleo.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, alisema benki hiyo inafanya kazi kubwa na nzuri hasa ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji kupitia mikopo mbalimbali na kuendelea kuibuliwa na kuibuni kila siku.

Alisema wameamua kwenda mbali zaidi ya hapa kwa kuanzisha mikutano itakayosaidia kuwafanya wafanyabiashara wajione kama sehemu ya familia.

Alisema kupitia mfumo huo walioubuni wa kuwakutanisha pamoja wateja wao angalau mara moja kwa mwaka wanafahamiana ikiwamo kupata fursa ya kupata ufahamu wa mambo waliyoratibu na watakayo yafanyia kazi.

Alisema benki hiyo ina mafanikio makubwa na inachangia sana katika mafanikio ya serikali, hivyo ina umuhimu wake wa kipekee kwenye kuchangia ukuaji wa uchumi.

# Serikali yaombwa fursa wenye watoto uzito pungufu

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

SERIKALI imeombwa kugharamia kambi za kinamama wanaobainika kuwa na watoto wenye uzito pungufu wanaokusanywa na kuwekwa kwenye kambi maalum kwa ajili ya kuwafundisha kupika chakula dawa, ikiwa ni jitihada mojawapo ya kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Wakizungumza wakati wa kupokea miradi iliyokuwa ikifadhiliwa na Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kagera kupitia mradi wa Ibwera DP, baadhi ya wananchi na wahudumu wa afya ngazi ya kijiji kutoka katika kata tatu za Ibwera, Nyakibimbili na Mikoni, walisema shirika hilo lilifadhili miradi mbalimbali ikiwamo ya lishe kwa watoto na sasa mradi umefikia kikomo, lakini bado tatizo la utapiamlo kwa watoto ni kubwa.

Sued Rashid, ni mhudumu wa afya ngazi ya jamii, alisema serikali iwe tayari kusaidia kulingana na itakavyoweza ili kuwawezesha wanaohusika na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu namna ya kuwahudumia watoto wenye utapiamlo, maana ili wafundishwe lazima wawekwe katika kambi kwa siku 12 na kuwa bila kuwezeshwa kambi hizo haziwezi kufanyika.

**Utasikia kuna hujuma mahala, hata sababu ya kufanya hivyo haipo, lazima kwa umoja wetu sisi watumishi wa umma, viongozi kwa maana ya madiwani na wenyeviti wa vitongoji na vijiji.**

Ester Ndibalema, alisema elimu juu ya utapiamlo ambao ndiyo chanzo kikuu cha watoto kudumaa inabidi iendelee kutolewa kwa wananchi, maana vyakula vyote muhimu vinavyoweza kuimarisha afya za watoto vinapatikana katika maeneo wanayoishi.

Savera Mutayabarwa, alisema vyakula kama viazi lishe vinapaswa kutiliwa mkazo ili vilimwe kwa wingi, kwa lengo la kuhakikisha afya za watoto zinakuwa salama.

"Tumeweza kuwafundisha watu kulima viazi lishe kwa ajili ya kupunguza tatizo la utapiamlo, lakini tumewafundisha namna ya kutunza mbegu ili watakapolima wasikose mbegu, lakini halijazingatiwa, baadhi yao wanakula hadi mbegu, na hii inatokana na baadhi kutozingatia wanayofundishwa," alisema.

Akizungumza wakati wa kupokea mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawilo, aliwataka viongozi wa ngazi za vijiji na kata kushirikiana na wananchi kutunza miradi hiyo na kuwa serikali haiko tayari kwenda kwenye miradi na kukuta imeharibiwa.

"Utasikia kuna hujuma mahala, hata sababu ya kufanya hivyo haipo, lazima kwa umoja wetu sisi watumishi wa umma, viongozi kwa maana ya madiwani na wenyeviti wa vitongoji na vijiji, na wananchi wote kwa ujumla, tuipokee miradi tunayofadhiliwa na tuisimamie na kuitunza, ili iwe endelevu," alisema Kinawilo.

Mkurugenzi wa miradi kutoka makao makuu ya Shirika la World Vision Tanzania, Dk. Yosh Kasilima, alisema katika mwaka huu wa fedha wanatekeleza miradi ya maendeleo katika mkoa wa Kagera ikiwamo ya elimu, afya, maji, kilimo, ufugaji na lishe kwa watoto, yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 8.3.

Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa yenye kiwango kikubwa cha watoto wenye udumavu ambao kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2018 na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Kituo cha Chakula na Lishe, asilimia 39 ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano mkoani humo wamedumaa.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akizungumza na waandishi wa habari jijini humo jana, wakati akimpongeza Rais John Magufuli kwa kupata nafasi ya kuwa mwenyekiti wa jumuiya ya nchi ya wanachama wa SADC.
**PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Wazazi Dar wapewa tano uchangiaji damu

**Na Enock Charles**

MPANGO wa Taifa wa Damu Salama (NBTS) Kanda ya Mashariki umewashukuru wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya jirani kwa namna walivyojitokeza kuchangiaji damu kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa wenye uhitaji ikiwamo majeruhi wa ajali ya moto iliyosababishwa na lori la mafuta lililopinduka na kulipuka eneo la Msamvu mkoani Morogoro.

Ajali hiyo ya Agosti 10, mwaka huu, ilisababisha vifo vya zaidi ya watu 90 na wengine kujeruhiwa.

Aidha, mpango huo umeendelea kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kuchangia damu, huku ukiwahimiza kuendelea kuchangia damu zaidi ili kuokoa maisha ya wagonjwa wenye uhitaji wa damu waliopo kwenye vituo mbalimbali vya afya nchini.

Akizungumza wakati wa hitimisho la zoezi la uchangiaji damu kwa siku tatu kwenye viunga vya stendi ya mabasi ya Mbagala jijini Dar es Salaam ili kusaidia majeruhi hao, mwamasishaji jamii kutoka NBTS, Mariamu Juma, alisema shukurani hizo zinafuatia mafanikio makubwa yaliyopatikana wakati wa zoezi hilo muhimu lililoandaliwa na NBTS kwa kushirikiana na benki ya Exim Tanzania.

"Kwa kweli mwitikio ulikuwa wa kuridhisha na tumefanikiwa kukusanya chupa takribani 155 kulingana na malengo yetu, hivyo tunawashukuru sana wakazi wa Mbagala na vilevile tunawashukuru sana Benki ya Exim Tanzania ambao ni washirika wetu wakubwa kwa kujitoa kwao kwa hali na mali hadi kufanikisha zoezi hili," alisema na kuongeza:

"Pamoja na wakazi wa Dar es Salaam kwa ujumla wanaoendelea kuchangia damu kwenye vituo vingine ikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili."

Tangu kutokea kwa ajali hiyo ya moto mkoani Morogoro imeshuhudiwa idadi kubwa ya wakazi wa Dar es Salaam na kwinginepo nchini wakiguswa na kuitikia wito wa kuchangia damu kwa majeruhi hao ambapo imearifiwa kuwa bado kuna uhitaji wa damu, huku jamii ikiendelea kuhamasishwa kujitolea zaidi ili kuokoa maisha ya wagonjwa wenye uhitaji.

# Kilimo hai kahawa chatajwa kuwa fursa

**Na Restuta Damian, KYERWA**

BODI ya kahawa Kagera imetoa wito wa kuchangamkia fursa ya wakulima kulima kilimo hai, ili kuondokana na tatizo la masoko kwa wakulima wanaolima kahawa kwa kiwango cha chini.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja wa Bodi ya Kahawa Kagera, Melkiol Massawe, walipotembelea shamba la mkulima bora wa kahawa aina ya Robusta Tanzania lenye ekari zaidi ya 100 pamoja na kumpa elimu zaidi.

Alisema kilimo hai hakina usumbufu katika soko la dunia na la ndani kutokana na kahawa hiyo kulimwa pasipo kutumia dawa zenye sumu.

"Kahawa ya kilimo hai ambayo inalimwa kwa mkulima huyu Albert Katagira ni tofauti sana na kahawa inayolimwa na wakulima wengine mkoani Kagera kwani walio wengi wanatumia mbolea ya sumu, lakini mkulima huyu anatumia mbolea ya asili ambayo ni nyasi, masalia ya migomba, mbolea ya samadi pamoja na mboji ambapo kahawa inayozalishwa katika mashamba yake ni bora kwa matumizi ya watu wote kwa sababu ni bora kiafya," alisema Massawe.

Katagira ambaye ni mkulima bora Tanzania kwa mwaka 2019, alisema shamba lake la ekari 100, kati ya ekari 50 zimepandwa na kwa mwaka amevuna magunia 400.

Katagira alisema ili kilimo kiweze kuleta manufaa, lazima wakulima kuongeza bidii katika kilimo kwa kuzalisha malighafi nyingi ambayo itamsaidia kuongezea kipato cha familia na jamii inayomzunguka na kuleta maendeleo.

"Nitumie nafasi hii kuwashauri wakulima wenzangu kulima kilimo cha kulinda afya zetu na kujiongeza kuanzisha viwanda ambavyo vitasaidia kuchakata malighafi itakayosaidia kuongeza thamani katika mashamba yetu," alisema na kuongeza:

"Ndio maana niliamua kufanya kilimo cha kisasa ambacho nikilima hekta moja ninavuna tani 1.7 kwa msimu."

# Wafunzwa athari mimba utotoni

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

KATIKA jitihada za kukabiliana na ndoa za utotoni wasichana takribani 70 wa Wilaya ya Longido mkoani Arusha, wamefunzwa athari za ndoa hizo kwa lengo la kuihamasisha jamii kuziepuka.

Mabinti hao wenye umri wa miaka 11 hadi 17 walipata elimu hiyo wametakiwa kupinga mila na desturi kandamizi zinazowalazimisha kufanyiwa vitendo vya kujamiiana ambavyo ni ukatili dhidi ya mtoto wa kike.

Mafunzo hayo yalitolewa na Shirika la Maendeleo ya Jamii (Pido) linalofanya kazi zake wilayani Longido.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Martha Ntoipo, alisema Pido ilianza kufanya shughuli zake tangu mwaka 2010 ikijikita katika masuala ya elimu juu ya afya ya uzazi, vita dhidi ya mimba na ndoa za utotoni, madhara ya ukeketaji pamoja na mafunzo juu ya maambukizi ya VVU na Ukimwi.

"Tumeona tutibu tatizo kabla halijakuwa kubwa, watoto hawa wafahamu madhara ya mimba na ndoa za utotoni, tunaamini watapokea na mabadiliko yataonekana," alisema Martha.

Aidha, alisema baadhi ya mila na desturi kandamizi kwa jamii ya kifugaji zimekuwa zikikwamisha malengo mbalimbali ya serikali.

"Kuwavusha wanawake salama, kinamama wajawazito ni malengo ya serikali, ila mila zinakwamisha, mfano mimba za utotoni, ndoa za utotoni pamoja na ukeketaji, wanawake wengi wanapoteza maisha, vifo vya mama na mtoto, kutokana na kushindwa kumudu afya ya uzazi, yote ni mila na desturi kandamizi," alisema Martha.

Juni 21 Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alizindua kampeni ya jiongeze tuwavushe salama wilayani hapa, iliyobeba dhamira ya kuokoa maisha ya mama na mtoto kabla na baada ya kujifungua.

Aidha, aliwataka kinamama wajawazito kuacha kujifungulia majumbani.

Kauli mbiu katika kampeni hiyo ilikuwa "Kila mmoja wetu anao wajibu wa kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi, na vya watoto wachanga, maneno basi, sasa vitendo."

Mwaisumbe alisema ili kufikia malengo ya kitaifa ya asilimia 80 kupunguza vifo vya mama na mtoto, kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa jamii, pamoja na kuhakikisha vifaa tiba vinapatikana katika vituo vyao vya afya.

" Tuhakikishe tunaowakunga wa kutosha kwenye vituo, wahudumu wa afya, pamoja na madaktari vikiambatana na vitendea kazi," alisisitiza Mwaisumbe.

Mratibu wa Kitengo cha Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto wilayani hapa, Josiah Mruve, alipokuwa akiwasilisha taarifa kwa Mkuu wa Wilaya Mwaisumbe, alisema kiwango cha kinamama kujifungulia katika vituo vya afya, kimeongezeka kutoka asilimia 27 mwaka 2017 hadi asilimia 51.3 mwaka 2019.

"Lakini pia kumekuwa na ongezeka la wanaume kuhudhulia kliniki na wake zao kwa asilimia 59.2 tofauti na miaka ya nyuma, hii ni dhahiri wamekuwa na uelewa juu ya afya ya uzazi," alisema Mvure.

# Shule binafsi zajipanga kufaulu

**Novatus Makunga,** ARUSHA

SHULE binafsi za msingi na sekondari katika Mkoa wa Arusha, zimekuja na mkakati wa kuanzisha maonyesho ya wazi yajulikanayo kama elimu fair, ikiwa ni jitihada za kukabiliana na ushindani kutoa elimu bora.

Mkoa wa Arusha umekuwa ukifanya vizuri katika matokeo ya mitihani ya taifa kwa shule za msingi na sekondari, kwa vipindi tofauti ambapo kwa mwaka huu wa 2019 umeshika nafasi ya kwanza kitaifa, katika matokeo ya kidato cha sita.

Maonyesho hayo yaliyoshirikisha shule 11 yalifanyika mwishoni mwa wiki mjini hapa.

Wamiliki na mameneja wa shule walioshiriki katika maonyesho hayo, Getrude Vitus na Ursula Trappr walisema maonyesho hayo yakitumika vizuri yana nafasi kubwa ya kukuza sekta ya elimu, ambayo ni muhimu katika maendeleo ya taifa.

**Mpango huo umesababisha ushindani mkubwa baina ya shule za serikali na shule binafsi ambazo zimeanza jitihada za kukabiliana na ushindani huo.**

"Hivi sasa kila mmoja anajitangaza kwenye mitandao bila kuwapo kwa nafasi ya kukutana na wazazi wengi watahangaika kutafuta nafasi za shule za watoto wao kwa kuwauliza wasiohusika," alisema Vitus.

Aliongeza kuwa maonyesho hayo yamezileta shule nyingi kwa pamoja katika eneo moja na hivyo kuwarahisishia wazazi kupata maelezo na kuuliza maswali, ambayo mwisho wa siku yanawapa maamuzi ya kuchagua shule wanayoitaka.

Mratibu wa maonyesho hayo, Mary Mwananogu alisema kuwa kupanda kwa viwango vya ufaulu kwa shule za msingi na sekondari, ni matokeo chanya ya mpango wa serikali wa kutoa elimu bure.

"Mpango huo umesababisha ushindani mkubwa baina ya shule za serikali na shule binafsi ambazo zimeanza jitihada za kukabiliana na ushindani huo," alisema.

Mmoja ya wazazi walioshiriki maonyesho hayo, Peter Manjala, alisema hiyo ni nafasi nzuri na muhimu kwa wamiliki na wasimamizi wa shule, kuonana na watu wanaotafuta shule kwa vijana wao.

"Ni wazo zuri la kusaidia kukuza elimu yetu na likitumika vizuri litaleta hata muunganiko wa malezi ya watoto kati ya walimu, wamiliki wa shule na wazazi," alisema.

Maonyesho hayo yameonyeshwa kwa msimu wa kwanza, ambapo Shule 11 zinazotoa elimu kwa mtaala wa kitaifa na kimataifa zimeshiriki maonyesho hayo.



Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara, Martha Umbullah (CCM), akizungumza na wanachama wa Umoja wa Wanawake wa UWT Tarafa ya Moipo wilayani Simanjiro juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# CCM kimasomaso uchaguzi Simanjiro

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

DIWANI wa Kata ya Orkesumet wilayani Simanjiro Mkoa wa Manyara, Sendeu Laizer, amechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa kipindi kijacho cha mwaka mmoja.

Laizer (CCM) ambaye hakuwa na mpinzani kwa Chadema amepata kura 19 za ndiyo na kura nne za hapana, hivyo kushika nafasi hiyo iliyokuwa inashikiliwa na Diwani wa Kata ya Ngorika Albert Msole.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Silvanus Tairo, akitangaza matokeo ya uchaguzi huo juzi alisema madiwani 23 akiwamo Mbunge wa Jimbo hilo, James Ole Millya, wameshiriki upigaji kura huo.

Tairo alisema Chadema yenye madiwani watano hawakupitisha mgombea wao, hivyo Laizer wa CCM, baada ya kukosa mpinzani amepigiwa kura ya ndiyo au hapana.

Akizungumza baada ya kutangazwa kushikilia nafasi hiyo Laizer alisema, imani kubwa waliyomwonyesha madiwani hao ndiyo nguzo kubwa atakayoitegemea kufanya kazi hiyo.

"Nawashukuru wote pamoja na madiwani wa Chadema ambao kwa namna moja au nyingine mmeniunga mkono, kwani hamkusimamisha mgombea wa nafasi hii japokuwa uwezo mlikuwa nao," alisema Laizer.

Kwa upande wake, Msole ambaye ameshikilia nafasi hiyo kwa muda wa miaka minne, aliwashukuru madiwani hao kwa ushirikiano mkubwa waliompatia.

"Nilikuwa msaidizi wa mwenyekiti wa halmashauri yetu kwa miaka minne mfululizo tangu mwishoni mwa mwaka 2015 hadi sasa 2019, nawashukuru sana kwani tumeshirikiana kuijenga Simanjiro kwa pamoja," alisema Msole.

Diwani wa Kata ya Endiamtu, Philemon Oyogo (Chadema) alisema waliamua kutoweka mgombea wa nafasi hiyo, kwani demokrasia inawaruhusu kufanya hivyo.

Diwani wa Kata ya Komolo, Michael Haiyo (CCM), alimpongeza Laizer kwa kuchaguliwa kushika nafasi hiyo na alimtakia kila la heri katika kutumikia nafasi hiyo.

# DC aonya watakaookwamisha jitihada za JPM uwekezaji

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MKUU wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, ameonya kuwa mtu yeyote au kikundi chochote kitakachoibuka kukwamisha juhudi za Rais John Magufuli kuvutia uwekezaji wenye tija kiuchumi katika sekta za madini na viwanda wilayani humo atashughulikiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria za nchi.

Senyamule alikuwa akizungumza jana, wakati akifungua mkutano wa siku moja wa baraza la biashara la wilaya hiyo ambalo lilikutana chini ya maofisa wa Wizara ya Viwanda na Biashara.

"Tunataka Same iwe kimbilio la wawekezaji, kwa kutoa huduma nzuri kwao na niseme wazi kwamba hatutamvumilia mtu atakayekwamisha juhudi hizi zilizoanzishwa na Rais wetu," alieleza.

**Tunataka Same iwe kimbilio la wawekezaji, kwa kutoa huduma nzuri kwao na niseme wazi kwamba hatutamvumilia mtu atakayekwamisha juhudi hizi zilizoanzishwa na Rais wetu.**

Alisema majadiliano yaliyofanyika baina ya sekta ya umma na binafsi yameweza kutatua matatizo yanayoikabili sekta ya biashara na kwamba hivi sasa baraza hilo limeanzisha vikosi kazi kwa ajili ya kuanza mchakato wa kuvutia wawekezaji katika sekta za utalii, mazingira na biashara, madini na viwanda, kilimo, mifugo na uvuvi, elimu na afya.

Baraza hilo lilikutana kutekeleza agizo la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, aliyeagiza mabaraza yote nchini kuhuishwa kutokana na utendaji wa mabaraza hayo umekuwa siyo endelevu.

Kitendo cha mabaraza hayo katika ngazi ya mikoa na wilaya nchini, kutofanya vikao vya aina hiyo ni kukiuka waraka wa Rais Namba 1 wa mwaka 2001, unaosisitiza kuanzishwa kwa mabaraza hayo na utendaji wake kuwa endelevu.

Dhumuni la kuanzishwa kwa mabaraza ya biashara hususani katika ngazi ya wilaya na mikoa ni kuweka mfumo rasmi wa kuwakutanisha viongozi wakuu wa serikali na sekta binafsi katika kila ngazi ya utawala ili kujadiliana jinsi ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Pia inalenga kukuza sekta binafsi ambayo ndio muhimili muhimu wa kukuza uchumi wa nchi.

Aidha, kwa mujibu wa Senyamule, katika kikao hicho cha kuhuisha Baraza la Biashara la Wilaya ya Same, wamekubaliana kuanza kwa kutekeleza jukumu hilo kwa ari mpya ili kuifanya wilaya kukua haraka.

"Kwa hiyo tumekuja pia na mkakati maalum wa kutangaza fursa zilizopo wilayani kwetu kama vivutio vya utalii ili kuongeza idadi ya watalii wanaokuja kuvitembelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, imeshaleta wataalamu wake kutoa elimu kwanza kuhusu blue print (mpango mkakati) itakavyofanya kazi ya kuboresha mazingira ya biashara," alieleza zaidi Mkuu huyo wa Wilaya.



Mjumbe wa kamati ya ujenzi sekondari mpya ya vijijini vya Kigera Etuma na Kakisheri, Musoma Vijijini, mkoani Mara, Stella Majira, akishiriki katika kuandaa saruji kwa ajili ujenzi wa msingi wa madarasa ya shule hiyo jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Meya kuongoza ujumbe ziara ya Ujerumani

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

UJUMBE maalum wa maofisa unaoongozwa na Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, unatarajia kuondoka mjini hapa wakati wowote, kwenda Ujerumani kusaini makubaliano ya kupokea mitambo ya kuchakata takataka na kutengeneza mbolea.

Akizungumza jana na Nipashe katika mahojiano maalum kuhusu taarifa za kuiva kwa mradi huo, alisema mitambo hiyo iko tayari inasubiri kukamilishwa kwa taratibu za kusafirishwa kuja nchini.

"Tuko katika maandalizi hivi sasa ya kwenda nchini Ujerumani, kusaini makubaliano ya kupokea mitambo mikubwa ya kisasa inayotumika duniani kuchakata takataka na kisha kubadilishwa kuwa mbolea za kukuzia mazao mbalimbali, tunakwenda kufanya hivyo baada ya kuafikiana na wenzetu ambao tumekuwa tukishirikiana nao kama mji dada," alisema Mboya.

Alisema kiwanda hicho cha kuchakata takataka na kuzalisha mbolea, uwekezaji wake unakisiwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 900.

Mradi huo unatarajiwa kujengwa katika eneo lake la dampo lililopo kati ya Kata ya Kaloleni na Njoro.

Kwa mujibu wa meya huyo, mchakato wa kuileta mitambo hiyo na kuweka miundombinu yake ukikamilika, mradi huo utaongeza uwezo wa halmashauri hiyo kuzoa taka kutoka tani 168 kwa siku hadi kufikia tani 230.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda hicho kutatoa fursa za ajira kwa vijana, serikali kuongeza mapato yake kupitia uzalishaji wa mbolea na pia mradi huo utaongeza ufanisi katika udhibiti wa usafi.

"Mkakati wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ni kutaka kuendelea kubakia kileleni na kutetea heshima yake ya kuwa kinara wa usafi wa mazingira kitaifa. Tulianza mchakato huu wa uwekezaji katika hifadhi ya mazingira, kwa kuagiza malori makubwa matatu nchini China ambayo yana uwezo wa kuchukua tani 100 kwa awamu moja," alisema Mboya.

# Jaji mfawidhi awapa somo mahakimu kesi za watoto

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi, Dk. Fauz Twaib, ametoa 'dira' kwa mahakimu wa mkoa wa Kilimanjaro ya namna gani wanaweza kujielekeza kushughulikia mashauri ya watoto ili kupunguza kesi hizo mahakamani.

Dk. Twaib ametaka mahakimu hao na wadau wa mahakama walioanza kujengewa uwezo zaidi wa kushughulikia kesi hizo katika Mahakama za Watoto, kupitia sheria zote zinazohusiana na watoto.

Hayo yamo katika maelekezo yake aliyoyatoa jana, kwa washiriki 45 ambao ni mahakimu na wadau wa mahakama, wakiwamo Waendesha Mashtaka wa Polisi (PP), Ofisi ya Mawakili wa Serikali na Maofisa Ustawi wa Jamii.

"Ili kuongeza ufanisi, nasisitiza kwamba wekeni katika vitendo maarifa mtakayoyapata wakati wa kushughulikia mashauri ya watoto katika Mahakama za Watoto. Lengo la mafunzo haya ni kuwapatia ninyi ujuzi na maarifa zaidi ya kutafsiri na kutekeleza Law of the Child Act No. 21 of 2009, (Sheria ya Watoto, Namba 21 ya Mwaka 2009)," alisema Jaji Twaib.

Mafunzo hayo ya siku tano yaliyoanza Agosti 19, hadi Agosti 23 katika Mji wa Moshi, yanaratibiwa na kuendeshwa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) kilichopo mkoani Tanga.

Mahakama ni moja kati ya mihimili mitatu ya dola, wenye jukumu la msingi la kutoa haki sawa kwa wote na kwa wakati.

Mhimili huu hufanya kazi ya kutafsiri sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge la Tanzania ili kuwapatia wananchi haki.

Mhimili huo wa Mahakama ya Tanzania, unasimamia haki za watoto kama zilivyo haki nyingine wanazostahili kuzipata wananchi wa Tanzania.

Mahakama ya Watoto ilianzishwa kisheria, kwa lengo la kushughulikia kesi maalum zinazohusu watoto.

Ukurasa 18



Boris Johnson ajiandaa kuliburuza Bunge kuhusu Brexit Uingereza

Kunahitajika chombo kitaifa kuratibu shughuli za serikali



Ukurasa 15

# Kimataifa



## Waandamana sababu ya ukosefu wa usalama Mashariki ya DRC

Ukurasa 17

siasa

JUMATANO AGOSTI 21, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



## JPM alivyofanikisha kampeni ya Kiswahili kuwa lugha ya SADC

Ukurasa 14

### BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-10

PIUS Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa Serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kina-

Endelea 16



Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

## India yapimana nguvu na Pakistan

Ukurasa 20

# JPM alivyofanikisha kampeni ya Kiswahili kuwa lugha ya SADC

Na Beatrice Moses



Mwenyekiti wa SADC, Rais John Magufuli (kulia), akiwa na Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa (katikati). Kushoto ni Rais wa Nambia Hage Geingob. **PICHA: MTANDAO**

"MCHEZA Kwao hutuzwa" ni msemo wa Wahenga wenye ujumbe mzito unaoweza kutumika kuelezea hatua ya mafanikio ya kampeni iliyoanzishwa na Rais John Magufuli ya kupigia debe matumizi ya Lugha ya Kiswahili.

Rais Magufuli ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), amezichanga vyema karata zake katika dhima ya kuhakikisha kwamba Kiswahili kinapata fursa ya kuwa lugha rasmi ya nne kwenye shughuli za jumuiya hiyo.

Agosti 18 mwaka huu akitoa hotuba ya kufunga mkutano wa Wakuu wa SADC, Rais Magufuli alisema kupitishwa rasmi kwa Kiswahili kuwa lugha ya nne katika Jumuiya hiyo ni faraja kwa sababu ndiyo lugha iliyotumika kwenye mafunzo ya harakati za ukombozi.

"Ni heshima kubwa kwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere ambaye aliongoza harakati za ukombozi zilizofanywa na wapigania uhuru barani Afrika," anasema na kuongeza:

"Kutokana na upendo wake kwa watu wa mataifa mengine ya Afrika, alikubali taifa na wananchi wake wateseke ili kufanikisha ukombozi huo."

Akitumia Lugha adhimu ya Kiswahili katika hotuba hiyo, Rais Magufuli anabainisha juhudi kubwa zilizofanywa na Tanzania kuhakikisha amani na utulivu vinapatikana katika ukanda wa SADC na Bara la Afrika kwa ujumla.

Anatoa mfano wa namna Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lilikwenda nchini Shelisheli kuzima Mapinduzi mwaka 1975 ambapo Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi alishikilia uongozi wa nchi hiyo kwa muda.

### MCHANGO WA KISWAHILI

Akizungumzia mchango wa Kiswahili baada ya kupitishwa rasmi kuwa lugha ya nne ya SADC baada ya Kiingereza, Kifaransa, na Kireno, Rais Magufuli anabainisha kuwa kutasaidia kwa kiasi kikubwa kukuza ushirikiano na utengamano wa wananchi.

"Kiswahili ni Lugha ya Afrika na sisi ni wananchi wa Bara hili, hivyo tunapaswa kuitumia...ni vyema kama viongozi wa nchi za SADC wataiga mfano wa Afrika ya Kusini ambayo itaanza kufundisha Kiswahili katika shule zake kuanzia mwakani," anasema.

Anabainisha kuwa Tanzania ipo tayari kusaidia kufanikisha malengo ya kufundisha na kutumia Kiswahili katika shughuli mbalimbali kwenye ukanda wa SADC.

Awali akifungua mkutano huo, Rais Magufuli alitumia Lugha ya Kiingereza kuwashawishi viongozi wenzake wamruhusu kutoa hotuba yake ya ufunguzi kwa Lugha ya Kiswahili.

"Nina imani kwa kufanya hivyo mtashawishika kukubali na kupitisha Kiswahili kuwa lugha rasmi ya SADC, lugha ambayo ilitumika wakati wa harakati za ukombozi," anasema.

Anabainisha kwamba Kiswahili ni lugha kubwa ambayo tayari inazungumzwa kwenye nchi 34 za Afrika, kati ya hizo sita ziko katika SADC.

### HARAKATI ZA KUKIPIGANIA KISWAHILI

Harakati za Rais Magufuli kuipigania lugha hiyo itumike ipasavyo Afrika na katika uga wa kimataifa hazikuanzia kwenye mkutano huo.

Amekuwa akisisitiza matumizi ya lugha hiyo kwenye warsha na mikutano mbalimbali nchini na nje ya nchi.

Ni vyema kwamba hatimaye azma yake imefanikiwa hasa baada ya kuitumia vyema ardhi yake ya nyumbani na nafasi yake ya uenyekiti wa SADC kuchombeza vionjo, faida na umuhimu wa matumizi ya lugha hiyo.

### SEIF KHATIBU

Mohamed Seif Khatib ni mwanasiasa anayetajwa kuwa mwalimu na mpenzi wa lugha ya Kiswahili, anazungumzia hatua hii akimpongeza Rais Magufuli kwa kujitokeza hadharani na kuendesha kampeni ili Kiswahili iwe lugha rasmi SADC.

Khatibu ambaye pia ni mwanasiasa mkongwe aliyewahi kushika uongozi ndani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na uwaziri anabainisha kuwa juhudi zinazofanywa na Rais Magufuli zitakuwa na manufaa iwapo utekelezaji wake utafanywa kwa mikakati madhubuti.

### CHAKUBALIWA AFRIKA

Khatib anabainisha kuwa miaka sita iliyopita Umoja wa Afrika (AU) ulipitisha rasmi kwamba Kiswahili kianze kutumika kama mojawapo ya lugha rasmi Afrika.

"Ni hatua ambayo ilikuwa ni fursa muhimu lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua," anasema.

Mwanasiasa huyu aliye miongoni mwa waumini wazuri wa matumizi ya lugha hiyo maridhawa, amekuwa akiitumia katika utunzi wa nyimbo mbalimbali za taarab, kuandika mashairi ambayo yamechapishwa kwenye magazeti na majarida tofauti.

Miongoni mwa vitabu vyake ni pamoja na 'Pambazuko la Afrika, Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar na 'Fungate' ya Uhuru.

Anabainisha kuwa hata Ilani ya CCM Ibara ya 95 inabainishwa kuwa Kiswahili kitakuwa bidhaa.

"Kwa hiyo kupitishwa kuwa lugha rasmi ni fursa kubwa kwa Watanzania hasa vijana waliosoma masuala ya lugha na ualimu ambapo watapata ajira za kwenda kufundisha au kutafsiri," anasema na kuongeza:

"Hatua hii imefikiwa kutokana na juhudi binafsi alizozifanya Rais Magufuli, kwani wamepita marais kadhaa nchini tangu uhuru upatikane lakini huyu ndiye wa kwanza aliyejitokeza wazi kupigia kampeni matumizi ya lugha hii," anasema Khatibu.

### ANGALIZO

Khatib anatoa angalizo kwamba iwapo utekelezaji wake hautasimamiwa vizuri basi inaweza kuwa kama maagizo yaliyotolewa kule AU, kuhusiana na matumizi ya lugha hiyo ambapo utekelezaji wake si madhubuti.

"Hivyo ni vyema kwa nafasi yake ya uenyekiti Tanzania ijipange vyema kuhakiksha jambo hili linatekelezwa na kuwa na mafanikio yaliyokusudiwa," anasema na kuongeza:

"Tumepata bidhaa nzuri ya kuuza... Kiswahili ni bidhaa...Rais Magufuli amekuwa mfano wa kuhakikisha anafanikisha matumizi ya lugha ya Kiswahili."

### WENGINE

Baadhi ya viongozi wamejitokeza pia kuunga mkono kampeni hizo za Rais Magufuli na miongoni mwao ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki nchini Profesa Palamagamba Kabudi.

Prof. Kabudi amehakikisha anasimamia na kuwezesha mapendekezo ya kuifanya lugha hii kuwa rasmi ya SADC yanafka kwenye mkutano wa wakuu wa nchi wanachama uliomalizika karibuni.

Akiwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la SADC, Profesa Kabudi aliwajulisha waandishi wa habari kuwa Baraza hilo liliwasilisha mapendekezo yake kwenye Mkutano wa 39 wa Wakuu wa nchi na Serikali wanachama wa SADC likiwamo la kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya nne katika nchi 16 wanachama.

"Wajibu wa baraza letu ni kutoa mapendekezo ambayo hupelekwa kwa wakuu wa nchi wanachama kwa ajili ya kuyatolea maamuzi....kwetu ni heshima kubwa, Kiswahili ni lugha ya ukombozi," anasema.

### DK. SHEIN

Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dk Ali Mohamed Shein naye alijiunga na harakati za kuipigia debe lugha hii maridhawa wakati akifunga Maadhimisho ya Maonyesho ya Nne ya Wiki ya Viwanda SADC.

Dk Shein anabainisha kuwa wazo la kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha rasmi za mawasiliano katika majukwaa ya SADC ni jambo jema.

"Hii ni hatua muhimu kuimarisha umoja na mshikamano kwa wanachama wa Jumuiya hii pamoja na kukuza shughuli za biashara na viwanda," anasema.

Anabainisha kwamba historia inaonyesha namna ambavyo Kiswahili kimeweza kuwaunganisha Watanzania kuwa wamoja.

"Licha ya kwamba Watanzania wanazo lugha tofauti za makabila mbalimbali, bado Kiswahili kimekuwa na mchango mkubwa katika harakati za ukombozi wa Afrika," anasema.

Anabainisha kuwa lugha ya Kiswahili imerahisisha mawasiliano na kukuza biashara katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na tayari AU imeikubali iwe ni Lugha rasmi.

"Kwa hivyo, wazo la kukifanya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha rasmi za SADC ni muhimu na vyema tukaungana kulifanyia kazi suala hili," anasema.

# Kunahitajika chombo kitaifa kuratibu shughuli za serikali

**Na Dk. Felician Kilahama**

AWALI ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na wingi wa neema lakini pia kutupatia uwezo na nguvu kusimamia na kutumia rasilimali zilizopo kwa faida ya kizazi hiki na vizazi vitakavyofuata.

Tanzania imejaliwa kupata rasilimali na vivutio vya kipekee duniani. Kidunia ukitaja Mlima Kilimanjaro, Mbuga za Serengeti na Ngorongoro itafahamika unamaanisha Tanzania.

Tanzania pia imejaliwa kuwa na misitu ya asili yenye thamani kubwa duniani mfano, Hifadhi Misitu Asilia (Nature Forest Reserve) zaidi ya 12 hasa kwenye Milima ya Tao la Mashariki (Eastern Arc Mountains).

Misitu hiyo ni muhimu kuhifadhi makazi ya bioanuwai na vyanzo vya mito mikubwa nchini (i.e. Kagera, Kilombero, Kihansi, Mara, Pangani, Wami, Ruaha, Ruvu, Ruvuma, na Zigi).

Vilevile, taifa letu limebahatika kuwa na madini aina mbalimbali na vito vya thamani (germ stones).

Isitoshe kuna rasilimali samaki za kutosha kwenye maji baridi na yenye chumvi baharini bila kusahau ardhi ya kutosha na rasilimali watu zaidi ya milioni 50.

Haya yote ni hazina kubwa katika Tanzania je, rasilimali hizo tunazitumia vipi kujiletea maendeleo endelevu sisi na kwa faida ya vizazi vitakavyofuata?

Julai 31 na Agosti Mosi, 2019 Taasisi ya Uongozi kupitia Jukwaa la Maendeleo Endelevu (Green Growth Platform); iliandaa Kongamano lililofanyika Jijini Dodoma kwenye Ukumbi wa TAKWIMU.

Kongamano lilihusu utunzaji na usimamizi imara wa misitu kwa upatikanji endelevu wa maji kwa matumizi mbalimbali nyumbani na shughuli za kiuchumi.

Kwenye kongamano hilo jumla ya mada nne zilitolewa zikifuatiwa na majadiliano kupitia Jopo la Wataalamu watano waliobobea katika masuala ya rasilimali misitu na maji.

Baada ya hapo ukafuata mjadala wa pamoja, maoni na majumuisho hatimaye kutembelea msitu wa Chenene na chanzo cha maji Mzakwe.

Wadau waliweza kujifunza uhusiano kati ya msitu Chenene na Mzakwe na kushauri nini kifanyike ili kuhakikisha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma unakuwa endelevu.

Kongamano lilifunguliwa na Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Vilevile, walihudhuria George Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; George Simbachawene, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano na Dk. Benilith Mahenge, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

Kongamano lilifikia kwa asilimia 88 ya waliokuwa wametarajiwa kuhudhuria hususani Maofisa Waandamizi kutoka Sekta za Umma na Binafsi wakiwemo viongozi wa Taasisi na Mashirika mbalimbali pamoja na Wakuu wa Mikoa ya Katavi, Mbeya na Ruvuma na Wakuu wa Wilaya za Bahi, Kilolo, Mufindi, Nantumbo na Rufiji.

Kabla ya ufunguzi, Prof. Joseph Semboja, Mtendaji Mkuu, Taasisi ya Uongozi alitoa maelezo ya utangulizi kwanza, kwa kumshukuru Makamu wa Rais kukubali kuwa Mlezi wa Jukwaa la Maendeleo Endelevu na pili, kukubali kuwa Mgeni Rasimi.



Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan.**PICHA: MTANDAO**

Kimsingi Kongamano lilikuwa na mafanikio ya kutosha kutokana na majadiliano ya kina na matokeo ya kutembelea msitu Chenene na rasilimali maji Mzakwe.

Hata hivyo, nilijifunza kuwa baadhi ya waliostahili kuhudhuria hawakufanya hivyo kutokana na kukabiliwa na majukumu mengine au kushiriki kwenye kongamano au semina nyingine.

Kwa miaka mingi kumekuwepo na hali ya sekta au taasisi mbalimbali kupanga na kutekeleza shughuli zake bila kushirikisha wadau ipasavyo.

Tunajifungia kwenye ofisi zetu na kukosa kujua nini matokeo kwa sekta zingine kutokana na shughuli tunazozifanya hasa kwa taasisi au sekta ambazo zinategemea sana matumizi ya rasilimali ardhi na vilivyopo juu/chini yake (inadequate cross-sectoral linkages).

Mfano, sekta kama kilimo, mifugo, maji, misitu, wanyamapori, uvuvi, umwagiliaji, madini, miundombinu, viwanda, nishati, vijiji na ardhi).

Kutokana na kutokuwepo uratibu madhubuti kuhusu shughuli za kila sekta au taasisi, matokeo ya utendaji au utekelezaji wa kazi za kila siku kisekta au taasisi; yamekuwa na changamoto kadhaa kutokana na kutoratibiwa shughuli za kisekta au taasisi ipasavyo.

Uzoefu unaonyesha kuwa kufanya kazi kisekta au taasisi bila kuhusisha wadau kikamilifu tumekuwa tukitumia fedha au muda kutekeleza shughuli zinazoshabihiana (duplication of efforts) lakini bila kukusudia tunajikuta tunasababisha madhara kwa sekta zingine.

Mathalani, kupoteza misitu kutokana na kilimo cha kuhamahama (shifting cultivation); kuchunga mifugo kiholela maeneo yaliyohifadhiwa kisheria; kufyeka na kuchoma misitu moto na masuala ya nishati ya kupikia kusababisha misitu kuharibika kisa matumizi makubwa ya mkaa nakadhalika.

Kila sekta au taasisi kufanya kivyake (operating in silos/boxes) mfano, misitu, nishati, kilimo na mifugo) na nyinginezo: ni matokeo ya kutokuwepo na Chombo madhubuti cha kurartibu shughuli za kisekta ili kuondoa changamoto katika matumizi ya rasilimali zetu kwa faida ya wote.

Misitu inatoweka kwa kasi kubwa kutokana na shughuli za sekta nyingine na kwa miaka mingi kumekuwepo ushirikishwaji hafifu wakati wa kutunga Sera au kutayarisha mikakati ya kutekeleza shughuli za kisekta/taasisi hivyo kukosa nguvu ya kupata matokeo chanya.

Huenda rasilimali maji zinaathirika kwa njia hiyohiyo. Serikali kupitia Sera ya Uchumi wa Viwanda imefanya sahihi kuweka Kituo kimoja cha kuratibu shughuli za wawekezaji ndani na kutoka nje (Tanzania Investment Centre-TIC).

Sasa taifa linahitaji Kituo kama hicho kuratibu shughuli za Kisekta au Taasisi kuhusu masuala ya Kongamano, Semina na Mikutano inayohitaji ushiriki wa Wadau ili kuondoa mkanganyiko kwa shughuli zinazofanana kutekelezwa wakati mmoja wakati wadau ni walewale: ni kama kugombania watakaoshiriki.

Kukiwepo na chombo cha kuratibu shughuli hizo itakuwa rahisi kupunguza gharama na kupata matokea chanya na kuongezeka ushirikiano kati ya sekta au taasisi hasa zenye shughuli za kutumia rasilimali asilia ikiwemo ardhi na watu.

Ili tufanye vizuri zaidi tunahitaji Uratibu sahihi na Chombo hicho kitahakikisha tunafanikiwa vizuri.

Nitumie fursa hii na kwa heshima na taadhima nimwombe Dk. John Magufuli, Rais wa Serikali ya awamu ya Tano; Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa manufaa yetu wote, aridhie kuanzishwe Chombo cha Kitaifa kuratibu shughuli za Serikali hasa zinazoshabikiana kiutendaji. Ninachomaanisha ni Chombo au Mamlaka kwa nia ya kuondokana na mazoea ya kufanya kazi kisekta au kitaasisi na kutotumia muda, rasilimali fedha na watu vizuri.

Faida ni kuhakikisha mipango ya sekta au taasisi husika hasa inayohusu masuala kama kongamano, semina au mikutano ya kuandaa au kuboresha Sera au Mikakati ya kufanikisha maendeleo endelevu inaratibiwa ipasavyo (effective coordination).

Chombo au Mamlaka itapitia na kuangalia ni shughuli zipi zinashabihiana na kuelekeza wahusika wakae na kutayarisha utekelezaji wa pamoja (cross-sectoral linkages).

Kwa kufanya hivyo tutaepuka kufanya yanayofanana kwa wakati mmoja na kuokoa fedha na muda.

Siyo hivyo tu bali pia kuimarisha ufanisi na kuongeza tija kwa shughuli za Serikali pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi au sekta mbalimbali kwa faida ya taifa letu.

***Mwandishi ni Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki Mstaafu.***

UCHAMBUZI

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-10



Vijana wa chipukizi wakionyesha manjonjo kwenye maadhimisho ya 53 ya Muungano wa Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

**Inatoka Uk. 13**

choweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa na leo hii tunaendelea kutokea tulipoishia wiki iliyopita. Endelea na sehemu hii

ya 10 ya kitabu hicho inayoanzia na sehemu ya 6.6 ya Kitabu hicho….

6.6 Kinga halisi ni kuwapo kwa Utashi wa Kisiasa (Political will)

Mifano hii unatuonesha kwamba, kinga ya uhakika dhidi ya kuvunjika kwa Muungano, ni kuwapo kwa Utashi wa kisiasa kwa Viongozi Wakuu wa nchi husika zilizoungana. Ndiyo kusema kwamba, haijalishi kama Muungano ni wa Serikali mbili au Serikali tatu, utashi wa kisiasa ukitoweka, Muungano utavunjika.

Kwa mfano, tumekwishakuona kwamba, lile tukio la uzushi na uwongo lilielezwa hapo juu katika kifungu cha 'Masimulizi ya Sheikh Thabit Kombo' lilikaribia sana kuvunja Muungano wetu. Muungano uliingia katika hatari ya kuvunjika siyo kwa sababu ya muundo wake wa Serikali mbili, bali ni kwa sababu lilimfanya Rais Nyerere aamini (kwa kudanganywa) kwamba, Rais Karume alikuwa hana tena utashi wa kisiasa wa kuendelea kubaki katika Muungano. Kama Muungano ungevunjika kutokana na njama hizo, sababu yake isingekuwa ni muundo wa Serikali mbili, bali ingekuwa ni kutokuwapo kwa utashi wa kisiasa kwa upande wa Rais Karume wa kuendelea kubaki ndani ya Muungano.

Kwa hiyo, kwa kweli, kinga madhubuti dhidi ya kuvunjika kwa Muungano, ni kuwapo kwa utashi wa kisiasa kwa viongozi wakuu wanaohusika. Ndiyo sababu Ibara ya 46B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inawataka Viongozi wetu Wakuu, kila mmoja wao kula kiapo maalum cha "kutetea, kulinda na kuimarisha umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." Viongozi wanaohusika ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Zanzibar na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano.

Kwa maneno mengine, Viongozi wetu Wakuu wa pande zote mbili za Muungano wanabanwa na Katiba, pamoja na kiapo hicho walichokula, wasiache kuwa na utashi wa kisiasa wa kulinda Muungano huu usivunjike.

**6.7 Hasira za wanasiasa zinaweza kuvunja Muungano**

Nimekwishakueleza jinsi tukio la Zanzibar kujiunga ana OIC lilivyoleta mzozo. Basi mzozo huo ndio uliozaa kitita cha hasira zilizosababisha Bunge kupitisha

> Wahenga walisema: "Hasira Hasara." Ni dhahiri kwamba Azimio hilo la Bunge lilisukumwa na hasira. Ndiyo sababu Mwalimu Nyerere akaonya kwamba, "Mkiunda Serikali ya Tanganyika kwa msukumo huu (wa hasira), Muungano utavunjika."

Azimio la kudai kuwapo kwa Serikali ya Tanganyika. Aidha, hasira hizo za wabunge ndizo zilizosababisha kutolewa kwa kauli nzito kutoka kwa Mwalimu Nyerere, aliposema kwamba, "Mkiunda Serikali ya Tanganyika kwa msukumo huu, Muungano utavunjika." Mchakato wa ndani ya Bunge ulikuwa hivi:

Hoja ya kwamba, Zanzibar imevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa kujiunga na OIC iliwasilishwa Bungeni na Kamati ya Katiba na Sheria. Mjadala juu ya Hoja hiyo ulijikita katika kuhoji na kulaumu kitendo hicho cha Serikali ya Zanzibar cha kuvunja katiba. Majibu ya Rais wa Zanzibar Dkt Salmin Amour kwa lawama hizo dhidi ya Serikali yake, yalikuwa ni kwamba, "Wanatingisha kiberiti, watagundua kuwa kimejaa."

Kauli hiyo ilizua hasira kubwa miongoni mwa Wabunge wa Tanzania Bara, na hapo ndipo kundi la wabunge lililojulikana kwa jina la G55 lilipoundwa kwa ajili ya kuandaa hoja ya kutaka Serikali ya Tanganyika irejeshwe, wakidai kwamba Serikali ya Tanganyika itakuwa ni "Kiberiti kingine kilichojaa;" sawa na Kiberiti cha Zanzibar.

Wahenga walisema: "Hasira Hasara." Ni dhahiri kwamba Azimio hilo la Bunge lilisukumwa na hasira. Ndiyo sababu Mwalimu Nyerere akaonya kwamba, "Mkiunda Serikali ya Tanganyika kwa msukumo huu (wa hasira), Muungano utavunjika."

**6.8 Muungano ulivyowaokoa washtakiwa Wazanzibari**

Kuna kesi mbili ambazo zinaonesha jinsi washtakiwa wenye asili ya Zanzibar walivyoweza kuokolewa na hali ya Zanzibar kuwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano.

Kesi ya kwanza ilimhusu mtu mmoja mwenye jina la Sheikh Mohammad Nassor Abdulla. Mnamo mwaka 1983, Bwana huyu alikuwa ni mzaliwa wa Makunduchi, na alikuwa ni mtumishi wa Umma. Alipostaafu kazi, aliamua kuishi Mabibo, Dar es Salaam, ambako alikuwa amejenga nyumba yake akitumia haki yake ya uraia wa Tanzania. Tarehe 9 Oktoba 1983, Sheikh Abdullah alipewa amri ya uhamisho (deportation order) iliyosainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano, ya kumhamisha kwa nguvu kutoka Dar es Salaam na kurejeshwa Zanzibar, baada ya kuonekana kuwa vitendo vyake vilikuwa vinahatarisha usalama wa mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa jirani. Mawakili wake walikwenda Mahakama Kuu kupinga amri hiyo.

Uamuzi wa Mahakama ulitolewa kwamba, (tafsiri yangu kutoka kiingereza):

- "Sheria iliyotumika katika kutoa Amri hiyo inampa Rais madaraka ya kuhamisha mtu kwa nguvu kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine ya nchi. Lakini, neno "nchi" limeandikwa kwa kiingereza kuwa ni "Territory", na neno hilo "Territory' limetamkwa na sheria kuwa ni "Tanganyika Territory." Ndiyo kusema kwamba, kwa tafsiri ya kisheria, sheria ya deportation inampa Rais madaraka ya kuhamisha mtu kutoka sehemu moja ya Tanganyika Territory kwenda sehemu yake nyingine. Haimpi madaraka ya kumhamishia Zanzibar. Kwahiyo amri iliyotolewa na Rais haikuwa halali. Mshtakiwa hawezi kuhamishwa."

Uamuzi huo wa Mahakama ulimuokoa Sheikh Abdullah.

Kesi ya pili ilikuwa ni kesi nzito ya uhaini. Kwa kutumia sheria za Zanzibar, Wazanzibari 18 walishtakiwa Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa kosa la uhaini, yaani, jaribio la kutaka kupindua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mahakama Kuu ya Zanzibar, iliwatia hatiani. Washtakiwa walikata rufaa kwa Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Uamuzi wa Mahakama ya Rufani ulikuwa kama ifuatavyo (tafsiri yangu kutoka Kiingereza):

- "Kwa mujibu wa Ibara ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, "Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano." Maana yake ni kwamba, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano. Kosa la uhaini linahusu jaribio la kupindua Serikali ya nchi husika. Kwa kuwa nchi inayohusika hapa ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kosa la uhaini linaweza tu kutendekea dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano."

Hali hiyo ya Zanzibar kuwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano ndiyo iliyowaokoa washtakiwa hao.

**SURA YA 7 MUUNDO WA SERIKALI MBILI NI SERA YA CHAMA CHA MAPINDUZI**

7.1 Sera ya Chama Cha Mapinduzi ni ya Serikali mbili

Tofauti na sera zingine za chama hiki, Sera ya 'Serikali mbili' iliridhiwa na wanachama wote wa CCM. Katika utaratibu wa kawaida wa Chama hiki, sera zake zote hupitishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama hicho, na ikibidi, kuridhiwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

Lakini, kutokana na juhudi zilivyokuwa kubwa za kudai serikali tatu, ilifika mahali ambapo ilibidi wanachama wote wa CCM waulizwe kama wanataka sera hiyo iendelee, au ibadilishwe.

Hatua hiyo ilifikiwa mwaka 1993, baada ya Bunge la Muungano kupitisha Azimio la kutaka iundwe Serikali ya Tanganyika, jambo ambalo lingebadilisha muundo wa Muungano kuwa ni wa Serikali tatu. Azimio hilo lilitokana na Hoja Binafsi iliyowasilishwa Bungeni na kundi la Wabunge lililojulikana kwa jina la G55. Wakati huo Bunge lilikuwa bado ni la Chama kimoja, kwahiyo wabunge wote walikuwa ni wanachama wa CCM.

Ni dhahiri kuwa, Azimio hilo lilipingana moja kwa moja na sera ya CCM ya Serikali mbili. Kwahiyo, ilibidi Chama Cha Mapinduzi kifanye uamuzi wa nini kifanyike katika hali hiyo, ambayo kwa hakika ilikuwa ni ngumu sana kwake.

7.2 Chama Cha Mapinduzi kilivyohangaishwa na Azimio hilo

Hali hiyo ilikuwa ngumu sana, kwa sababu ilitishia kutokea kwa mgogoro wa kikatiba, ambao ungetokea kwa sababu mbili zifuatazo:

Kwanza, Katiba inatambua kwamba, Wabunge ni wawakilishi wa wananchi wote, yaani wale ambao ni wanachama wa Chama Cha Mapinduzi, pamoja na wale wasiokuwa wanachama wa Chama hicho. Kwahiyo, maamuzi wanayoyafanya ndani ya Bunge, huchukuliwa kwamba, wanayafanya kwa niaba ya wananchi wanaowawakilisha. Pili, maamuzi ya Bunge ni lazima yatekelezwe na Serikali. Kwa Serikali kutokufanya hivyo pia kunazaa mgogoro wa kikatiba. Kwa kutambua hivyo, isingekuwa ni busara kwa Chama Tawala kulipuuza tu Azimio hilo, kana kwamba halikuwa na madhara yoyote. Kwa hiyo, (kwa mashinikizo mazito kutoka kwa Mwalimu Nyerere), Chama kilichukua mfululizo wa hatua zifuatazo:

**ITAENDELEA WIKI IJAYO**



Maandamano jijini Kinshasa mbele ya ofisi ya Rais Felix Tshisekedi yakishinikiza ahadi ya kuimarisha usalama Mashariki mwa DRC. **PICHA: MTANDAO**

## Waandamana sababu ya ukosefu wa usalama Mashariki ya DRC

MAANDAMANO makubwa yamefanyika jijini Kinshasa mbele ya ofisi ya Rais wa Felix Tshisekedi, kumshinikiza atimize ahadi yake ya kampeni ya kuimarisha usalama Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Hayo ni kufuatia kuuawa kwa watu saba juzi katika eneo hilo la Mashariki, linalotazamwa kama ngome ya uasi.

Changamoto kubwa inayomkabili Tshisekedi tangu alipoingia madarakani ni kutathmini vipi anaweza kuleta amani kwa taifa hilo hususan eneo la Mashariki, ambako kumeshuhudiwa ghasia na umwagikaji damu mkubwa wa raia, na uwepo wa wanamgambo waliojihami wanaotekeleza mashambulizi.

Maelfu ya watu wamelazimika kuyatoroka mapigano na kuyaacha makazi na mali zao. Na hata kwa waliosalia, wanaishi maisha wakihofia usalama wao.

Raia mmoja mwenye umri wa miaka 32, ambaye baba yake aliuawa anaeleza uchungu wa uovu uliowakabili.

"Tumeomba Rais wetu atusaidie… tunateseka huko Beni, kila siku watu wanauawa… tunaandamana kwa sababu ndugu zetu wamekufa, watoto wamebaki yatima," anasema mmoja wa waandamanaji na kuongeza:

"Rais alifika huku akasema atamaliza vita lakini hajafanya kitu…hatutatoka hapa, tutalala hapa siku tatu."

Raia walioandamana walisindikizwa na baadhi ya Wabunge waliochaguliwa wa kutoka eneo la Beni huko Mashariki mwa nchi.

Wabunge hao wanasema, kuna ripoti ambayo waliwaandikia viongozi wa nchi kuhusu hali hiyo lakini mpaka sasa ripoti hizo 'zinafichwa ndani ya kabati ofisini.'

"Wabunge wa muhula uliopita walifika Beni kuangalia nini kinachosabisha vita huko… waliandika ripoti yao na kueleza wazi nini kinachopatikana huko lakini hadi sasa swali hilo halijazungumziwa katika Bunge… ripoti imefichwa," anasema mbunge Katembo Mbusa na kuongeza:

"Watu wamepeleka habari za uongo ya kwamba ni raia wenyewe ndio wanauana, ni uongo."

Ripoti iliyotolewa Agosti 14 na Shirika la Haki za Binadamu la Human Rights Watch inasema kwamba watu 1900 waliuawa na wengine 3300 walitekwa nyara na vikundi vya watu walio na silaha katikati ya Juni 2017 na Juni 2019.

Zaidi ya makundi 130 yaliyojihami yanapigana kwa sababu tofauti katika majimbo ya Mashariki ya Kivu na kulifanya eneo hilo kuwa "mojawapo ya maeneo hatari zaidi duniani," anasema Lewis Mudge, Mkurugenzi wa Afrika ya Kati kutoka Human Rights Watch na kuongeza:

"Kuelewa nani anayetekeleza uhalifu huu ni hatua ya kwanza ya kuwawajibisha waliohusika na kusitisha uhalifu huo."

**BBC**

UCHAMBUZI

# Boris Johnson ajiandaa kuliburuza Bunge kuhusu Brexit Uingereza

**Na Ani Jozeni**

BAADA ya mtangaza nia, Boris Johnson kushinda nafasi ya uwaziri mkuu kwa sera ya Uingereza kujitoa Umoja wa Ulaya (EU) hata bila makubaliano, mvutano mkali kuhusu agenda hiyo unatazamiwa kufumuka bungeni wakati kipindi cha mapumziko cha joto kali kinapoisha na Bunge kuanza kazi mwezi Septemba.

Tayari kiongozi wa chama cha upinzani cha Labour, Jeremy Corbin, ameshaweka mikakati ya kupigwa kura ya maoni bungeni ya kutokuwa na imani na waziri mkuu atakapofikisha bungeni mpango wake huo.

Uingereza ina muda hadi Oktoba 31 kuondoka EU endapo Bunge halitaridhia mkataba uliofikiwa na Waziri Mkuu Theresa May aliyejiuzulu na Michel Barnier, Kamishna wa Ulaya.

Wachunguzi wa habari nchini Uingereza bado wanaangalia nini hasa kinaweza kutokea katika mpangilio huo wa sera, kwani Bunge la Uingereza liliwahi kukataa kwa wingi wa kura pendekezo la kujitoa bila mkataba, kutokana na kuhofia athari zake.

Ila Bunge halikufaulu pia kupitisha mkataba ulioridhiwa na hata ulipoboreshwa kwa kiwango kidogo, kutilia maanani zaidi shauku za wabunge Uingereza, bila kuvuruga kanuni endelevu za uanachama katika umoja huo, au za kujitoa.

Endapo idadi ya wabunge wanaokataa sera ya kujitoa bila mkataba itabaki pale pale ina maana Waziri Mkuu Johnson atajiuzulu.

Johnson ambaye amekuwa Meya wa jiji la London na baadaye Waziri wa Mambo ya Nje, alijiuzulu kutoka serikali ya May alipoona wajumbe wa Uingereza wanaanza kukubaliana na masharti ya kujitoa ambayo wahafidhina wa dhati katika chama tawala wanaona ni hasimu kwa maslahi ya Uingereza.

Na kwa vile EU haiko tayari kujadili kipengele chochote cha mkataba ulioko mezani, ina maana kuwa Johnson hawezi kusimamia utekelezaji wake hata kama Bunge lingefikia uamuzi wa kuuridhia, jambo ambalo pia halitazamiwi.

Ina maana Johnson atakuwa madarakani kusimamia uharibifu endapo Uingereza itasukumwa 'dirishani' kutoka EU Oktoba 31, dalili za kuyumba uchumi zikizagaa.

Wachunguzi wa habari wanasema moja ya mbinu za kuzuia mkakati wa kujitoa bila mkataba ni wabunge kutawala mchakato wa kujitoa, jambo ambalo si rahisi kuelewa kuwa litafanyika vipi kwani siyo Uingereza inayoamua kitakachotokea bali Umoja wa Ulaya ulishaamua.

Na ndiyo msimamo wa Johnson tangu aingie ofisini mapema mwezi huu, kuwa Uingereza inatoka EU hapo Oktoba 31 'liwalo liwe,' bila tahadhari yoyote maalum ila hatua za kibajeti zitakazotokana na hali itakayojitokeza.

Johnson bado anatetea kwa ncha ya mdomo umuhimu wa mkataba wa kujitoa Ulaya, akisema ni jambo jema kwa maslahi ya Uingereza na Ulaya kwa pamoja, lakini anataka uwe mkataba unaokubaliwa na wahafidhina nchini humo, jambo ambalo haliwezekani kimsingi.

Msimamo kuwa Johnson hapendi kujitoa bila mkataba umezusha hisia kuwa anaweza kujaribu kufikia mkataba mwingine, pendekezo ambalo halijadiliki EU, lakini wakinzani wa kujitoa bila mkataba wanakazania asimamie hapo, wakitazamia kuwa itabidi aache sera hiyo.

Ina maana Uingereza itajisukuma tu, au wabunge wa chama cha Conservative wakubali mkataba uliooreshwa wakati wa May, kukwepa kuchupa Oktoba 31.

Takwimu za hisia za wapigakura hazimpi Johnson raha akiangalia jinsi ya kuchupa kutoka Umoja wa Ulaya ifikapo Oktoba 31 kwani kura za maoni zinaonyesha kuwa sehemu kubwa ya Waingereza wanapinga sera hiyo.

Suala linaloangaliwa kisiasa ni kama Johnson akiamua kuitisha uchaguzi mkuu mpya kuwezesha Brexit ikamilike kwa kuafikiwa na Bunge, atafanikiwa. Anaweza kupoteza viti zaidi.

Ndivyo ilivyokuwa wakati Theresa May alipoingia madarakani baada ya kuunga mkono Uingereza kujitoa EU katika kura ya maoni kitaifa mwaka 2016, halafu akaitisha uchaguzi mpya wa Bunge kupata upana zaidi wa kutekeleza mpango huo.

Hakufanikiwa pamoja na Conservatives kubaki chama tawala kwa wingi wa viti bungeni, vilipungua na kuzuia kufikiwa kwa mkataba wa kujitoa EU kwani wengi wa wabunge hao hawapendi matakwa ya EU katika mkakati wa kujitoa.

Sasa kama wapigakura hawataki mpango wa kujitoa bila mkataba, wanaweza wakawaondoa Conservatives madarakani endapo Johnson ataitisha uchaguzi wa Bunge kwa haraka au kwa pupa kufanikisha mkakati huo.

Mkanganyiko mkubwa zaidi katika suala hilo unaonekana upande wa wabunge wa chama tawala, kwani ni hivi karibuni tu wameshiriki mchakato wa mwezi mzima kupata kiongozi mpya baada ya kujiuzulu May, huku msimamo wake katika suala la Brexit unajulikana bayana, na aliutetea kwa nguvu, na kwa staha aliyomudu.

Kushindwa kutetea msimamo huo pale Waziri Mkuu Johnson atakapoufikisha mbele ya Bunge itakuwa kichekesho, kwani itaonekana wanachama wa Conservatives na makundi ya wabunge waliojiunga na watangaza nia na kuwapigia kampeni walikuwa wanachagua sura. Hawazijui sera zao.

Wachunguzi wa habari wanakiri kuwa mawaziri wanapoteza usingizi wakifikiria watakavyomudu kutetea kuchupa kutoka Umoja wa Ulaya, kwa athari zinazohofiwa za hatua hiyo, hasa kupungua kwa mauzo ya bidhaa za viwanda na kilimo nchi za Ulaya wakati ushuru wa forodha ukipanda kwa nguvu.

Hata hivyo, wanakiri siyo rahisi kupata mbadala wa kukamilisha mkakati huo, licha ya kuwa soko la fedha la London linaonyesha kuwa sarafu ya nchi hiyo, sterling, tayari inaugua 'homa ya Brexit' kwani wafanyabiashara na wenye viwanda kwa jumla hawataki mpango wa kujitoa Ulaya bila mkataba.



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson. **PICHA: MTANDAO**

Aliyeonekana kufurahia mpango huo ni Rais Donald Trump wa Marekani akimpigia chapuo Johnson kumrithi May uwaziri mkuu.

Kwa vile suala la kumwondoa Johnson madarakani kuzuia kuchupa kutoka Umoja wa Ulaya halipo mezani kwani siyo mazingira mapya katika kukubaliwa kwake kama ilivyokuwa kwa May, ambaye aliahidi kupata mkataba na siyo kujitoa kwa mkanganyiko, ina maana kuwa Uingereza itachupa Oktoba 31.

Milango imefungwa EU kutafuta mkataba mwingine, na hakuna uwezekano wabunge wa Conservative wamtose Johnson bungeni, waafikiane na wale wa Labor na wazalendo wa Scotland kukataa kujitoa Ulaya bila mkataba.

Ni utii kwa Johnson utakaohakikisha kuwa Uingereza inatoka Ulaya Oktoba 31 kama inavyotarajiwa, kwani wabunge hawana mbadala kwa nafasi hiyo na wapigakura bado hawakiamini chama cha Labor, au kiongozi wake bungeni Jeremy Corbyn, kutoa uongozi stahiki kwa taifa hilo kwa sasa.

Anashukiwa kuwa mmojawapo kati ya wanaopiga vijembe Wayahudi kila kukicha.

Kunyaukanyauka kwa sarafu ya Uingereza kunaleta mashaka kiasi fulani lakini wapo baadhi ya wataalamu wanaona kuwa ni suala la mpito.

Kwa upande mwingine itategemea hatua za kibajeti ambazo serikali ya Johnson itachukua pindi kujitoa kukikamilika au suala hilo kuondolewa bungeni kuwa siyo la mjadala tena ila la kutekelezwa. Mojawapo kati ya hatua hizo ni kupunguza kodi kwa bidhaa kutoka barani Ulaya zinazoingia Uingereza badala ya kupandisha kodi kutokana na kujitoa, hivyo kuwezesha EU nayo ipunguze viwango vya ushuru wa forodha kwa bidhaa za Uingereza, zisifanane na nchi nyinginezo zisizo na makubaliano kama hayo.

Kilichoshindikana hata hivyo ni umoja wa forodha.

Baadhi ya wanaounga mkono kujitoa Umoja wa Ulaya walikuwa wanadhani Uingereza inaweza kupanua biashara na China, pamoja na nchi nyingine.

Ila matukio ya hivi karibuni kama vurugu zinazoendelea jiji la Hong Kong ambako kuna mvutano kati ya China na Uingereza, pamoja na vikwazo vilivyowekwa dhidi ya kampuni ya Huawei na utawala wa Trump, vinafanya uwezekano huo kuwa finyu.

Nyenzo za kawaida za kupunguza kodi, hata kuboresha miundombinu, kulegeleza mikopo ya benki, itafanikiwa.

UCHAMBUZI

# Kuchauka na utumishi wake Jimbo la Liwale

- Afurahia mawasiliano ya simu Liwale
- Aahidi msukumo zaidi kulipaisha Jimbo hilo



Mbunge wa Liwale, Zuberi Kuchauka, akiwa katika moja ya mikutano alipokuwa akiwania ubunge.**PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

LIWALE ni moja ya majimbo ya Mkoa wa Lindi, ambalo kwa muda mrefu limekuwa nyuma kwa mawasiliano ya simu, hali ambayo inasababisha usumbufu kwa wakazi wake wanapohitaji kupata huduma hiyo.

Hali hiyo inaweza kuwa inakwamisha ukuaji na uendelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo zikiwamo za biashara, kutokana na ukweli kwamba mawasiliano yana mchango mkubwa katika suala zima la maendeleo.

Kutokana na ukuaji wa teknolojia matumizi ya simu za mkononi na mtandao wa intaneti, vimekuwa ni msaada mkubwa kwa ajili ya kuwafikia wateja wengi na wadau mbalimbali wa biashara kwa muda mfupi.

Matumizi sahihi ya teknolojia ya mawasiliano yanasaidia ufanisi wa biashara.

Kwa kutambua hilo, mbunge wa jimbo hilo, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Zuberi Kuchauka, anasema amejitahidi kuweka msukumo wa kusaidia Liwale kuwa na mawasiliano ya simu ili kurahisisha mawasiliano.

Mbunge huyo anasema hayo katika mahojiano na gazeti hili akielezea pia shughuli nyingine za maendeleo zinazofanyika kwa sasa jimboni mwake.

**SWALI:** Mawasiliano ya simu yakoje kwa sasa na awali yalikuaje?

**JIBU:** Kwa muda mrefu mawasiliano ya simu Liwale kwa ujumla yalikuwa ni duni kwani yalipatikana sehemu chache na hasa mjini na maeneo ya jirani. Lakini ndani ya kama mwaka mmoja tangu nichaguliwe kuwa mbunge, nimeweka msukumo na kushawishi kampuni za simu na sasa yanapatikana kwenye kata tisa kati ya 20. Na ninaweza kusema kwamba kwa sasa mawasiliano ya simu kwa Liwale ni asilimia 70. Jukumu langu kama mbunge ni kuweka msukumo kwenye mamlaka husika na kushirikiana na viongozi wa serikali kuhamasisha maendeleo ili kuhakikisha Liwale inasonge mbele na ndivyo nimekuwa nikifanya.

**SWALI:** Umesema kwa sasa mawasiliano ya simu yanapatikana hadi kufikia kata tisa, ni zipi hizo?

**JIBU:** Kwanza kabisa kama nilivyosema awali, mawasiliano yalikuwa yakipatikana Liwale mjini na maeneo ya jirani, lakini sasa yamefika hadi kwenye kata za Mpigamiti, Ngongowele, Mirui, Mlembwe, Kibutuka, Lilombe, Kimambi, Liwale Mjini na Liwale B, yaani kwa sasa raha tupu, watu hawapati shida kwenye mawasiliano kama ilivyokuwa zamani na bado ninaendelea kushirikiana na viongozi wa serikali nikitia msukumo ili kuhakikisha kata zote zinakuwa na mawasiliano. Kumbuka kwamba ukuaji wa teknolojia ya matumizi ya simu za mkononi yamekuwa ni makubwa siyo mjini wala vijijini na yanasaidia kuwaunganisha wakulima, wafanyabiashara na watu wa kada mbalimbali. Hivyo nasi Liwale hatuna budi kuunganishwa na wengine kwa njia ya mawasiliano ya simu.

**SWALI:** Mbali na mawasiliano ya simu, kipi kingine kinaendelea jimboni mwako?

**JIBU:** Kingine kinachoendelea ni upembuzi yakinifu kwenye barabara ya Liwale hadi Nachingwea ili baadaye iwekewe lami na kuunganisha mawasiliano kati ya maeneo hayo na mengine ya mkoa wa jirani wa Mtwara. Hatua ya kuwekea lami barabara hiyo yenye zaidi ya kilometa 100, itaondoa pia usumbufu ambao abiria na madereva wamekuwa wakiupata wakati wa mvua. Mkuu wetu wa wilaya, Sarah Chiwamba, amewahi kuomba kwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa, kuwa wananchi wake wanaamini kwamba Liwale itafunguka kibiashara na kiuchumi iwapo itaimarishwa katika mtandao wa barabara hiyo inayounganishwa na Nachingwea. Ninafurahi ninapoona mchakato umeanza na ninakuwa na uhakika kwamba mawasiliano kwa njia ya barabara Liwale sasa yanaelekea pazuri ili kurahisisha usafiri. Kimsingi ni kwamba ninajivunia mambo mengi tu ya maendeleo, ambayo niliahidi na kuyawekea msukumo

> Kumbuka kwamba ukuaji wa teknolojia ya matumizi ya simu za mkononi yamekuwa ni makubwa siyo mjini wala vijijini na yanasaidia kuwaunganisha wakulima, wafanyabiashara na watu wa kada mbalimbali. Hivyo nasi Liwale hatuna budi kuunganishwa na wengine kwa njia ya mawasiliano ya simu.

na sasa yameanza kuonekana tangu niwe mbunge. Nina uhakika yataendelea kufanyika mengi zaidi ili mradi Mungu aendelee kutujalia uhai.

**SWALI:** Kwa upande wa hali ya afya ikoje Liwale?

**JIBU:** Tunatengeneza Liwale ya kisasa, hivyo ni muhimu kuwa na vitu vya kisasa. Kwa upande wa afya ni kwamba tayari serikali inajenga hospitali mpya ya wilaya itakayokuwa ya kisasa zaidi. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 hadi 2020. Siyo kwamba hatuna hospitali ya wilaya, ipo, lakini inajengwa nyingine mpya, kwani iliyopo ilijengwa tangu Liwale inaanzishwa mwazoni mwa miaka ya 1970. Juhudi hizi na nyingine nyingi zinazoendelea ni wazi kwamba miaka michache ijayo Liwale itakuwa miongoni mwa majimbo ambayo yako juu zaidi kuliko ilivyo sasa. Jambo la msingi ni kuendelea kujipanga na kutekeleza kwa kuzingatia kaulimbiu ya 'Hapa Kazi Tu'. Hatutaki kuwa nyuma kimaendeleo na ninaamini kwa kasi ya serikali ya awamu ya tano tutafika mbali, kwani dalili zimeanza kuonekana kwenye mawasiliano.

**SWALI:** Awali ulikuwa mbunge kupitia Chama cha CUF, ulishindwaje kuweka msukumo wakati huo?

**JIBU:** Ilikuwa ni vigumu kuwatumikia wananchi kikamilifu huku chama kina mgogoro ambao kwa kweli ulinipa wakati mgumu wa kufanya shughuli zangu kama mbunge. Nikaamua kurejea CCM kwa sababu nina uhakika kufanya kazi bila changamoto kama hizo ambazo nilikumbana nazo na nilifanya utafiti wa kutosha na kubaini kuwa CCM ya Rais John Magufuli imerejea kwenye misingi ya TANU, na mimi kama mwananchi mpenda maendeleo sikuona kigugumizi kurejea. Sikuwa na sababu ya kupoteza muda kwani nilichaguliwa na wananchi kuwatumikia siyo kushiriki kwenye migogoro. Ninaowamba wananchi wa Liwale waendelee kuniunga mkono katika harakati hizi za kuibadili Liwale.

# India yapimana nguvu na Pakistan

• Yafuta utawala wa ndani Kashmir upande wa India

**Na Ani Jozeni**

WIZARA za Mambo ya Nchi za Nje maeneo mengi duniani wameanza kuweka mikakati ya dharura ya jinsi ya nini cha kufanya endapo mzozo kati ya India na Pakistan ulioanza kufukuta kwa nguvu kufuatia kuondolewa utawala wa ndani eneo la Kashmir iliyo chini ya India ukipanuka.

Ndicho kinachohofiwa baada ya Waziri Mkuu Narendra Modi kutangaza hatua hiyo akisema imelenga kuwawezesha wananchi katika eneo hilo wawe na haki sawa na wengine nchini India, na waweze kuondokana na ugaidi. Ni eneo ambako makundi ya jihad yana nguvu.

Bodi ya gazeti la Los Angeles Times ilichapisha tahariri maalum ya kueleza wasiwasi wa kina kuhusu hali hiyo, ikisema kuwa ukamataji wa madaraka uliofanya na India eneo la Kashmir, unaweka eneo hilo ambalo lina viashiria vya uasi na vita katika hali mbaya zaidi.

Eneo la Kashmir linafanana na lile la Wakurdi, ambako nchi kadhaa zinagawana eneo ambalo lina dhamira ya kuwa nchi huru, lakini haliwezi kujitenga na nchi hizo.

Kwa upande wa Kashmir imegawanyika kati ya India, Pakistan na China, lakini ni India na Pakistan zinazotishana hapo.

Baadhi ya wachunguzi wa habari wanadhani kuwa sababu halisi ya kuondoa utawala wa ndani jimbo la Kashmir ni kuruhusu kampuni kubwa za India pamoja na wanunuzi binafsi kuchota amana zinazopatikana katika eneo hilo.

Kifungu cha 370 cha Katiba ya India kinachotoa mamlaka ya ndani kwa Kashmir pia kinakataza wageni kumiliki mali isiyohamishika katika eneo hilo, hali ambayo imezuia fedha na mitaji nchini India kuingia eneo hilo na kuwekezwa, hivyo kulibakiza nyuma katika maendeleo.

Isitoshe, muda unavyozidi kwenda, kujitenga kunashamiri.

Kuna wadadisi wanaoshangaa kwanini Waziri Mkuu Modi amengoja hadi aingie muhula wa pili ili achukue hatua hiyo, kwani haiwezekani kuwa ni jambo lililofanyiwa uamuzi wa kushtukiza.

Cha kushangaza ni kuwa China imejiunga na Pakistan katika kulaumu hatua hiyo, wakati hakuna jimbo China lenye uwezo wa kujiamulia ambako raia wengine wa China hawaruhusiwi kuwa na mali.

Hata hivyo, kwa miaka mingi China na Pakistan zimekuwa na mahusiano mazuri, licha ya kuwa Marekani imekuwa na mahusiano ya karibu ya kijeshi na Pakistan, ila sasa yanasuasua.

Inawezekana hapa kuna mwanya uliotokeza kwa India kuingilia kwa nguvu zaidi kuhusu hali ya Kashmir, kwani uhusiano wa India na Marekani ni bora zaidi kuliko Pakistan na Marekani, wakati uhusiano wa Pakistan na China hautakuwa na nguvu katika suala hili.

China inajaribu kila iwezalo kukwepa kuwekewa vikwazo vingine na Marekani, hivyo haitazamiwi kununua ugomvi huo kwa kujitolea mno, wakati ambapo yenyewe haitaki suala la Kashmir kuendelea kutajwa kwa nguvu.

Ingekuwa ikipata shida katika jimbo la Xinjiang kutokana na harakati ya Kiislamu eneo hilo, hivyo China ikiiunga mkono Pakistan inaelekea itakuwa ni kidiplomasia tu, si zaidi.

Isitoshe hisia za kizalendo nchini India zimekuwa zikipanda kwa kasi kipindi hiki cha Waziri Mkuu Modi, na inatumia mwanya wa matatizo kibao nchini Pakistan hasa migawanyiko katika tabaka tawala; kiongozi wa kihafidhina wa siku nyingi, Nawaz Sharif aliondolewa, akashtakiwa.

Tahariri ya Los Angeles Times ilifananisha hatua zilizochukuliwa na serikali ya India na zile za utawala wa China kuhusu Hong Kong, kuwa ni kuzuia uhuru uliopo na kuvamia kuingiza sheria nyingine.

Kulikuwa na wasiwasi pia kuhusu hali itakavyokwenda kama vita ikizuka kati ya India na Pakistan, kwani nchi hizo mbili zina silaha za nyuklia, ila baadhi ya wachunguzi wa mahusiano ya kimataifa hawatazamii kuwa Pakistan itafikisha suala hilo katika ngazi ya vita.

Ingekuwa ni nchi inayotawaliwa kidini moja kwa moja hiyo ingewezekana ila Pakistan siyo serikali ya kidini.

Moja ya mabadiliko makubwa yanayotazamiwa baada ya hatua zilizochukuliwa na Waziri Mkuu Modi ni kuwa watu wa dini ya walio wengi nchini India, Wahindu, watahamia kwa wingi katika eneo hilo na kununua makazi.

Hiyo itamaliza wingi wa wafuasi wa dini ya Kiislamu unaolipatia jimbo la Kashmir hadhi ya utawala maalum, kana kwamba ni nusu Pakistan na nusu India.

Tofauti na Wakurdi ambao angalau wana hisia ya utaifa wa pamoja, suala la Kashmir ni la mpaka wa Pakistan na India na siyo India na Kashmir, hivyo halina uwezo wa kuzua uzalendo wa ki-Kashmir.

Ni mwendelezo tu wa mvutano kati ya nchi hizo mbili, na kimsingi hauna tiba.

Tofauti ipo katika mazingira ya kiuchumi na kisiasa kuwa India sasa iko katika mwinuko wa kiuchumi na kidiplomasia, ikiwa na umoja wa kitaifa wa kiwango kikubwa zaidi kuliko miaka ya nyuma.

Wakati Modi anashinda uchaguzi na kuingia muhula wa pili, wachunguzi wa habari na wafuatiliaji uchumi kama shirika la habari la Bloomberg walisema kuwa ushindi mkubwa wa Modi katika uchaguzi mwezi Mei umebadili hali ya siasa nchini humo.

Mirji Sharma, akiandika kutoka India kwa shirika hilo alisema "Hii sasa ni India ya Modi. Uchaguzi huu ulipiganiwa kuhusu kujitambua kuwa Mhindi, kujitambua kama nchi na kujitambua kwa wananchi wake."

Kwa hisia hizo, kuweka mkazo kuwa Kashmir upande wa India ni India tu na siyo nusu Pakistan ni hatua inayofanana na uamuzi wa Rais Donald Trump kutambua Yerusalemu kama mji mkuu wa Israel, kuwa ni jiji la Israel na siyo nusu Israel na nusu Palestina.

Na kama ilivyo kwa suala la Yerusalemu, wakinzani wa uamuzi huo watapiga kelele na kufanya maandamano lakini viashiria vya uelekeo wa uchumi viko upande wa wahafidhina, iwe ni suala la Yerusalemu au Kashmir.

Licha ya serikali ya Waziri Mkuu Imra Khan kuungwa mkono na jeshi la nchi hiyo na makundi ya kihafidhina, ina uelekeo wa kimaendeleo na zaidi amani, hata kama bado inatetea uzalendo.

Taarifa za hivi karibuni kuwa Shahbaz Sharif, mtu wa karibu wa Nawaz Sharif alitoa hotuba kali bungeni kumsuta Imran Khan ni kielelezo fasaha kuwa tabaka tawala nchini Pakistan halina umoja wa kutosha kuwakusanya watu kwa vita dhidi ya India hivi sasa.

Khan ameishia kufuta safari za treni ambazo zinaunganisha nchi hizo mbili, akitazamia kuisumbua India, lakini katika biashara kuvuruga mahusiano hakuwezi kuumiza upande mmoja tu.

Katika mazingira ya sasa, haitakuwa rahisi kwa Khan kufanya lolote, kuhusu jimbo ambalo Pakistan haitawali tangu 1947.

(



Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi. PICHA: MTANDAO

> Tahariri ya Los Angeles Times ilifananisha hatua zilizochukuliwa na serikali ya India na zile za utawala wa China kuhusu Hong Kong, kuwa ni kuzuia uhuru uliopo na kuvamia kuingiza sheria nyingine.

## Abiria usafiri wa bajaji wapewa onyo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADA ya Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kuendesha operesheni ya kuwashughulikia madereva wa pikipiki za magurudumu matatu maarufu kwa jina la bajaji, sasa limetangaza kuwageukia abiria wanaotumia usafiri huo.

Operesheni inayoendelea sasa ni ya kuwakamata madereva wa vyombo hivyo wanaokiuka sheria kwa kuingilia njia za magari ya abiria (daladala) kwa kuchukua abiria kwenye vituo vya magari hayo hali ambayo inasababisha migogoro miongoni mwa wasafirishaji hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema kwa mujibu wa sheria, bajaji ni chombo cha kukodiwa kama ilivyo kwa teksi, lakini wao wanakiuka kwa kuanza kuchukua abiria kwenye vituo.

Alisema wamefanya opereshani hiyo na kukamata bajaji nyingi na zoezi bado linaendelea mpaka wahakikishe kila mmoja anafanya kazi kwa kuzingatia sheria za usafirishaji ili kuepuka migogoro ambayo huwa inawaumiza wananchi.

Alisema baada ya operesheni hiyo kuzaa matunda wana mpango wa kuwageukia abiria wa vyombo hivyo ambao wanawasababishia madereva kuonekana wanavunja sheria.

Alisema kwa mujibu wa taratibu, bajaji inatakiwa isibebe abiria zaidi ya watatu na hivyo wataanza kuwakamata abiria watakaoonekana kuwa wamezidi kwenye vyombo hivyo na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

"Mtu anayetaka kupanda bajaji akikuta ndani ya bajaji hiyo kuna abiria watatu hatakiwi kupanda," alisema Kamanda Matei.

Alisema wataendelea kutoa elimu ya usalama barabarani ili kupunguza makosa ya barabarani ambayo wakati mwingine yanagharimu maisha ya watu.

Mwezi Machi mwaka huu, madereva wa daladala jijini Mbeya waligoma kufanya kazi kwa siku mbili mfululizo wakidai kuwa wanaingiliwa kwenye njia zao na watu wa bajaji hali inayowafanya wasipate faida, Serikali ya Wilaya ya Mbeya iliingilia kati na kuyaita makundi yote mawili kisha kumaliza mgogoro.

# Wakulima washauriwa kupima udongo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wameshauriwa kupima afya ya udogo kabla ya kupanda ili waongeze tija kwenye uzalishaji kwa kupanda mazao yanayoendana na virutubisho vilivyomo kwenye udongo huo.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mazao nchini (Tari), Kituo cha Uyole kilichopo jijini Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa anazungumza na Nipashe kwenye maabara ya kupima udongo iliyopo kituoni hapo.

Alisema kwa sasa mavuno yameanza kushuka katika maeneo mengi ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kutokana na udongo kuchoka kwa kukosa virutubisho muhimu kwa mimea hali ambayo inawafanya wakulima kutumia rasilimali nyingi, lakini bado tija inakuwa ndogo.

Alisema ili kurejesha mavuno katika hali ya awali wakulima wanatakiwa kupeleka sampuli za udongo kutoka kwenye mashamba yao na kwenye maabara ya taasisi hiyo ili wapimiwe na kushauriwa namna ya kurejesha virutubisho vilivyopotea.

**Wakati huu ambao serikali inasisitiza kuingia katika uchumi wa kati ndio wakulima wanatakiwa wazalishe sana, lakini changamoto ni udongo kuchoka kutokana na kulimwa bila kupumzishwa, udongo hauna virutubisho vinavyohitajika na mimea**

Dk. Bucheyeki alisema udongo wa baadhi ya maeneo una kiasi kikubwa cha tindikali na mengine yana chumvi nyingi na hivyo kusababisha mazao kudumaa tofauti na ilivyokuwa awali.

"Wakati huu ambao serikali inasisitiza kuingia katika uchumi wa kati ndio wakulima wanatakiwa wazalishe sana, lakini changamoto ni udongo kuchoka kutokana na kulimwa bila kupumzishwa, udongo hauna virutubisho vinavyohitajika na mimea," alisema.

"Hapa kwetu tuna maabara ya kisasa ambayo ni kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu, wanatakiwa kushirikiana na maofisa kilimo wa maeneo yao kuleta sampuli za udongo wao, ili zipimwe hapa na tuwape ushauri wa kitaalamu," aliongeza.

Alisema endapo wakulima hawatafanya hivyo, watakuwa wanatumia mbegu bora za kilimo, lakini bado mavuno yataendelea kuwa chini kuliko tafiti zinavyoonyesha.

Dk. Bucheyeki aliongeza kuwa ili kupunguza tindikali kwenye udongo, wakulima wanatakiwa kutumia chokaa ambayo kazi yake ni kufyonza tindikali hizo.


Hata hivyo, baadhi ya wananchi waliuomba uongozi wa taasisi hiyo kuwa na utaratibu wa wataalamu wake kuwatembelea moja kwa moja katika maeneo yao kwa madai kuwa hawana uelewa wa kutosha juu ya matumizi ya teknolojia ya kupima udongo.

Mmoja wa wakulima hao, John Mwashitete, ambaye analima maharage katika bonde la Utengule, alisema wakulima wengi hawajui kuwa udongo unatakiwa kupimwa.

Alisema yeye huwa anaenda kwenye taasisi hiyo kwa ajili ya kununua mbegu za mazao mbalimbali, lakini alikuwa hajui kuwa inahusika pia kupima udongo.

"Mimi nimejua kuwa udongo unapimwa kutokana na kuja mara kwa mara kununua mbegu hapa, wataalamu wamekuwa wakiniuliza maswali mengi kuhusu eneo ninalolima na ndipo waliponiuliza kama nimewahi kupima udongo niliposema sijawahi ndipo walinipeleka kwenye maabara na wakanielimisha," alisema Mwashitete.

Alisema ni vizuri wataalamu hao wawe wanawatembelea wakulima kwenye maeneo yao ili kuwapatia elimu na kwa njia hiyo itawasaidia wakulima wengi kupata huduma hiyo.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mazao (Tari) Kituo cha Uyole, jijini Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki (mwenye suti), akiangalia watafiti wa udongo wanavyotumia moja ya mashine za kupimia udongo zilizopo kwenye maabara ya taasisi hiyo, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ukosefu elimu wakosesha mikopo wanawake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wanawake nchini wanashindwa kunufaika na mikopo ya asilimia nne inayotolewa na halmashauri kutokana na kukosa elimu kuhusu mikopo hiyo ambayo ipo kwa mujibu wa sheria za nchi.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Mradi wa Uboreshaji wa Masoko ya Maziwa na Alizeti (Tam), unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo la nchini Uholanzi (SNV) chini ya ufadhili wa Shirika la Msaada la Uingereza (UKaid), Tom Ole Sikar.

Aliyasema hayo wakati wa mkutano wa siku mbili wa kuhamasisha upatikanaji wa mikopo kwa wanawake ulioandaliwa na SNV na kuwashirikisha wasindikaji wa mafuta ya alizeti, maofisa maendeleo ya jamii na wakulima wa alizeti kutoka katika mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Mikoa iliyohusika katika mradi huo ni Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi na kwamba mikopo hiyo ipo kwa mujibu wa sheria, lakini baadhi ya vikundi vya wanawake vinashindwa kunufaika nayo kutokana na elimu ndogo kuhusu namna mikopo hiyo inavyopatikana.

Aliwashauri maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri pamoja na wakurugenzi kushirikiana kutoa elimu ili wakopaji wajue namna ya kupata mikopo hiyo na namna wanavyotakiwa kurejesha.

Kwa upande wao baadhi ya maofisa maendeleo ya jamii kutoka katika mikoa hiyo, walieleza namna ambavyo wanahakikisha mikopo hiyo inapatikana kwa makundi yote matatu ambayo ni kundi la vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Wambi Mwalukisi, alisema mikopo hiyo ipo kwa mujibu wa sheria na halmashauri zinaitoa kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

Alisema katika Halmashauri ya Songwe, vipo vikundi vingi ambavyo vimenufaika na mikopo hiyo tangu ilipoanzishwa na moja kati ya sifa ya kikundi kupata mkopo huo lazima kiwe na shughuli ya kufanya na kiwe na watu wenye sifa.

Alisema awali kulikuwa na changamoto ya baadhi ya vikundi kutorejesha mikopo hiyo, lakini baada ya kuvielimisha mikopo hiyo inarejeshwa.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka katika Halmashauri ya Mpanda mkoani Katavi, Halima Kitumba, alisema baada ya fedha hizo kupatikana wanavitangazia vikundi wakivitaka vianze kuomba.





# Waliosababisha mgomo wa daladala waondolewa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BAADA ya mgomo wa daladala kutikisa Jiji la Dodoma juzi, uongozi wa jiji umewahamisha wafanyabiashara ndogo 165 waliokuwa kwenye kituo cha daladala cha Sabasaba.

Hatua hiyo imechukuliwa kufuatia mgomo wa madereva wa daladala walioshinikiza wamachinga hao waondoke kwa madai kuwa ni chanzo cha ajali sehemu hiyo.

Hatua hiyo ilifikiwa jana baada ya Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, kuagiza Ofisa Masoko kuwahamisha wafanyabiashara hao kwa kuwa wamevamia eneo hilo.

Akituliza mgomo wa madereva hao juzi, Kunambi aliagiza wafanyabiashara hao wakiwamo wa matoroli, wachoma nyama, mahindi na walioko katikati ya kituo hicho kuondoka mara moja ili kupisha magari hayo.

"Najua kila mtu ana haki ya kutumia eneo hili, lakini kuna watu wamevamia mpaka katikati ya daladala, ninawataka kuondoa biashara zenu humu, njooni munione nitawafanyia utaratibu wa kupata maeneo mbadala," alisema Kunambi.

**Tumewahamisha wafanyabiashara wenye meza takribani 165, hakikisheni mnafanya biashara katika maeneo rasmi ambayo yametengwa ili kujiepusha na changamoto ambazo zinaweza kujitokeza kama hizi.**

Aidha, aliagiza kuorodheshwa kwa majina ya wafanyabiashara wote ndani ya kituo hicho ili kupangiwa maeneo mengine ya kufanyia biashara.

Aliyataja maeneo yaliyotengwa na jiji kwa ajili ya wajasiriamali na wafanyabiashara ndogo ndogo kuwa ni soko la Bonanza na Sabasab, hivyo hakuna mfanyabiashara atakayekosa eneo la kufanyia shughuli zake.

Kutokana na maagizo hayo, Ofisa Masoko James Yuna, alisema, jana walitekeleza maagizo ya mkurugenzi ambapo wafanyabiashara hao wamepelekwa soko la Sabasaba na soko la matunda na mboga la Bonanza.

"Tumewahamisha wafanyabiashara wenye meza takribani 165, hakikisheni mnafanya biashara katika maeneo rasmi ambayo yametengwa ili kujiepusha na changamoto ambazo zinaweza kujitokeza kama hizi," alisema.

Ofisa huyo alisema yapo madhara yatokayo na wafanyabiashara kuvamia maeneo ambayo hayajarasimishwa kibiashara na kusababisha ajali na kwamba wamejitahidi kwa kiasi kikubwa kuwaelekeza na kuwarudisha katika eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya biashara za matunda na mboga.

Yuna alisema kazi ya kuwahamisha wameifanya kwa kushirikiana na polisi ili kuhakikisha usalama wa mali zao unakuwapo.

Alisisitiza wafanyabiashara kutambua kuwa wateja ndio wanatakiwa kufuata bidhaa na sio muuzaji kumfuata mteja.

Akizungumzia hatua hiyo, mwenyekiti wa madereva hao, Shukuru Mushi, alishukuru jiji hilo kwa hatua ilizochukua kuwaondoa wafanyabiashara hao kwa kuwa walikuwa wamehodhi eneo kubwa na kuhatarisha usalama wao.

"Kama mnavyojua athari za moto sasa hapa kulikuwa na matumizi holela ya moto kulikuwa na wachoma mishikaki, mahindi, na wote walikuwa wanatumia majiko ya mkaa na gesi. Moto ukitokea hapa tunapata madhara makubwa, ndiyo maana tuliona tugome ili hatua zichukuliwe," alisema Shukuru.



Meneja Masoko wa kampuni ya kutotolesha vifaranga vya kuku ya AKM Glitters Co. Ltd, Dofrian John (kushoto), akizungumza katika mafunzo ya wafugaji kuku na mawakala wa kampuni hiyo, kutoka mikoa ya Kanda ya Kati ambayo ni Dodoma, Singida, Kigoma, Katavi na Tabora, yaliyofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vijana watakiwa kufuga, kulima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIJANA wametakiwa kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa na serikali katika halmashauri mbalimbali hapa nchini, ili iwasaidie kuendesha shughuli za kilimo cha bustani na ufugaji.

Akizungumza na Nipashe kuhusu uboreshaji wa kilimo cha mboga, Mkurugenzi wa Asasi ya Kiraia ya Ijen Agripreneurship Wilfred Ngalaba, alisema vijana wasomi wanapaswa kutumia taaluma zao ikiwamo kuunda vikundi ili kupata mikopo hiyo na kujiinua kiuchumi.

Ngalaba alisema kinachotakiwa ni kuungana pamoja kupanga mikakati ya nini cha kufanya jambo ambalo litawasaidia kubuni miradi itakayoleta tija kwao na wananchi kwa ujumla.

"Naomba vijana tuchangamkie fursa za mikopo ambazo zinatolewa na serikali katika halmashauri hii itatusaidia kutengeneza ajira kupitia miradi tunayobuni kwenye sekta mbalimbali ikiwamo kilimo," alisema Ngalaba.

Alisema hakuna sababu ya kukaa na kusubiri ajira rasmi inachotakiwa ni kuwa wabunifu kupitia taaluma walizopata vyuoni kuanzisha miradi ambayo itatuwezesha kupata kipato cha kila siku.

Alieleza lengo la taasisi hiyo ni kuona vijana wanakuwa mstari wa mbele kupata mikopo hiyo kufanya uwekezaji kwenye kilimo na ufugaji.

Aidha, alisema wanaendelea kutoa elimu ya utunzaji bora wa bustani katika mikoa mbalimbali hapa nchini ambapo tayari wameanza zoezi hilo jijini Dodoma.

Ngalaba alisema hadi sasa wametoa elimu hiyo kwa vikundi vya wajasiriamali jijini Dodoma katika eneo la Ihumwa, ambapo wakulima wengi wa mboga wameanza kunufaika.

# Masuala ya kijinsia yafanyiwe utafiti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IDARA ya Habari Maelezo imewataka wadau wa habari kufanya utafiti wa masuala ya kijinsia katika vyombo vya habari.

Aidha, wanahabari wanawake wametakiwa kujiamini ili waweze kuaminiwa na kupewa nafasi za uongozi ndani ya vyombo hivyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Habari Maelezo, Rodney Thadeus, alipokuwa akifungua mafunzo kwa wanahabari wa mkoa wa Dodoma kuhusu usawa wa kijinsia kwenye vyombo vya habari.

Mafunzo hayo yanatolewa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa) kwa ufadhili wa Taasisi ya Maendeleo na Vyombo vya Habari Finland (Vikes).

Mkurugenzi huyo alisema kwenye vyombo vya habari wanaume ndiyo wengi ukilinganisha na wanawake.

"Tunamaliza kwenye vyuo, lakini tukija 'newsroom' wanaume ndio wengi kuliko wanawake, ni vyema mkajijengea uwezo wa kujiamini ili kuweza kufanya kazi kwenye vyombo vya habari," alisema.

Alisema wanawake wana uwezo mkubwa hivyo wanatakiwa kujiamini na kujifunza zaidi hasa ikizingatiwa kuwa hata malengo ya maendeleo endelevu(SDGs) yanahimiza usawa wa kijinsia.

Sambamba na hilo, mkurugenzi huyo aliwataka kuonyesha uwezo na kazi za kiwango cha juu ili waweze kuaminiwa na kushika nafasi za uongozi.

"Mjijengee kujiamini na kufanya kazi katika ubora unaotakiwa mnaweza kufikia nafasi za juu za uongozi ambazo zinashikwa na wanaume kwenye vyombo vyenu vya habari," alisema Thadeus.

Aidha, aliwasisitiza kusoma na kuongeza maarifa ili kukidhi matakwa ya Sheria ya Huduma kwa Vyombo vya Habari ambayo imeweka kiwango cha elimu angalau stashahada ya uandishi wa habari.

"Pia dunia imebadilika haipo ardhini lazima tujikite kwenye mitandao ya kijamii msibaki kwenye magazeti tu mjikite na huko," alisema Thadeus.

Aliwaasa kutumia mitandao ya kijamii bila kupotosha na kuzingatia maadili.

"Kuna shida sana sasa hivi kwenye masuala ya mitandao ya kijamii na utangazaji, yaani ukisikiliza redio unasema nini hichi matumizi ya lugha ovyo, vichwa vya habari kwenye mitandao ya kijamii vya ajabu, najua ni kwa sababu vinawekwa na wanaume, wanawake mnaweza kubadili hii hali," alisema.

Mkurugenzi wa Tamwa, Rose Reuben, alisema wanawake wanakabiliwa na changamoto nyingi kwenye vyombo vya habari ikilinganishwa na wanaume.

Alisema Taasisi ya Vikes ilitoa ufadhili kuhusu masuala ya kijinsia kwenye vyombo vya habari na kupitia mafunzo hayo wanatarajia kuwapo na kujiamini kwenye utendaji kazi wao.



# Wanawake watakiwa kugombea urais Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI Rais wa Zanzibar, Dk Ali Muhamed Shein anatarajiwa kumaliza muda wake wa uongozi mwaka 2020, wanawake wametakiwa kujiandaa kugombea nafasi hiyo ya urais.

Akizungumza jana katika mkutano wa kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi huko Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja, Mkurugenzi wa Huduma za Uchaguzi kutoka Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Idrisa Jecha, aliwataka wanawake kuondoa woga na kugombea nafasi hiyo wakati ukifika ambayo haina masharti magumu.

Mkurugenzi huyo pia aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu kugombea nafasi zingine za uongozi wakati ukifika na hakuna vikwazo vitakavyowafanya kutimiza dhamira yao hiyo.

Alisema wanawake wengi wana sifa za kugombea nafasi hizo lakini huwa waoga na badala yake huwaachia wanaume pekee.

Jecha alisema katika mfumo wa uchaguzi uliopo katika ZEC, fursa za kugombea nafasi za uongozi ziko wazi kwa makundi yote wakiwamo wanawake na wanaume.

"Tume (ZEC) haina vikwazo kwa mwanamke kugombea nafasi za uongozi katika kipindi cha uchaguzi mkuu ukifika. Makundi yote yako sawa katika kugombea nafasi za uongozi," alisema.

Alisema katika kipindi kifupi kijacho, ZEC inatarajia kuanza kutekeleza uandikishaji wapiga kura wapya na kufanya uhakiki.

Naye Haji Ubwa kutoka timu ya wanaume wa mabadiliko, aliwataka viongozi wa vyama vya siasa, dini na jamii kuondoa vikwazo ili wanawake wagombee nafasi ya uongozi na kusimamia taifa.

Ubwa ambaye pia ni kiongozi wa dini, aliwataka wanawake wasikatishwe tamaa na baadhi ya kauli za watu wanaosema mwanamke amekatazwa kujitokeza kugombea uongozi kwa mujibu wa dini ya Kiislamu.

# Dk. Shein awapa matumaini wazee

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

**Tunapoletewa kesi za udhalilishaji wa kijinsia kutoka polisi baada ya kukamilika kwa uchunguzi wake kwa kiasi kikubwa huwa hazijakamilika na ndiyo maana tunazifuatilia zaidi kwa kutaka kujua mambo ya ziada.**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, amekubali maombi ya wazee wanaopokea pensheni jamii kuwaongezea kiwango cha fedha pamoja na pensheni ya wazee wastaafu.

Pensheni jamii wanayopewa wazee wote waliofikia umri wa miaka 65 hutolewa na serikali kila mwezi na kila mmoja hupatiwa Sh. 20,000 hivyo Dk. Shein aliwaahidi kuwa kiwango hicho atakiongeza kabla ya kumaliza muda wake wa uongozi.

Akizungumza katika mkutano mkuu wa Jumuiya ya Wastaafu na Wazee uliofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakili mjini Zanzibar jana, Dk. alisema ataendelea kulifanyia kazi ombi hilo ili kuongeza kiwango cha pensheni hiyo.

"Maombi mliyonipa si magumu. Ombi lenu nimelikubali wazee wangu, niwaahidi kuwa nitalitekeleza lakini naomba mnipe muda ili kulifanyia kazi na kujua kuwa naongeza kiasi gani cha fedha katika pensheni hiyo pamoja na pensheni ya wazee wastaafu," alisema.

Pamoja na ahadi hiyo, Dk. Shein aliwataka vijana kuwaenzi na kuwathamini wazee kwa kuwa wako baadhi ya vijana wanavuka mipaka ikiwamo kuwadhalilisha na kuwanyanyapaa wazee.

Alisema pia baadhi ya vijana hao wamekuwa wakiwadharau na kuwatuhumu kuwa ni wachawi jambo ambalo ni kinyume cha maadili.

"Wamekuwa wakiwatuhumu wazee kuwa ni wachawi jambo ambalo hawana hata ushahidi. Pia wazee wamekuwa wanatengwa hata katika familia na hutengewa vyumba vya uwani wakati wametumia thamani na nguvu zao kujenga nyumba zao," alisema.

Aidha, aliitaka Jumuiya ya Wazee Zanzibar kukemea vitendo hivyo na kutoa elimu kwa jamii ili wazee watunzwe na kuthaminiwa.

Dk Shein alisema kuwafanyia ukatili wazee ni sawa na kuwanyima fursa na haki zao za msingi kwa kuwa wazee wana mchango mkubwa katika taifa na wamechangia maendeleo ya nchi, hivyo ni vyema kuthamini juhudi zao hizo.

Pia alielezea kusikitishwa na vitendo vinavyofanywa na baadhi ya vijana katika familia kwa kuwalazimisha wazee kuwapa urithi wa mali kabla ya kufariki dunia.

Alisema jamii inapaswa kujua na kuzisamini haki za wazee ikiwamo kulindwa , kupewa hifadhi na mambo yote umuhimu ili nao kujihisi ni sehemu ya watu katika jamii.

Hata hivyo, Dk. Shein aliwataka wazee kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi na kuangalia afya zao mara kwa mara ili kuweza kuwa na afya imara.



Baadhi ya wanachama wa Jumuiya ya Wastaafu na Wazee Zanzibar, wakifuatilia hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani), wakati akizindua jumuiya hiyo, katika ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Uwekezaji sekta ya utalii wawakuna mabalozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UIMARISHAJI wa miundombinu na katika sekta ya utalii uliofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, umewavutia mabalozi wa Tanzania wanaowakilisha nje ya nchi.

Wakizungumza baada ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo visiwani Zanzibar, mabalozi wamepongeza kazi kubwa inayofanywa na serikali hiyo kwa ajili ya kuongeza pato la taifa.

Balozi wa Tanzania nchini Uingereza, Dk. Asha Rose Migiro, alisifu kazi zinazofanywa katika ujenzi wa jengo la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na kusema mradi huo ni muhimu na utasaidia kuongeza idadi ya watalii Zanzibar.

Alisema mapato ya nchi yanategemea sana uwapo kwa miundombinu bora ya uwanja wa ndege ambao ndiyo sura ya nchi.

"Nimefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha uwanja wa ndege mikakati inayokwenda sambamba na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika kukuza utalii," alisema.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Brazil, Dk. Emmanuel Nchimbi, alipongeza juhudi zinazochukuliwa za kuitangaza sekta ya utalii ambayo ni moja ya vyanzo vya kuingiza mapato.

Alitaka juhudi zaidi zichukuliwe ili kupenya soko la utalii katika mabara mbalimbali hasa Amerika ya Kusini na Kaskazini yenye idadi kubwa ya watu.

"Tukiwa wawakilishi wa Tanzania nje ya nchi, moja ya kazi zetu kubwa tunazofanya ni kutangaza Zanzibar pamoja na vivutio vyake," alisema.

Kwa upande wake, Balozi wa Tanzania nchini Sweden, Dk. Wilibrod Slaa, alisema mipango imeanza kufanywa kuhakikisha ndege ya moja kwa moja inafanya safari katika nchi za Scandinavia hasa Sweden, Norway na Denmark kutoka Tanzania.

Alisema jina la Zanzibar linauzika katika sekta ya utalii na kuongeza kuwa kazi iliyobaki ni kuvitangaza vivutio zaidi vilivyopo ndani.

Mapema, Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, alisema kazi ya kutangaza vivutio vya utalii na kushiriki katika maonyesho ya utalii ya kimataifa zinaendelea.

"Sekta ya utalii sasa ndiyo tegemeo la uchumi wa Zanzibar badala ya karafuu. Sasa tumejipanga zaidi kuona tunapenya katika soko la dunia katika mabara yote," alisema.

Mabalozi 32 wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi, walifanya ziara ya siku moja Zanzibar kuangalia miradi ya maendeleo na vivutio vya utalii.

# Singida yaongoza wajawazito kupata vidonge kuongeza damu

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

ASILIMIA 98 ya wajawazito wamepatiwa vidonge vya kuongeza damu, hivyo kusababisha Wilaya ya Ikungi mkoani Singida kuwa ya kwanza kitaifa kwa kuwa na idadi kubwa ya wajawazito waliopatiwa vidonge hivyo.

Akitoa taarifa ya hali ya lishe ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kwenye kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji mwakilishi wa ofisa lishe wa wilaya, Ofisa Afya wa wilaya hiyo, Vestina Balaukwa, alisema asilimia 98 ya wajawazito walipewa matone ya vitamini 'A' baada ya kujifungua.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za Mtuha za mwaka 2018 hali ya lishe ya watoto chini ya miaka mitano katika halmashauri hiyo, asilimia 101 ya watoto chini ya miaka mitano walipewa matone ya vitamin 'A' na dawa za minyoo wakati asilimia tatu waligundulika kuwa na ukondefu na asilimia mbili waliozaliwa kwenye vituo vya kutolea huduma walikuwa na uzito pungufu.

**Baada ya kujifungua mtoto wake alianza kwa kusafisha maziwa na baada ya muda alianza kumnyonyesha na anatarajia kumnyonyesha kwa miezi sita.**

Aidha, Balaukwa alibainisha asilimia 14 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano waligundulika kuwa na uzito pungufu, asilimia 46 ya watoto wananyonya maziwa ya mama pekee kwa miezi sita bila kupewa chochote, hata maji ya kunywa na asilimia 68 ya watoto wenye umri wa miezi 0-23 walinyonya kwa miaka miwili.

Alisisitiza kwamba mila na desturi potofu katika jamii za kuwazuia watoto wasinyonye maziwa ya mwanzo ya njano ambayo yana kinga kwa mtoto mchanga ni moja ya sababu zinazoathiri hali ya lishe ya watoto chini ya miaka mitano na wanawake wenye umri wa kuzaa wenye umri wa kuanzia miaka 16 hadi 49.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Iglansoni, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Stephano Misai, alikemea suala la mimba za utotoni kwa watoto wenye umri wa kati ya miaka 15- 20 kwani kunawasababishia madhara makubwa watoto hao.

Naye ofisa mradi wa uboreshaji huduma za lishe katika kuimarisha afya ya uzazi kwa mama na mtoto (ENRICH), Irene Mmando, alisema mradi huo unaofadhiliwa na serikali ya Canada ni wa miaka mitano kuanzia 2018 hadi 2020 na unatekelezwa katika mikoa ya Shinyanga na Singida.

Baba bora wa mradi, Majinja Magaga, alitoa wito kwa kinababa wenzake wajenge utamaduni wa kuwasaidia wake zao kupeleka watoto kliniki kwani kazi ya kubeba mimba ni ya mtu mmoja, lakini malezi ni ya wote.

Mamalishe, Rebeca Ifegelo, alisema baada ya kujifungua mtoto wake alianza kwa kusafisha maziwa na baada ya muda alianza kumnyonyesha na anatarajia kumnyonyesha kwa miezi sita.

# CCM yashauri vyama upinzani

**Na Christina Haule,** MOROGORO

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Morogoro kimevitaka vyama vya upinzani nchini kuacha kubeza juhudi za serikali kwani kufanya hivyo, kutavifanya vipuuzwe na kuonekana vinaongozwa na watu wenye ufahamu mdogo.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa CCM Mkoa wa Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, wakati akizungumza na waandishi wa habari kufuatia kumalizika kwa mkutano wa wakuu wa nchi na serikali za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Alisema mada zilizotolewa kwenye mkutano wa SADC zililenga kuibua mageuzi ya huduma za kiuchumi kama ulivyo mpango mkakati uliowekwa na serikali.

Alisema licha ya kutoa mwelekeo kwa serikali, lakini pia kumevijengea ufahamu vyama vya upinzani vijue changamoto zilizopo na namna ya serikali ya CCM inavyoweka mikakati bila kubahatisha ili kusaidia kupunguza changamoto zilizopo katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Shaka alisema mada na mijadala iliojadiliwa kwa utaalamu kwenye kikao hicho, ililenga kukuza mbinu za kukuza huduma za jamii, maboresho na uondoaji changamoto katika sekta kama elimu, miundombinu, maji, umeme na kutanua wigo wa biashara.

Alisema matatizo ya kimaendeleo Kusini mwa Afrika kwa ujumla wake yamewekewa mkazo, huku serikali zikitakiwa kujiwekea misingi ya ushughulikiaji changamoto zinazowakabili wananchi kwa kutafuta ufumbuzi wa haraka na wa kudumu kadri inavyowezekana.




Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa (wa pili kulia), akikabidhi cheti kwa mmoja wa wafanyabiashara na wateja wazuri wa Benki ya NMB mkoani humo, Ephraim Lwoga, wakati wa kongamano la wanachama wa klabu ya wafanyabiashara Mkoa wa Tanga jana, lililolenga kuwapa mafunzo na nidhamu ya biashara. Wa pili kushoto ni Meneja wa Benki hiyo, Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kesi za udhalilishaji wa kijinsia 45 zaripotiwa

**Na Mwandishi Wetu,**

JUMLA ya kesi 45 za udhalilishaji wa wanawake na watoto zimeripotiwa katika Ofisi ya Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba kuanzia Januari hadi Julai mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mkuu wa Wilaya hiyo Rashid Hadid Rashid, alisema, hali ya matukio ya udhalilishaji mwaka huu yameongezeka kwa kesi 15 ukilinganisha na mwaka jana.

Alisema kuanzia Julai hadi Desemba mwaka jana, ofisi hiyo ilipokea kesi 30 za udhalilishaji wa wanawake na watoto, ambapo mwaka huu wamepokea jumla ya kesi 45 za udhalilishaji.

"Kwa kipindi cha miezi saba ya mwaka huu inaonyesha kwamba kesi zimeongezeka kwani tumepokea kesi 45, wakati mwaka jana kuanzia Julai hadi Desemba tulipokea kesi 30," alisema.

Alitaja sababu ya kuongezeka kwa kesi hizo ni kutokana na wananchi kupata mwamko wa kuyaripoti matukio hayo kwenye vyombo vya sheria.

"Zamani wananchi walikuwa hawana utamaduni wa kuripoti matukio haya ya udhalilishaji kwa kuona aibu na ndio maana yalionekana kuwa kidogo, lakini kutokana na mwamko wanaoupata sasa wanayaripoti kila siku bila ya woga," alisema.

Alieleza kati ya kesi hizo zilizoripotiwa ubakaji ni kesi 30, ambapo mwaka jana ziliripotiwa tisa na mwaka huu zimeripotiwa 21.

"Pia kuna kesi za utelekezwaji wa watoto, ambazo kinababa hutelekeza familia zao ama kwa kwenda dago au kuwapa talaka wake zao, jambo ambalo linasababisha kuongezeka udhalilishaji," alisema.

Mkuu huyo aliwataka wanaume kuacha tabia ya kutoa talaka kiholela, ili kupunguza vitendo vya udhalilishaji na ukatili kwa wanawake na watoto.

Aliwaomba wazazi na walezi kushirikiana pamoja katika kurejeshe malezi ya zamani ya kuwalea watoto kwa pamoja, jambo ambalo litasaidia sana kupunguza udhalilishaji ndani ya jamii.

"Pia muhali ni tatizo kubwa linaloikumba jamii yetu ambayo husababisha kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji siku hadi siku, hivyo wananchi waache rushwa muhali na watoe ushahidi mahakamani," alisema.

# Serikali ya mpito Sudan kuongoza miaka mitatu

**KHARTOUM, Sudan**

UONGOZI wa kijeshi na kiraia utakaoongoza Sudan umezinduliwa jijini Khartoum baada ya mkataba utakaotoa mwongozo wa serikali hiyo kutiwa saini hivi karibuni.

Serikali hiyo ya mpito ambayo ilitarajiwa kutangazwa siku ya Jumapili iliyopita, iliahirishwa hadi wiki hii kwa mujibu wa taarifa za kijeshi.

Serikali hiyo itaongoza nchi hiyo kwa kipindi hicho, baada ya kuondolewa madarakani kwa Rais wa zamani Omar Al Bashir mwezi Aprili, mwaka huu kufuatia maandamano ya wananchi.

Mbali na wanajeshi, serikali hiyo inaundwa na viongozi wa waandamanaji na vikundi vya upinzani.

Baraza la juu litakaloongoza, litakuwa na wajumbe 11, sita kutoka upande wa kiraia na wengine watano upande wa kijeshi.

Uongozi huo wa juu, utasimamia uteuzi wa Baraza la Mawaziri wakiwamo wabunge watakaowakilisha raia wa nchi hiyo.

Awamu ya kwanza ya uongozi wa serikali itaongozwa na Jenerali wa kijeshi kwa kipindi cha miezi 21 huku kiongozi wa kiraia akimalizia awamu ya pili ya miezi 18.

**RFI**

# Raia Zimbabwe wajipanga kuandamana tena

**HARARE, Zimbabwe**

WAANDAMANAJI Zimbabwe wanapanga kufanya maandamano tena, baada ya juzi kuzuiliwa na Jeshi la Polisi.

Hatua hii inafuata licha ya ukamataji uliofanyika Jumatatu saa kadhaa kabla ya maandamano kuanza ambayo yalipigwa marufuku na Jeshi la Polisi la nchi hiyo.

Hata hivyo, Waziri wa Mambo ya Nje na Biashara ya Kimataifa wa Zimbabwe, Sibusiso Moyo kutetea hatua iliyochukuliwa na vyombo vya dola.

Moyo ameutetea ukamataji uliofanyika Jumatatu kwa waandamanaji wanaoipinga serikali na alitoa wito kuwapo hali ya kustahmiliana katika kipindi hiki cha kurejesha uchumi wa nchi hiyo ulioharibika.

Moyo alisema kuwa japokuwa kila mtu ana haki ya kuandamana, kumekuwapo na kampeni nyingi zinazochochea ghasia na kukiuka usalama wa umma.

Vilevile ilikubaliana na Mahakama ya Zimbabwe kuunga mkono marufuku iliyokwekwa na polisi kwa maandamano yaliyoandaliwa na ushirika wa upinzani wa Movement for Democratic Change-MDC

**DW**

# Wanajeshi Uturuki wapigwa shambulio shtukizi

**DAMESKI, Syria**

SHAMBULIO la angani la serikali ya Syria lililolenga msafara wa kijeshi wa Uturuki uliokuwa ukielekea katika eneo linalotawaliwa na waasi kaskazini mwa Syria, limesababisha vifo vya raia watatu, Uturuki imedai.

Imeeleza kuwa watu wengine 12 walijeruhiwa katika shambulio hilo katika mji wa Idlib siku ya Jumatatu kulingana na Wizara ya Ulinzi ya Uturuki.

Mji wa Idlib ambao ni mojawapo ya maeneo machache yasiodhibitiwa na serikali, ilitarajiwa kulindwa na kuwa eneo huru linalotenganisha majeshi pinzani lililoafikiwa na Uturuki inayowaunga mkono waasi mwaka uliopita.

Lakini mashambulizi ya serikali yamekuwa yakiongezeka tangu mwezi Aprili.

Mamia ya raia wameuawa kutokana na hilo na kuna hofu kwamba wengi watafariki iwapo hali itaendelea kuwa mbaya.

Jan Egeland kutoka baraza la wakimbizi la Norway alisema: “Hii ndio hatari inayotukabili kwa sasa, kwa miaka kadhaa sasa tumeonya kuhusu hatari inayoikabilia Idlib, ambapo hakuna mahala pa kutorokea kwa raia milioni tatu” alisema na kuongeza:

“Kuna wapiganaji wabaya mjini humo. Lakini shambulio la jumla katika eneo hilo pamoja na lile lililo mkabala la kaskazini mwa Hama litamaanisha kwamba watoto milioni moja wataathiriwa na vita hivyo na hicho ndicho tunakiona kikifanyika”

Uturuki inayounga mkono baadhi ya waasi na sio wote ina majeshi yake mjini Idlib kama mojawapo ya makubaliano na Urusi yaliyofanyika mwaka uliopita. Msemaji wa waasi wa National Liberation Front, Naji Mustafa, alisema msafara huo ulikuwa ukielekea katika mojawapo ya vituo vyake vya uchunguzi na walinzi wakati shambulio hilo lilipotokea,

Alisema msafara huo ulikuwa na magari 50 ya kijeshi, matano kati yao yakiwa vifaru.

Kwa upande wao Syria imesema kuwasili kwa msafara huo katika eneo hilo ni kitendo cha uchokozi.

Imesema kuwa silaha hizo hazitasitisha harakati za wanajeshi wa Syria kukabili kile ilichokitaja kuwa magaidi.

Kulingana na Shirika la Haki za Kibinadamu la Syrian Observatory for Human Rights (SOHR), lililo na makao yake nchini Uingereza, ndege ya kijeshi ya Urusi ilitekeleza mashambulio karibu na msafara huo juzi.

Uturuki imesema kuwa shambulio hilo linakiuka makubaliano yaliyofanyika mwaka uliopita, huku kisa hicho kikizua hofu kuhusu makubaliano ya moja kwa moja kati ya mataifa hayo mawili.

***BBC***



Vijana wa chama cha CNDD-FDD kinachotawala nchini Burundi na wale wa chama cha upinzani cha CNL wakiwa katika mapigano. **PICHA: REUTERS**

# Burundi kwazidi kuwaka moto

**BUJUMBURA, Burundi**

MTU mmoja ameuawa na wengine sita wamejeruhiwa katika makabiliano kati ya vijana wa chama cha CNDD-FDD kinachotawala nchini Burundi na wale wa chama cha upinzani cha CNL.

Mtafaruku huo umeibuka baada ya takribani vijana 300 wa chama cha upinzani CNL kukabiliana na wafuasi wa chama tawala waliokuwa wamebeba mapanga wakati wakitokea katika uzinduzi wa makao makuu ya chama hicho katika Mkoa wa Muyinga.

Katibu Mkuu wa chama tawala, Evariste Ndayishimiye, amewataka wakuu wa tawi hilo la vijana kwenye ngazi tofauti kukaa meza moja na wenzao wa chama CNL na kujadiliana, ili kuepusha hali kama hiyo isitokee tena.

Taarifa kutoka katika kijiji cha Rugari Mkoa wa Muyinga kaskazini mwa Burundi zinasema vijana wapatao 300 wa chama cha upinzani CNL waliokuwa katika uzinduzi wa makao makuu ya chama chao, waliingia katika mtego wa baadhi ya vijana wa Imbonerakure wafuasi wa chama tawala waliokuwa wamebeba mapanga.

Makabiliano kati yao yalisababisha kijana mmoja wa CNL kuuawa huku wengine sita wakijeruhiwa vibaya.

Picha zimesambaa kwenye mitandao ya kijamii zikionesha majeruhi wenye majeraha makubwa baada ya kupigwa mapanga vichwani.

Tukio kama hilo limeripotiwa pia katika kata ya Ruziba Kusini mwa Bujumbura ambapo vijana wafuasi wa vyama hivyo viwili wamekabiliana.

Taarifa zaidi zinasema kuwa nyumba kadhaa za eneo hilo zimebomolewa huku nyingine zikichomwa moto, ikiwamo makao ya chama hicho yaliyotarajiwa kuzinduliwa rasmi jana.

Mkuu wa Tarafa ya Muha, Kabura Daniel, amewatupia lawama wafuasi wa chama cha upinzani CLN ya kwamba walikiuka sheria.

Kabura alisema kuwa waliafikiana katika mikutano yao kuwa pindi chama kinapokusudia kuandaa mkutano ama shughuli yoyote ile ya kisiasa ni lazima kitaarifu mamlaka husika ili hatua za usalama zichukuliwe kuepusha vurugu, lakini chama cha CNL hakijafanya hivyo.

Mkuu wa chama hicho, Agathon Rwasa, amekuwa akilalamika na kusema matukio kama hayo yamekithiri.

Hali hiyo inajiri wakati Burundi Inajiandaa kwa uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani, ambapo Rais Pierre Nkurunziza aliahidi kuwa hatogombea tena

***DW***

## Vodacom yatoa mil. 330/- kuwezesha Dodoma ya kijani

Na Mwandishi Wetu

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Vodacom Tanzania Foundation (VTF), jana imesaini mkataba wa makubaliano na World Wide Fund for Nature (WWF) ili kuchangia Sh. milioni 303 kwa ajili ya mradi wa 'Kijanisha Dodoma' ambao umeratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na WWF.

Hafla hiyo ilifanyika jana ofisi za WWF jijini Dar es Salaam na kushuhudiwa na Ofisa wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Thomas Bwana, aliyemwakilisha Naibu Katibu Mkuu katika wizara hiyo, Balozi Joseph Sokoine.

Dk. Bwana alisifu mpango wa VTF na WWF kupambana na hali ya mabadiliko ya tabia nchi na kufurahishwa na kampuni na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanavyoungana kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu namba 13 kuhusu hali ya hewa.

"Kutokana na asilimia 80 ya watu kutegemea mazingira na maliasili kwa ajili ya kutengeneza kipato, kulinda maliasili, ni jambo muhimu litakalochochea mafanikio ya kufikia mpango wa maendeleo ya kiuchumi. Serikali imeweka mikakati kwa ajili ya kupambana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi nchini Tanzania pamoja na kuhakikisha kuwa jamii ina mifumo ya kukabiliana na mabadiliko haya, jambo linalofanya tufurahie ushirikiano huu," alisema.

Alisema serikali ina mpango wa kupanda miti milioni 280 kila mwaka ili kuunga mkono mpango wa taifa wa kusimamia na kupanda miti kwa ajili ya kuifanya nchi inakuwa ya kijani.

Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia, alisema wamefurahia kuingia ubia na WWF ili kutekeleza mpango huo ambao unawiana na mpango mkakati wa VTF kwa mwaka 2019/21 ambao umejikita kuchochea hatua za kudhibiti mabadiliko ya tabia nchi.

"Maono yetu ni kuwaunganisha watu ili kuleta maendeleo Tanzania, tuna matumaini ya kuunda jamii ya kidijitali, tukilenga kujenga uchumi jumuishi na kufanya kazi katika sayari ambayo athari zetu ni ndogo. Mradi huu umejizatiti kuifanya Dodoma kuwa ya kijani, lakini tunatumaini uwapo wa ongezeko la hatua za kisasa dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi kutoka ufahamu na uhamasishaji wa jamii," alisema Mworia.

Akizungumzia ushirikiano huo, Mkurugenzi Mkazi wa WWF Tanzania, Dk. Amani Ngusaru, alisema mfuko huo utaelekezwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kuufanya mji wa Dodoma kuwa kijani kwa kupanda miti 100,000 kwa mwaka wa kwanza na kutengeneza bustani ndani ya mji mkuu pamoja na kuongeza ufahamu na kuhamasisha jamii kwa kuwapa mafunzo makundi ya vijana na wanawake katika uzalishaji na matumizi ya mifuko ya plastiki mbadala na kusimamia taka kama shughuli ya kuwawezesha kiuchumi. Mradi huo uliopewa jina 'Kuishi kwa amani na mazingira asili' utaanza rasmi mwezi Septemba, mwaka huu na utatekelezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Halmashauri ya Jiji la Dodoma na taasisi ya huduma za misitu (TSF).

# JPM aipongeza Maabara Mkemia Mkuu wa Serikali

Na Mwandishi Wetu

RAIS Dk. John Magufuli ameipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchunguza sampuli mbalimbali, kusimamia sheria za usimamizi wa kemikali na kudhibiti vinasaba vya binadamu.

Rais Magufuli alitoa pongezi hizo jana alipotembelea Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali iliyopo Kivukoni jijini Dar es Salaam na kuona jinsi mitambo ya uchunguzi vya kisasa inavyofanya kazi ikiwamo uchunguzi wa vinasaba vya miili ya watu waliopoteza maisha katika ajali ya moto iliyotokea mjini Morogoro Agosti 10, 2019 baada ya lori lililobeba mafuta kupinduka na kisha kulipuka moto.

Akiwa katika maabara hiyo, Rais Magufuli alijionea mitambo mipya ya uchunguzi wa vinasaba vya binadamu, sumu, dawa za kulevya, kemikali na dawa inavyofanya kazi kwa haraka na uchunguzi wa sampuli moja huchukua muda wa dakika 45 na unafanywa na vijana wa Tanzania.

Akizungumza na wafanyakazi wa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Rais Magufuli aliwapongeza kwa kazi kubwa ya utambuzi wa vinasaba waliyoifanya kwa miili 10 ya ajali ya kuzama kwa kivuko cha MV Nyerere, miili 14 ya ajali ya moto iliyotokea Tarime Mkoani Mara na miili 50 kati ya 69 ya watu walioungua moto katika ajali ya lori la mafuta Mjini Morogoro.

Pamoja na kufanikisha utambuzi wa vinasaba katika miili hiyo na hivyo kuwawezesha ndugu wa marehemu kutambua ilipozikwa miili ya ndugu zao, Rais Magufuli pia amewapongeza kwa uadilifu na uchapakazi wao katika majukumu mengine yakiwamo kutambua dawa za kulevya, kutoa ushahidi mahakamani na kufanya kazi katika mazingira yenye kemikali hatari kwa afya ya binadamu.

Rais Magufuli alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Tano iliamua kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kununua vifaa vipya na vya kisasa, kuongeza wafanyakazi na kuibadili kutoka kuwa Wakala wa Serikali na kuwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kutambua umuhimu wake mkubwa na kuiongezea nguvu za kufanya kazi kwa uhuru zaidi ili kupata manufaa yanayotarajiwa.

"Nafahamu kuna wakati mlikuwa mnachunguza jambo na mnaandika ripoti ya uchunguzi wenu lakini hizo ripoti zilikuwa zinazimwa kwa sababu mlikuwa hamna nguvu, sasa mna nguvu nataka mfanye kazi," alisema.

Aliwataka wafanyakazi wa Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuendelea kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa, kutopokea rushwa, kutotoa siri na kuepuka kuingiza vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha watumishi wa ofisi hiyo wanaofanya uchunguzi wa masuala mazito wanakuwa salama na hawaingiliwi katika majukumu yao.

Alimuagiza Mwenyekiti wa Bodi ya mamlaka hiyo, Prof. Ester Jason na Mkemia Mkuu wa Serikalim Dk. Fidelice Mafumiko, kusimamia vizuri matumizi ya fedha zinazotumika kununua mahitaji mbalimbali vikiwamo vitenganishi vitumikavyo maabara.

Mapema katika taarifa yake, Dk. Mafumiko alimshukuru Rais Magufuli kwa Serikali ya Awamu ya Tano kutoa Sh. bilioni 5.338 kwa ajili ya kununulia mitambo na kuongeza wafanyakazi kutoka 110 hadi 294 hali iliyoongeza ufanisi wa kazi na kwa kipindi cha miaka minne tangu 2015 vielelezo 204,974 vimechunguzwa sawa na wastani wa vielelezo 51,244 kwa mwaka, kiwango ambacho ni ongezeko la asilimia 510 ikilinganishwa na rekodi za mwaka 2015/16.

Alibainisha kuwa ufanisi wa mamlaka hiyo pia umesaidia kuongeza mahudhurio mahakamani kutoka kesi 35 kwa mwezi (2015) hadi kufikia kesi 220 kwa mwezi mwaka huu (2019) na imeongeza ofisi nyingine mbili za Kanda ya Kati na Kanda ya Kusini hali iliyorahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Rais Magufuli alipata nafasi ya kuwasiliza wafanyakazi wa mamlaka hiyo na kuahidi kufanyia kazi changamoto mbalimbali zikiwamo mahitaji ya vifaa vya kisasa zaidi vya kufanyia kazi, kuboresha maslahi ya watumishi na kuimarisha miundombinu.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akikabidhiwa cheti cha shukurani na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wastaafu na Wazee Zanzibar (JUWAZA), Masururu Saadun Ferouz, baada ya kuzindua jumuiya hiyo, Kikwajuni Zanzibar jana. Kulia ni Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Zanzibar, Maudline Castico. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Namna kubaini samaki aliyevuliwa kwa bomu

INATOKA UK 4

"Huwa nasikia tu kuna samaki wanavuliwa na mabomu, lakini mimi sijawahi kuwaona wala kuwagundua, ninachojua kununua samaki na kuwaleta dukani kwangu," Omary alisema.

Isaak Barnabas, muuzaji wa samaki eneo la Mbezi jijini, alisema hutumia kigezo kimoja tu cha kumwangalia samaki kwenye matamvua kama kuna damu inayochuruzika kubaini kama amevuliwa kwa bomu au la.

Bala Gomwa, mmoja wa madalali wa samaki jijini, aliiambia Nipashe kuwa watu wengi hawana uwezo wa kutambua samaki waliovuliwa kwa kutumia mabomu.

"Siyo rahisi kumtambua samaki aliyevuliwa kwa mabomu hasa kama hauna uzoefu na uvuvi. Kati ya madalali 60, unaweza kupata wawili au watatu wenye uelewa wa samaki na wakamtambua samaki aliyevuliwa kwa bomu," alisema.

Takwimu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zinaonyesha kuwa mwaka 2018/2019, Tanzania ilikuwa na tani 2,803,000 za samaki. Kati yake, Ziwa Victoria kuna tani 2,210,000, Ziwa Tanganyika tani 295,000 na Ziwa Nyasa tani 168,000, kwenye maziwa madogo ya kati, mito na mabwawa tani 30,000 na Bahari ya Hindi tani 100,000.

Kwa mujibu wa Waziri Mpina, kwa mwaka 2018/2019, jumla ya wavuvi 202,053 wanaotumia vyombo vya uvuvi 58,930 walishiriki moja kwa moja kwenye shughuli za uvuvi na kuvuna tani 389,459.40 za samaki wenye thamani ya Sh. trilioni 1.83.

Kati yake, tani 333,782.32 (asilimia 85.7) zilitoka maji baridi na tani 55,677.08 zilitoka maji bahari.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

**MASHAMBA YANAUZWA DODOMA:** Kuanzia ekari 1 hadi ekari 50 bei maelewano, wasiliana na Dodoma Pazuri Group (DPG) Simu:0745312845/0657746365

**VIWANJA VINAUZWA KISEMVULE:** Malipo awamu mbili urefu futi 50 kwaa upana futi 40 bei Sh.1,700,000/=na Sh.1,200,000/= tu, Simu:0714564651/0623528465.

**MAFUTA ORIJINO YA ALIZETI:** Toka Singida, lita 5 tunauza kwa Sh.20,000/= tu ukiagiza kuanzia lita 20 tutakuletea mahali ulipo. Simu:0623528465/0655782175.

**WACHIMBAJI WA VISIMA:** Tunachimba visima virefu/ vifupi mijini/vijijini kwa bei nafuu na tunakupatia ofa ya pampu 1 HP ya buree!! Simu:0657746365/0788767141.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO


### KUPOTEA KWA CHETI




**Lucia Ishemango** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0360-029 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1990 katika shule ya Sekondari KISHOJU

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: KAR/RB/2170/2016**

115377502

### KUPOTEA KWA CHETI



**Kasmir David Kanijo** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato nne chenye **index namba S741/0022** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1995 katika ya Shule ya Sekondari Itende.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: URP/RB/9393/2014**

115377502

### KUPOTEA KWA CHETI



**Esther Donald Victor** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0804-0007** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika shule ya Sekondari DCT Mvumi.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DAR/CHA/RB/176749/2019**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PAUL JUSTINE OLOMY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA PICK UP yenye namba za usajili T 759 BWD, Chassis Na. RZN1470028267, Engine Na.1RZ-2543349.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/216713/2019.**

215383002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAMAKA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa Mirathi No. 71/2019**

Ombi la 1. NASSORO J. SWALEHE.
2. ZENA J. SWLEHE kuteuliwa

Msimamizi wa Mirathi Marehemu JUMANNE SWALEHE
Kwa yeyote ANAYEHUSIKA TANZANIA - BARA
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 23/9/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamni waweza kukaguliwa. Tarehe 20/08/2017

215383102

### KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LIMITED.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BAJAJ BOXER Yenye namba za usajili MC 257 BTT Chassis Na.MD2A21BY8HWE90989. Engine Na. PFZWHE62745.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/217034/2019.**

115382902


Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
NEWSPAPER
CLASSFIED ADVERTISEMENT

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# SOLSKJAER, RASHFORD WASIMULIA PENALTI YA POGBA

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesisitiza kwamba, hana tatizo na Paul Pogba kupiga penalti kwa Manchester United, baada ya Mfaransa huyo shuti lake kuokolewa na golikipa, Rui Patricio juzi Jumatatu usiku, wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Wolverhampton Wanderers kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Baada ya kuzawadiwa penalti hiyo, Pogba alizungumza na mchezaji mwenzake, Marcus Rashford kuamua nani ataipiga.

Na ikaamuliwa kati yao kuwa Mfaransa huyo atapiga, lakini shuti lake likaokolewa na golikipa Patricio.

Akizungumza na Sky Sports mara baada ya mchezo huo, Solskjaer alisisitiza kwamba hana tatizo na kiungo huyo kupiga penalti, kwani majukumu yote amewaachia Pogba na Rashford.

Alisema: "Wao wawili ndio wameteuliwa kupiga penalti za timu. Ni jukumu lao wenyewe kuamua nani anapiga penalti.

"Kuna wakati wachezaji wanahisi kwamba wanajiamini vya kutosha Paul amefunga penalti nyingi kwa timu yetu, leo (juzi) Patricio aliokoa vizuri.

"Unaweza kuona kwamba walizungumza kwanza, kwa sababu wote wamepewa majukumu ya kupiga penalti.

"Wote wawili wamekuwa wanajiamini kabla. Marcus alifunga wiki iliyopita na Paul alikuwa anajiamini. Napenda wachezaji wanaojiamini."

Si Rashford wala Pogba ambaye alionekana kuwa na shauku wakati wanajadiliana nani apige penalti, kwani wote wawili walionekana kutaka kumuachia mwenzake.

Hata hivyo, Pogba ndiye alipewa jukumu na kupiga na Rashford alisisitiza kupitia BBC Sport kwamba, hakuna tatizo lolote kwa kilichotokea.

"Paul alitaka kupiga, ni rahisi tu. Mtu yeyote anaweza kukosa penalti, amefunga penalti nyinkwa upande wetu na ni kawaida kukosa moja," alise- g i Rashford. m a

"Ni rahisi kama unataka kupiga, unapiga tu. Nilipiga moja wiki iliyopita kwa upande wangu hakukuwa na tati- zo.

"Ni bahati mbaya kwamba hakufunga, lakini huo ndio mchezo wa mpira wa miguu. Kujiamini kunakufanya mara zote uweze kufunga."

# NYOTA MADRID LAO MOJA NA BALE

**MADRID, Hispania**



WACHEZAJI wenzake na Gareth Bale ndani ya klabu ya Real Madrid wamesema wapo pamoja na nyota huyo wa Wales na kumtaka apambane ili kuzidi kupata mafanikio hapo Bernabeu licha ya majaliwa yake kuonekana hayajulikani baada ya kukaribia kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto.

Alionekana kutokuwa kwenye mipango ya kocha, Zinedine Zidane na karibia atue nchini China kwa dili ambalo lingemfanya apokee mshahara wa pauni milioni moja kwa wiki, lakini alikuwa na kikosi cha Real Madrid kwenye mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Baada ya mkanganyiko huo, Bale sasa ameonyeshwa kuungwa mkono na wawili kati ya wachezaji wenzake, huku Casemiro na Thibaut Courtois wakituma ujumbe wa wazi kabisa kwa Zidane kuonyesha kile wachezaji wanachokifikiria.

Akizungumza baada ya ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Celta Vigo, Casemiro alisema: "Ametupa mataji mengi, alifunga kwenye fainali na anapewa heshima kubwa miongoni mwetu.

"Anatakiwa kucheza. Yeye ni mchezaji mkubwa na ni muhimu mno kwetu."

Na ilikuwa sawa kwa kauli ya golikipa wa zamani wa Chelsea, Courtois, ambaye alisema:"Ni mchezaji muhimu na mkubwa kwa mechi kubwa.

"Kila mmoja anampenda na ni muhimu kwamba anacheza na sisi. Tuna furaha kuwa na Bale.

Wachache hawakutarajia Bale kuanza kwenye mchezo huo, lakini alijumuishwa kwenye kikosi cha kwanza na ndiye aliyepika bao la Karim Benzema.

Wakati alipotolewa kipindi cha pili, alikumbatiwa na Zidane kabla ya kwenda kukaa benchi.

# MAMA WA BALOTELLI ALIA MWANAWE KUTUA BRESCIA

**ROME, Italia**

MARIO Balotelli amebainisha kwamba mama yake alilia wakati alipomuambia anajiunga na timu ya mji wa nyumbani kwake Brescia na amesisitiza kwamba hana hofu ya kushindwa baada ya kurudi kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kufuatia kuikosa kwa miaka mitatu.

Balotelli alizaliwa mjini Palermo lakini alihamia Brescia akiwa na umri wa miaka miwili, na wazazi wake waliomuasili bado wanaishi hapo, ingawa baba yake alifariki mwaka 2015.

Akizungumza katika mahojiano yake ya kwanza Jumatatu, Balotelli alisema, "Mama yangu awali alilia wakati nilipomuambia kwamba ninatakiwa kwenda Brescia ... alikuwa na furaha iliyopitiliza."

Balotelli aliwasili Brescia kama mchezaji huru baada ya mkataba wake na Marseille kumalizika mwishoni mwa msimu.




Kwa mara ya mwisho kucheza nchini Italia alikuwa amekumbwa na majeraha na alifunga mara moja tu wakati akicheza kwa mkopo wa muda mrefu pale AC Milan kabla ya kurudi Liverpool mwaka 2016 na haraka akaenda nchini Ufaransa katika klabu ya Nice na baadaye Marseille.

Balotelli mwenye umri wa miaka 29, aliongeza kusema: "Sina hofu yoyote, niko vizuri kabisa hapa na nimetulia."



# DEMBELE

## ATIBUA FOWADI YA BARCA

**BARCELONA, Hispania**

OUSMANE Dembele atakuwa nje ya dimba kwa wiki tano baada ya kuumia misuli na kuifanya Barcelona kuwa na uhaba wa washambuliaji kuelekea kwenye mchezo wa Jumapili dhidi ya Real Betis.

Dembele mwenye umri wa miaka 22, alifanyiwa uchunguzi Jumatatu baada ya kuumia kwenye mchezo wa kichapo wa Ijumaa kutoka kwa Athletic Bilbao.

Majeraha hayo kwa Mfaransa huyo yamekuwa ni bahati mbaya kwa Barca, ambao tayari wanawakosa Lionel Messi na Luis Suarez.

Messi hajaichezea klabu yake tangu kumalizika kwa msimu uliopita kutokana na kuumia kigimbi cha mguu wakati wa mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya mapema mwezi huu.

Suarez, naye aliumia kigimbi cha mguu wakati wa mchezo wa kipigo cha bao 1-0 pale kwenye dimba la San Mames.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay hatarajii kurudi uwanjani haraka hadi Septemba wakati wa mapumziko ya mechi za kirafiki za kimataifa, ingawa kocha Ernesto Valverde anaweza kumtumia Messi kwenye mchezo wa wikiendi inayokuja dhidi ya Betis.

Messi bado hajarudi kwenye mazoezi na wachezaji wenzake, kwani amekuwa akijifua peke yake ili kujiweka fiti.

Antoine Griezmann, kwa sasa ndiye mshambuliaji pekee aliyebaki kwa Barcelona akiwa fiti bila majeraha.

Rafinha pia anaweza kucheza pamoja na Sergi Roberto na Carles Alena, huku pia winga kutoka timu B, Carles Perez amekuwa akifanya mazoezi na kikosi cha kwanza kwa kipindi chote cha majira ya joto.

Huku Philippe Coutinho yeye tayari ameshatua kule Bayern Munich na Malcom aliuzwa kwa klabu ya Zenit Saint Petersburg ya Urusi.

# Coutinho: Nataka kubaki kwa muda mrefu Bayern

**MUNICH, Ujerumani**

PHILIPPE Coutinho amesema anataka kukaa Bayern Munich "kwa muda mrefu" ili "kushinda mataji mengi" baada ya kukamilisha uhamisho wake wa muda mrefu kutoka Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alitua kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Jumatatu wiki hii huku mkataba wake ukiwa na kipengele kinachoitaka Bayern kumnunua nyota huyo wa kimataifa wa Brazil kwa pauni milioni 109.8 mwishoni mwa msimu huu.

Kiungo huyo mshambuliaji ametua Ujerumani baada ya kufunga mabao 21 katika mechi 75 alizocheza tangu atue pale kwenye dimba la Nou Camp akitokea Liverpool Januari mwaka 2018, huku akishinda mara mbili mfululizo taji la Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'].

Baada ya msimu mmoja na nusu nchini Hispania, Coutinho sasa ana nafasi ya kung'arisha kiwango chake kule Bayern.

"Nina changamoto kubwa hapa na natumaini kubaki hapa kwa muda mrefu na kushinda mataji mengi," alisema Coutinho wakati akitambulishwa kwa waandishi wa habari.

"Mara zote kuna matarajio makubwa hapa Bayern na bila shaka taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na nitafanya kila niwezalo kushinda



Kombe la Bundesliga, DFB-Pokal na Ligi ya Mabingwa Ulaya nikiwa na wachezaji wenzangu.

"Nimetua hapa nikiwa na matarajio makubwa, mimi ni mtu mwenye malengo na nilizungumza na Thiago, Rafinha na Lucio, na nimesikia mambo mengi mazuri, hakika wamenisaidia mno.

"Mimi malengo yangu ni kufanya kazi kwa bidii na wakati nikivaa jezi ya Bayern nitacheza kwa juhudi zote uwanjani ili kufikia malengo yangu na timu."

Mchezaji huyo atavaa jezi namba 10 ambayo ilikuwa ikivaliwa na Arjen Robben aliyestaafu.

Mholanzi huyo alistaafu msimu uliopita baada ya kufunga mabao 144 katika mechi 309 kwa kipindi cha zaidi ya miaka 10 aliyoichezea klabu hiyo ya Bavaria.

Coutinho anajua kwamba atakuwa na kazi kubwa kufikia mafanikio aliyopata mtangulizi wake hapo kwenye Uwanja wa Allianz Arena.

"Jezi ya FC Bayern na namba 10 niliyopewa ni majukumu makubwa kwangu," aliongeza.

"Ilikuwa inavaliwa na Robben, alikuwa mchezaji mkubwa wa soka. Natumaini kufikia matarajio kwa kucheza soka vizuri uwanjani."

Kuwasili kwa Coutinho ni baada ya kusajiliwa kwa Ivan Perisic kutoka Inter Milan, ambaye alijiunga na Bayern wiki iliyopita kwa mkopo wa muda mrefu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia mkataba wake una kipengele cha kumnunua moja kwa moja mwishoni mwa msimu huu 2019/20.

# PSG yakataa ofa ya mkopo kwa Neymar

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain inapanga kuikataa ofa ya kumtoa kwa mkopo kwenda Barcelona mchezaji wake anayataka kuondoka, Neymar, kwa mujibu wa ESPN FC.


Mapema Jumatatu, ESPN FC iliripoti kwamba miamba wa Catalunya, Barcelona walikuwa wanataka kumchukua Neymar kwa mkopo huku kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja kipindi cha majira ya joto kijacho, lakini mpango huo umepangwa kukataliwa.

Ofa hiyo ya mkopo ilitarajiwa kutolewa jana Jumanne au leo Jumatano, lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, hawataikubali.

PSG inayomilikiwa na tajiri kutoka nchini Qatari ipo tayari kumuuza Neymar kipindi hiki cha majira ya joto, lakini wanataka kulipwa euro milioni 222 ambazo wao walizitoa wakati walimleta hapo jijini Paris kipindi cha majira ya joto mwaka 2017.

Taarifa zaidi zinaeleza kwamba, Barcelona kwa sasa hawatakuwa na uwezo wa kulipa kiasi hicho cha fedha, kwani njia pekee wanayoweza kuifanya ni kulipa kwa mafungu.

Mkurugenzi wa michezo wa PSG, Leonardo anataka kupata fedha za mkupuo kwa kumuuza Neymar, angalau euro milioni 200.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP: CHAMBERLAIN LAZIMA AWE MVUMILIVU

●●●Anapaswa kuwa mvumilivu katika njia sahihi na pia kila kitu kitakuwa sawa kwa asilimia 100...

**Liverpool, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amemtaka Alex Oxlade-Chamberlain kuwa mvumilivu katika kuimarisha idara ya kiungo baada mchezaji huyo kusumbuliwa na majeraha ya goti kwa muda mrefu.

Oxlade-Chamberlain, 26, alionyesha kiwango cha kuvutia baada ya kujiunga na Liverpool miaka miwili iliyopita, lakini akakumbwa na majeraha ya goti Aprili 2018.

Kiungo huyo wa kimataifa wa England aliyeichezea timu hiyo ya taifa mara 32, alianza mechi mbili zilizopita za mabingwa hao wa Ulaya, na alifanyiwa mabadiliko muda wa mapumziko kwenye mechi ya UEFA Super Cup walioshinda dhidi ya Chelsea kabla ya kuisaidia Liverpool kuichapa timu yake ya zamani, Southampton.

Klopp alisema Oxlade-Chamberlain ambaye amecheza mechi mbili za Ligi Kuu msimu uliopita anapaswa kuwa mpole. "Anapaswa kuwa mvumilivu katika njia sahihi, na pia kila kitu kitakuwa sawa kwa asilimia 100," alisema kupitia Liverpool Echo.

"Tunazungumza tu kuhusu Ox kwa sababu kila mmoja anajua ni kwa namna gani alivyo mzuri, lakini tunataka kuhakikisha kwamba anaweza kuonyesha hilo uwanjani pia.

"Huo ni uamuzi wangu, na wakati ninapofanya uamuzi kuwa sasa yupo tayari kisha ni wajibu wangu bila shaka na kijana anapaswa kujaribu kuonyesha ubora wake."

Oxlade-Chamberlain alifanyiwa mabadiliko baada ya kuanza upande wa kushoto dhidi ya Chelsea, wakati aliporudi katika idara ya kiungo dhidi ya timu yake ya zamani, Southampton Jumamosi iliyopita.

Liverpool itaikaribisha klabu nyingine ya zamani ya Oxlade-Chamberlain, Arsenal, Jumamosi katika mchezo ambao ni wa timu mbili pekee zenye rekodi nzuri za kushinda mechi mbili za Ligi Kuu England msimu huu.

## KWA UFUPI

**NEYMAR KWA MKOPO BARCA**
Barcelona inajiandaa kutoa ofa ya kumsajili Neymar, 27, kwa mkopo kutoka Paris St-Germain wiki hii huku kukiwa na kipengele cha kumnunua jumla majira ya joto yajayo. ***(ESPN)***

**JUVE YAANZA KUTETTA NA PSG**
Juventus imefungua mazungumzo na PSG wakati ikiingia katika mbio za kumsajili mshambuliaji Mbrazil Neymar, ambaye alijiunga na klabu hiyo kwa pauni milioni 200 mwaka 2017. ***(AS)***

**GUENDOUZI ATOFAUTISHA NYWELE**
KIUNGO wa Arsenal, Mfaransa Matteo Guendouzi, 20, amedai nywele zake zimekatwa juu zaidi ya mchezaji mwenza wa klabu hiyo, David Luiz. ***(Mirror)***

**VARANE, VINICIUS WATAKIWA PSG**
PSG ipo tayari kumtoa ofa Neymar kwa Real Madrid lakini kwa makubaliano ya kupewa beki wa kati, Raphael Varane, 26, na winga Vinicius Jr, 19. ***(Telefoot, via Sun)***

**ERIKSEN ATAJA ANAZOZITAKA**
NYOTA wa Tottenham na Denmark, Christian Eriksen, 27, anavutiwa na kujiunga na timu tatu pekee, Barcelona, Real Madrid na Juventus. ***(ESPN)***

**LIVERPOOL YAMPOTEZEA VORM**
Liverpool ingemsajili kipa wa Tottenham, Michel Vorm, 35, ambaye amebaki bila klabu baada ya kuachwa majira ya joto yaliyopita. ***(Caught Offside)***

**MUSTAFI KUJIUNGA NA ROMA**
Arsenal inajiandaa kumuacha beki wa kimataifa wa Ujerumani, Shkodran Mustafi, 27, kujiunga na Roma kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu ikitazama kumuuza jumla kwa pauni milioni 23. ***(Forza Roma, via Sun)***

**SOLSKJAER AJIHAKIKISHIA POGBA**
Ole Gunnar Solskjaer ameweka wazi kuwa kiungo wa kimataifa wa Ufaransa, Paul Pogba, 26, hataondoka Manchester United majira haya ya joto. ***(Sky Sports)***

**AUBAMEYANG KUONGEZEWA ULAJI**
Arsenal inajipanga kumuongezea malipo mshambuliaji wake Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang, 30, kwa kumtunuku kutokana na kasi yake ya upachikaji mabao. ***(Telegraph)***

**JUVE KUMCHOMOA MIRANDA BARCA**
Juventus inaandaa ofa ya takriban pauni milioni tisa kwa beki wa kushoto wa Barcelona, Juan Miranda, 19. ***(Mundo Deportivo)***

**CAMAVINGA AZIVUTIA CITY, ARSENAL**
Manchester City, Arsenal na Tottenham zimetuma mashushu wao kwenda kumtazama kiungo Eduardo Camavinga, 16, anayeng'ara Rennes baada ya kuiwezesha kuichapa Paris St-Germain. ***(Mail)***

**BRAVO KUONDOKA MAN CITY**
KIPA raia wa Chile, Claudio Bravo, 36, anajiandaa kuondoka Manchester City mwishoni mwa msimu akiwa mchezaji huru. ***(Sun)***

**CELTIC KUMFUATA IBE**
Celtic ipo tayari kumfuata kwa mkopo nyota wa Bournemouth, Jordan Ibe, 23, kabla ya dirisha la usajili la Scotland kufungwa Septemba 2, mwaka huu. ***(Express)***

**LLORENTE KUJIFUNGA LAZIO**
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Tottenham, Fernando Llorente, 34, anakaribia kujiunga na Lazio kwa uhamisho huru baada ya kuachwa na Spurs majira ya joto. ***(Corriere dello Sport)***

HABARI MICHEZO

# ZFF WAITAKA KMKM KUJIBU KIPIGO ANGOLA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WACHEZAJI wa timu ya soka ya KMKM wametakiwa kuiwakilisha vema Zanzibar katika mechi yao ya marudiano dhidi ya Primeiro de Agosto ya Angola kwa kuhakikisha Jumamosi wanashinda na kusonga mbele kwenye mechi hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

KMKM ambayo inaondoka leo kuelekea nchini Angola, inatarajia kushuka dimbani Jumamosi ikiwa na lengo la kupata ushindi kuanzia mabao 3-0 ili kuweza kusonga mbele kufuatia mchezo wa awali uliopigwa Uwanja wa Amaan kukubali kipigo cha mabao 2-0. Akizungumza na wachezaji wa KMKM wakati wa kuwaaga jana, Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, aliwaambia ushindi wao ndio utakaoweza kuwapa nguvu ya kudai uwanachama wa Shirikisho la Soka Afrika (Caf) ambao kwa kipindi kirefu wanaudai.

Alisema kwa sasa timu yao imekuja kwa wakati mwafaka na ushindi wao ndio utakaokuwa silaha kubwa kwake katika kudai nafasi hiyo.

"Tunahitaji ushindi nendeni kapiganeni, mpo kwenye mashindano ikiwa ni wakati sahihi nendeni kafanyeni kazi," alisema.

Aidha, alisema iwapo watafanikiwa kuwatoa Waangola hao ambao walishawahi kutinga hatua ya nusu fainali mwaka jana, watakuwa wametoboa wingu na kuipatia sifa kubwa Zanzibar.

Alisema katika soka hakuna ugeni hasa wanapokuwa uwanjani, hivyo walikosea katika mchezo wa kwanza ila anaamini wamerekebisha makosa yaliyojitokeza na watakwenda kushinda.

Sambamba na hilo, aliahidi kutoa dola 500 (Sh. milioni 1.1) kwa timu hiyo iwapo itafanikiwa kuitoa Angola katika mchezo huo wa marudiano dhidi ya De Agosto.

Mapema Mkuu wa Utawala wa KMKM, Khamis Taji Khamis aliwataka wachezaji hao waende wakafanye vizuri na wapambane ili washinde, huku wakidumisha nidhamu ya kimchezo na kutunza majukumu yao kama ambavyo walivyoonyesha wapinzani wao walipokuja kwao.

Kwa upande wake kocha wa timu hiyo, Ame Msimu alisema wamejipanga na tayari wamesharekebisha makosa yao.

Alisema mipango yao na mikakati ni kwenda kupata matokeo ugenini kama ambavyo walipata wenyeji wao katika Uwanja wa Amaan.

**NI WETU SASA...**




Mshambuliaji wa zamani wa Simba, Mganda Emmanuel Okwi, akitambulishwa rasmi na viongozi wa klabu yake mpya ya Itthad Alexandria ya nchini Misri na kukabidhiwa jezi namba 19. **PICHA: MTANDAO**

## Cecafa U-20 kupigwa Uganda

**Na Mwandishi Wetu, ASMARA**

BARAZA la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), limesema kuwa mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (U- 20), mwaka huu yamepangwa kufanyika jijini Kampala nchini Uganda.

Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, aliliambia gazeti hili kuwa maandalizi ya mashindano hayo yameshaanza na tayari nchi 10 wanachama zimethibitisha kushiriki michuano hiyo.

Musonye alisema mashindano ya vijana ndiyo yatasaidia kuwaandaa wachezaji wa ukanda huu kupambana na timu kutoka nchi nyingine katika michuano mbalimbali ya kimataifa watakayoshiriki.

**"Baada ya mashindano haya ya U-15, tutaelekea Uganda kwenye michuano ya U-20, tunaamini kupitia programu hizi za mashindano ya vijana, ukanda wetu utanyanyuka na kupambana na timu za ukanda mwingine, hii ndio njia sahihi ya kuandaa vijana, mafanikio hayapatikani kwa ujanja, tuwekeza kwa vijana, mafanikio yataonekana," Musonye alisema.**

Alizitaja nchi zilizothibitisha kushiriki mashindano ya U- 20 kuwa ni pamoja na wenyeji Uganda, Tanzania, Kenya, Rwanda, Eritrea, Sudan, Sudan Kusini, Ethiopia, Somalia na Burundi.

# Tanzania U-15 yaipania Sudan Kusini

**Na Somoe Ng'itu, ASMARA**

USHINDI muhimu! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa timu ya soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 15, Maalim Saleh, ambaye kikosi chake kitashuka kuwakabili wenzao wa Sudan Kusini katika mechi ya Kundi B itakayochezwa leo mchana kwenye Uwanja wa Asmara, Eritrea.

Yosso wa Tanzania watashuka uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya kufungwa mabao 2-0 na wenzao wa Uganda katika mechi ya kwanza iliyochezwa juzi mjini hapa.

Akizungumza na Nipashe mjini hapa, Saleh alisema makosa yaliyojitokeza katika mechi ya kwanza yamefanyiwa kazi na anaamini watafanya vema kwenye mchezo wa leo na kujiweka nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo.

Saleh alisema wamewatazama vema wapinzani wao Sudan Kusini na kuona udhaifu wao, hivyo wanatarajia leo wataondoka na ushindi na kuwapa Watanzania furaha wanayoisubiri kutoka kwa vijana wao.

Kocha huyo alisema hana majeruhi katika kikosi chake na kila mchezaji anataka kuonyesha uwezo wake ili kuipeperusha vizuri bendera ya Tanzania kwenye michuano hii inayofanyika kwa mara ya kwanza kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

"Tumefanya mazoezi vizuri, tumepata muda wa kupitia na kurekebisha makosa yetu, naamini mechi ya kesho (leo), wachezaji wangu watakuwa vizuri na wataongeza umakini, bado ninawaamini wanauwezo wa kupambana na kurejea mchezoni," alisema Saleh. Mechi nyingine ya Kundi B itakayochezwa leo kuanzia saa 10:30 jioni itakuwa ni kati ya Ethiopia dhidi ya yosso wenzao kutoka Rwanda wakati kesho Somalia wataikabili Sudan na jioni Eritrea watawakaribisha Kenya.

Timu mbili zitakazofanya vema katika kila kundi zitatinga hatua ya nusu fainali ambayo itachezwa Agosti 28 na fainali ya michuano hiyo itachezwa Agosti 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Asmara.

Wakati huo huo, Ethiopia ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Sudan katika mchezo mwingine wa Kundi B uliochezwa juzi jioni.

## Savana FC bingwa Mtaa kwa Mtaa Cup

**Na Sabato Kasika**

TIMU ya soka ya Savana FC ya Nachingwea imejinyakulia zawadi ya gari aina ya Noah kwa kuibuka mshindi wa mashindano ya Mtaa kwa Mtaa Cup 2019 yaliyoshirikisha timu 80 kutoka wilaya nne za mkoa wa Lindi.

Fainali ya kombe hilo ilifanyika mwishoni mwa wiki mjini Lindi ikizikutanisha Savana FC na Manchester United ya Wilaya ya Kilwa, ambapo Savana ilipata ushindi wa mabao 2-0.

Baada ya ushindi huo, Savana FC ilikabidhiwa zawadi ya Noah na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Gogfrey Zambi, huku Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango akisema timu hiyo imeitoa kimasomaso wilaya yake.

"Nichukue fursa hii kuwapongeza Savana FC, kwani wametuletea heshima kubwa wana Nachingwea, tukutane tena mwakani tutakapokuwa tunapokea zawadi ya basi, kwani wembe ni uleule," alisema Muwango.

Kwa upande wake mratibu wa mashindano hayo, Hamis Maero, alisema mashindano hayo yalianzia wilayani ambao timu zilishindana huko na kisha mshindi wa kwanza na wa pili wakatinga ngazi ya mkoa kabla ya fainali hiyo kupigwa.

Michezo
Jumatano Agosti 21, 2019
Nipashe



## Klopp: Chamberlain lazima awe mvumilivu

HABARI UK 30

NDIYO ZANGU...




Beki wa kati wa Manchester United, Scott McTominay akiucheza mpira kwa kichwa kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Wolves iliyopigwa Uwanja wa Molineux na kumalizika kwa sare ya bao 1-1 juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# MANARA AFUNGUKA KUTEMWA SIMBA SC

Asema siwezi kuwa msemaji milele, UD Songo kutua nchini Ijumaa huku kiingilio Jumapili kikiwa buku tano...

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya maneno mengi kusambaa kwenye mitandao ya kijamii na vyombo mbalimbali vya habari kuwa Klabu ya Simba imemwajiri ofisa habari mpya kubeba jukumu hilo la Haji Manara, hatimaye msemaji huyo ameamua kufunguka kuhusu hatima yake.

Ni zaidi ya wiki moja sasa imekuwa ikielezwa kuwa Klabu ya Simba imemwajiri Mwandishi Gift Macha wa Azam Media kuchukua nafasi hiyo ya Manara, lakini msemaji huyo aliyejikusanyia mashabiki wengi kwa sasa, amesema nafasi hiyo bado ipo chini yake mpaka sasa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana kuelekea mechi yao ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo ya Msumbiji, waandishi wa habari walitaka kujua kuhusu majaliwa ya yeye kuendelea kukalia kiti hicho kufuatia taarifa zilizozagaa za kuajiriwa kwa mtu mwingine.

Hata hivyo, Manara alisema hawezi kukaa milele katika kiti hicho, lakini kwa sasa yeye bado ni msemaji halali wa timu hiyo mpaka hapo mabadiliko yatakapojitokeza yatawekwa wazi, na kudai hakuna matatizo yoyote kati yake na uongozi.

"Kwenye kiti cha usemaji ndani ya Simba siwezi kukaa milele ipo siku nitakiachia kitakaliwa na mtu mwingine kwa sababu hiki ni kipaji changu mwingine naye atakuja na kipaji chake ila kwa sasa mimi ndiye msemaji halali wa Simba.

"Naomba ifahamike kuwa hii ni taasisi kubwa kuliko mtu, si mimi wala si Crescentius Magori, wote tutaondoka," alisema Manara. Aliongeza kuwa ikitokea Simba imepata msemaji mpya, anaomba mashabiki pamoja na wanachama wampe ushirikiano kama ambavyo wanamfanyia yeye tangu alipopewa wadhifa huo, na akaeleza kushangaa kuona nafasi zimetangazwa nyingi ila ya kwake ndiyo imeleta gumzo.

Kwa upande wa mikakati ya klabu yao kuelekea mchezo wa marudio wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya UD Songo, alisema wapinzani wao wanatarajiwa kuwasili Ijumaa kujiandaa na mchezo wao utakaopigwa Jumapili wiki hii.

Alisema waamuzi wa mchezo huo watawasili kesho, Alhamisi kutoka Rwanda na kudai wachezaji wote wapo vizuri kuelekea mechi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa.

"Maandalizi yetu kuelekea mchezo wa marudio mpaka sasa yamekamilika kwa kiasi kikubwa tunaomba mashabiki na wanachama wetu wajitokeze kwa wingi uwanjani kuipa sapoti timu yetu,"alisema Manara.

Aidha, Manara alisema tiketi za mchezo huo zitaanza kuuzwa kesho katika vituo ambavyo watavitangaza ikiwa ni pamoja na kutumia gari maalum ambalo litawasaidia watu wengi kununua tiketi kwa urahisi.

Alitaja viingilio vya mtanange huo utakaopigwa majira ya saa 10:00 alasiri kuwa kwa upande wa VIP A (Platnum Plus) tiketi zitakuwa Sh. 150,0000 na Sh. 100,000 kwa Platnum, huku VIP B na C zikiuzwa kwa Sh. 15,000 wakati mzunguko ikiwa ni Sh. 5,000.

Simba inahitaji ushindi wowote ili kusonga mbele kufuatia mechi ya awali iliyopigwa Beira, Msumbiji kulazimisha sare tasa, na endapo itafanikiwa kusonga mbele itakutana na mshindi wa jumla kati ya FC Platinum ya Zimbabwe na Nyasa Bullets ya Malawi.

# Yanga na mkakati mzito wa ushindi

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA mechi yao ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi ugenini dhidi ya Township Rollers, Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera amewatoa hofu mashabiki kuhusu kupata matokeo, huku uongozi ukiomba sapoti kubwa kutoka kwa Watanzania waishio Botswana.

Akizungumza na Nipashe jana moja kwa moja kutoka Botswana, Makamu Mwenyekiti wa timu hiyo, Frederick Mwakalebela, alisema, wameanza kufanya mazoezi kwenye uwanja ambao watautumia siku ya mechi na wachezaji wote wana ari kubwa ya ushindi.

**"Tayari tumeanza mazoezi kwa ajili ya mchezo wa Jumamosi, lengo ni kuhakikisha tunavuka hatua hii na kuweza kusonga mbele," alisema na kuongeza kuwa jana mchana walifanya mazungumzo na Watanzania waliopo nchini humo, kwa lengo la kupanga mikakati ya ushindi.**

Alisema kocha Zahera amesema anataka kufika mbali katika michuano hiyo licha ya kuwa na ushindani mkubwa.

"Zahera amesema atahakikisha tunarudi na matokeo mazuri nyumbani kikubwa anaomba dua za Watanzania," alisema Mwakalebela.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >